**MKUTANO WA NANE**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 13 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:**

Taarifa ya Kamati ya uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 203

**Uboreshaji wa Sheria za Serikali za Mitaa**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (K.n.y. MHE. KABWE ZUBERI ZITTO)** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda, katika ziara yake Wilayani aliahidi kuboresha Sheria za Serikali za Mitaa ili Halmashauri ziwajibike, kwa mfano, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha kuwa Diwani kutoka kwenye (*Minority Party*) kwenye Halmashauri husika.

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya kufanya mabadiliko katika Sheria Namba 7, 8 na 9 za *Local Government Arts*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kogoma Kaskazini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inazingatia marekebisho ya Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287, 288 na 290 za Toleo la mwaka 2002 (awali Sheria Namba 7,8 na 9 za Mwaka 1982) kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea ya Kisera, Kiuchimi na Kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kamati za Halmashauri, Muundo wa Kamati za Halmashauri umeelezwa kwa ufasaha katika Kanuni za Kudumu za Halmashauri (*Council Standing Orders*) ambazo hupitishwa na Halmashauri na kuidhinishwa na Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa. Kanuni za Kudumu hizo zinaeleza kuwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha ni Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Halmashauri pamoja na Mbunge anayewakilisha Jimbo.

Aidha, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ni Mwenyekiti wa Halmashauri au Meya kwa kadri itakavyokuwa. Hata hivyo, kwa kuwa suala la Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha halimo katika Sheria za Serikali za Mitaa, Serikali haina mpango wa kurekebisha Sheria ili kumwezesha Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha atoke kwenye Chama chenye Wajumbe wachache yaani (*Minority Party*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuzifanyia marekebisho Sheria za Serikali za Mitaa, pendekezo la Mheshimiwa Mbunge haliwezi kutekelezwa kwa sababu Mwenyekiti wa Halmashauri huchaguliwa na Madiwani wote. Kwa hiyo, kumtaka moja kwa moja kwamba Mwenyekiti wa Kamti ya Fedha atoke kwenye *Minority Party* ni kuwanyima Madiwani haki yao ya Kidemokrasia ya kumchagua Mwenyekiti wao wa Halmashauri. *(Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, uzoefu wa Bunge letu pamoja na uzoefu wa Mabunge ya Jumuiya za Madola yaani *Common Wealth* unaonyesha kwamba masuala ya fedha yanaposimamiwa na chama kisichoko madarakani usimamizi unakuwa thabiti zaidi. Je, Mheshimiwa Waziri atakubali sasa kwamba pamoja na kwamba suala la Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha halipo kwenye Sheria lakini kwenye Kanuni kwamba

Taratibu zote na Sheria zote na Kanuni hizo zitarekebishwa ili kupata manufaa ya *Watch Dog Committee* ambayo ni Kamati ya Fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, swali la msingi liliuliza maeneo mapana zaidi ya marekebisho ya Sheria hii na kwa kuwa Waziri amejikita tu katika kujibu eneo la Kamati ya Fedha.

Je, Waziri atakubali kwamba mabadiliko aliyoyaeleza ya Kiuchimu, Kijamii na Kisiasa yamekuwa ni makubwa sana katika nchi yetu kiasi kwamba Sheria nzima Namba 7, 8 na 9 sasa zinahitaji kuangaliwa upya? Kwa mfano ukiangalia fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri sasa ni nyingi mno kuliko wakati wowote ule katika historia ya nchi yetu na kwa maana hiyo basi Halmashauri zinahitaji kuimarishwa kwa njia ya Sheria zetu mbalimbali.

Je, Waziri atakubali kwamba sasa wakati umefika wa kuleta mabadiliko haya ili kuyachukua haya mabadiliko makubwa katika nchi yetu ?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Wilbrod P. Slaa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba vyama vya upinzani vikisimamia masuala ya fedha ndiyo vinafanya vizuri zaidi, *otherwise* kama Mheshimiwa Mbunge anaweza akanipa *data* za kikamilifu kuonyesha kwamba kweli sehemu ambazo zinasimamiwa na vyama vya upinzani Serikali inafanya vizuri zaidi. Mimi nafikiri ni wajibu wetu wote kama Viongozi na kama Wabunge kusimamia vizuri mambo ya fedha.

Kwa upande wa suala la kubadilisha Sheria Namba 7, 8 na 9. Ni mwaka jana tu mwezi Desemba Sheria hizo ziliIetwa hapa Bungeni na Bunge lako Tukufu limefanya marekebisho mbalimbali na kama nilivyosema kwamba Sheria hizo zinabadilishwa au zinarekebishwa kulingana na mabadiliko ya Kisiasa, Kiuchimi na Kijamii. Sasa kipindi cha miezi sita tu Sheria hizo zimebadilishwa, ni kitu gani Waheshimiwa Wabunge ambacho kimebadilika kwa muda wa miezi sita ambacho kinahitaji marekebisho kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo hayo ya Mheshimiwa Mbunge yatazingatiwa kulingana na mabadiliko niliyoyasema kwa muda muafaka kama jamii itaona kwamba kuna ulazima wa kufanya mabadiliko haya. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Lakini swali la kwanza la Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Utaratibu wa Kimataifa ni Kamati *Watch Doc Committee* kama *Public Accounts Committee* yaani *LAAC* ndiyo zinasimamiwa na *Opposition* na siyo Kamati ya Uchumi na Mipango. Kwa hiyo, nadhani hii tuiweke sawa. (*Makofi*)

Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili.

Na. 204

**Posho ya Mafunzo kwa Wenyeviti wa Mitaa**

**MHE. RIZIKI O. JUMA (K.n.y. MHE. NURU AWADHI BAFADHILI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji wanafanya kazi kwa niaba ya Halmashauri zao na kwa kuwa, Wenyeviti hao wanafanya kazi bila ya kupata mafunzo yoyote:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mafunzo Wenyeviti hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani w akutoa posho kwa Wenyeviti hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiwapa mafunzo Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji ili kuwajengea uwezo na kuboresha utendaji wao. Wenyeviti waliochaguliwa mwaka 2004 wamepata mafunzo kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006. Ofisi yangu iliandaa mafunzo kwa Wenyeviti wapya kwa kuanzia katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Rukwa na Mtwara ambapo Wenyeviti wa Mitaa 178 walipatiwa mafunzo wakiwemo 76 kutoka Mkoa wa Tanga. Mafunzo hayo yalifanyika mwezi Oktoba, 2006. Mafunzo haya yataendelea kutolewa kwa awamu Tanzania nzima.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Nuru Bafadhili kuwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanafanya kazi kubwa ya kusimia shughuli za Maendeleo katika maeneo yao. Katika Mkutano wa tatu na saba wa Bunge lako Tukufu nilijibu maswali ya Waheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala na Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye Mbunge wa Biharamulo Magharibi yanayohusiana na Posho ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Nililifahamisha Bunge kwamba katika tangazo la Serikali Namba tatu (3) la tarehe 7 Januari, 1994 Halmashauri zote nchini zilielekezwa kuwalipa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji si chini ya asilimia tatu (3%) ya makusanyo ya vyanzo vya mapato alivyohamasisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kufuta kodi zenye kero na ambazo baadhi zilikuwa ni vyanzo vya mapato ambayo Halmashauri zetu bado kuna vyanzo vya mapato ambavyo Halmashauri zetu zinawajibika kuyakusanya. Aidha, kwa kutumia vema fedha za fidia ya vyanzo vya mapato. Halmashauri zina uwezo wa kuwalipa posho Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kwa kiwango vinavyostahili. Aidha, zipo Halmashauri

ambazo zinatekeleza agizo hili kikamilifu. Mifano michache ya Halmashauri hizo ni kama ifuatavyo: Ilala Manispaa inalipa shilingi 20,000/= kwa mwezi, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba shilingi 5,000/= kwa mwezi, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma (Ujiji) shilingi 10,000/= kwa mwezi na Halmashauri ya Mji Korogwe shilingi 15,000/= kwa mwezi. Kwa hiyo, nasisitiza Halmashauri nyingine pia zizingatia maelekezo ya Serikali kama nilivyoagiza hapo awali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, swali moja la nyongeza tafadhali.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize na mimi swali moja la nyongeza. Kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Kwa kuwa, jibu lake linaonyesha kwamba Halmashauri nyingi sana zinatofautiana kutegemeana na mapato katika kuwalipa hao Wenyeviti na Wenyeviti wa Vitongoji ambao wanafanya kazi nzito na muhimu sana na ndiyo nguzo ya Maendeleo katika nchi yetu.

Je, haingekuwa vema kwa vile kuna fedha ambazo zinatoka Hazina za kila Halmashauri ambazo zinarudishiwa au zinarejeshewa kwa kila Halmashauri, haingekuwa vizuri kwa TAMISEMI kuweza kuweka *uniform* au fedha ambazo ni sawa kwa nchi kwa Wenyeviti na kukata fedha moja kwa moja na kuwapelekea Wenyeviti hao wa vitongoji bila usumbufu huu kwa kila Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benedict K. Losurutia kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi nchi yetu ina vitongoji vipatavyo 57,000, Mitaa 1,756 na Vijiji zaidi ya 10,000 vyote hivyo ukijumlisha unapata karibu 68,993. Sasa hata ukisema uwalipe hao kwa kukata fedha zile ambazo ni za fidia fedha hizo hazitoshi kwa sababu fedha hizo zina mambo mengi ya michango katika Halmashauri zetu hizohizo. Ndiyo maana tumeagiza kwamba kila Halmashauri iangalie uwezekano wa kuwalipa hao Wenyeviti wa Mitaa kulingana na mapato yao. Halmashauri nyingi zina mapato yao ambayo siyo lazima wategemee Hazina kwa mfano *Property Tax* katika sehemu za mijini wanaweza wakawalipa Wenyeviti hao kulingana na mapato yanayotoka katika mitaa yao. Kwenye vijiji vilevile kuna fidia mbalimbali kwa mfano zile za uwindaji na mapato mbalimbali, hivyo ndivyo tunavyosema kwamba wawalipe siyo rahisi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa kuchukua hela hizo na kuanza kuwalipa moja kwa moja Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara inayofuata nayo ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, swali tafadhali!

Na. 205

**Umeme Jua kwa Ajili ya Zahanati Vijijini**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:

Kwa kuwa, mwaka jana Serikali ilitamka kwamba, Mfuko wa Bill Clinton, umekubali kutoa umeme wa jua kwa ajili ya Zahanati za Vijijini:

(a) Je, lini mpango huo utaanza?

(b) Je, Zanahati za Iguguno, Kinyangiri, Kibonda, Msingi, Gumanga, Kinandili, Nguguti, Malaja, Mwangeza, Munguli, Manela, Kvuni, Ikolo na kadhalika zilizoko Iramba Mashariki, zimejumuishwa kwenye mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Ni kweli Serikali ilitamka ahadi ya Rais Mstaafu wa Marekeni Bill Clinton ya kuweka mfumo wa Umeme – jua kwenye Zahanati na Vituo vya Afya vya Vijijini ambao utafadhiliwa na Mfuko wake, yaani *Clinton HIV/AIDS Foundation*. Wizara tayari imeandaa madodoso na kuyatuma kwenye Halmashauri za wilaya zote ili kupata taarifa sahihi za Zahanati na Vituo vya Afya vyote; madodoso haya ayatasaidia katika kuandaa mpango wa utekelezaji. Kila Wilaya imeagizwa ilete idadi ya Zanahati katika wilaya na umbali wa kila Zahanati na Kituo cha Afya kutoka umeme wa *Grid* ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huu utapangwa katika awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Vituo vilivyo mbali zaidi na umeme wa *grid* ndivyo vitakavyopewa kipaumbele wakati wa Kufunga umeme – jua. Aidha, ugumu wa mawasiliano katika eneo husika, ukubwa wa eneo, idadi ya wakazi na aina ya huduma zinazotolewa katika kituo (Kwa mfano upasuaji) ni baadhi ya mambo yatakayozingatiwa wakati wa kupanga kipaumblele kituo kipi kianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, majaribio ya mpango huu tayari yamekwisha fanyika katika Vituo vya Afya vitano na Zahanati moja katika Wilaya za Masasi na Nanyumbu Mkoani Mtwara.

Baada ya maelezo haya sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, mradi huu kwa sasa upo katika hatua ya upembuzi yakinifu. Aidha, kutokana na uzoefu uliopatikana Mtwara, inatarajiwa kuwa utekelezaji wa mpango huu utaanza katika mwaka 2007/2008 iwapo pesa, vifaa na mafundi mchundo wa kutosha watapatikana kwa wakati.

(b) Kwa kuwa, mradi huu ni wa nchi nzima, ni dhahiri kwamba Zahanati za Iguguno, Kinyangiri, Kibonda, Msingi, Gumanga, Kinandili, Nguguti, Malaja, Mwangeza, Munguli, Manela, Kivumi,Ikolo na kadhalika zilizopo Iramba Mashariki pamoja Vituo vya Afya vitafaidika na mpango huu iwapo vitakidhi mahitaji na sifa ya kupatiwa umeme wa jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu namwomba Mheshimiwa Mgana I. Msindai, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wafuatilie na kuhakikisha kuwa Waganga Wakuu wa wilaya wamewasilisha Wizarani madodoso ya Zahanati na Vituo vya Afya vyote katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Swali la Nyongeza Mheshimiwa Mgana I. Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa, hizi Zahanati zote nilizozitaja ziko mbali na umeme wa grid na kwa kuwa Iramba Mashariki tuna Vituo vya Afya vitatu yaani Kinyangiri, Mkarama na Ikolo. Je, Waziri atavipa kipaumbele hivi vijiji ili viweze kupata umeme kama vile vya Masasi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgana I. Msindai kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba vile Vituo ambavyo viko mbali na *Grid* ya Umeme ndiyo vitakavyopewa kipaumbele na vilevile nilisema kwamba nimeomba kwamba Mheshimiwa Mgana I. Msindai atusaidie ili Wilaya yake iweze kuleta madodoso na kwamba kama wenyewe watajumuisha hivi Vituo vya Afya alivyoviongeza hapa hakuna tatizo kwamba tunaweza tukaingiza katika Mfuko huo.

Lakini ninachosema ni kwamba madodoso kama yatakidhi yale maagizo tuliyoweka na kama vituo vyao vinakidhi basi hakutakuwa na tatizo la kupatiwa umeme.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata katika Wizara hiyo Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika.

Na. 206

**Kuongezeka kwa Watoto Wenye Mtindio wa Obongo Nchini**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la kuzaliwa kwa watoto wenye mtindio wa Ubongo au wale walifanana nao linaongezeka siku hadi siku na kufanya idadi ya watoto wa aina hiyo kuwa kubwa.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza tatizo hili linasababishwa na nini?

(b) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti kuhusiana na tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa kama ifuatavyo:-

(a) Zipo sababu nyingi ambazo zinaweza kusababisha mtindio wa ubongo kwa watoto. Aidha, kwa Tanzania sababu kuu mbili ni:-

Kwanza, kuchelewa kulia mara wanapozaliwa.Hiii inatokana na matatizo mbalimbali yaliyompata Mama wakati wa kujifungua, kwa mfano uchungu kuchukua muda mrefu na hivyo kusababisha watoto wanaozaliwa kukosa hewa kwenye ubongo. Hali hii husababisha athari inayomfanya mtoto aathirike kiakili na kimakuzi. Sababu kuu nyingine inayosababisha watoto kupata mtindio wa ubongo ni degedege hasa linaporudiarudia au kuchukua muda mrefu. Mtoto anapopata degedege kwa muda mrefu au mara kwa mara hufanya ubongo kukosa hewa na kuleta madhara ambayo yanaweza kuleta madhara ambayo yanaweza kuleta utindio wa ubongo. Hii huwapata zaidi watoto wenye umri chini ya miaka mitano ambao bado ubongo wao unakua. Kwa Tanzania degedege husababishwa zaidi na malaria.

(b) Serikali kwa kushirikiana na Vyuo vya Tiba pamoja na wadau mbalimbali kwa nyakati tofauti imefanya tafiti kuhusu suala hili. Matokeo ya tafiti hizi yametumika katika kubuni mbinu na mikakati mbalimbali ya kupambana na tatizo hili. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(1) Kuwahimiza kina Mama Wajawazito kuhudhuria kliniki ipasavyo na kupata huduma zinazotakia ikiwa ni pamoja na kutambua viashirio vya hatari.

(2) Kuhamasisha jamii hususani akina Baba kufanya maandalizi kwa ajili ya Mama kujifungua katika Vituo vya Afya ikiwa ni pamoja na kujiandaa endapo rufaa itahitajika.

(3) Kuwa na Vituo vya Afya vya kutosha karibu na wananchi wenye vifaa na wafanyakazi wenye ujuzi wa kutosha.

(4) Kuelimisha jamii na watoa huduma kuhusu huduma mahususi za watoto wachanga (*Essential Newborn Care*).

(5) Kuzuia Malaria kwa watoto chini ya miaka mitano, hasa kwa kutumia vyandarua vyenze viuatilifu.

(6) Kuwapeleka watoto mapema kwenye Vituo vya Afya mara wanapoonyesha dalili za kuumwa na hasa wanapopata degedege.

(7) Kutoa elimu kwa jamii na watoa huduma kuhusu mambo muhimu ya kufanya kwa ajili ya afya, malezi na Maendelao ya mtoto (*Community (IMCI*).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, swali la nyongeza.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza. Zamani ilikuwa hakuna maradhi ya mara kwa mara ya degedege, lakini sasa hivi kila mara mtoto anapata maradhi haya ya degedege. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchunguza ni chanzo gani hasa kinacholeta matatizo haya?

**NAIBU SPIKA:** Swali zuri sana, Majibu mafupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Si kweli kwamba zamani haikuwa inatokea magonjwa ya degedege, ukweli ni kwamba sasa hivi Vituo vya Afya na Huduma za Afya zimeongezeka na watu au jamii imeelimika ndiyo maana watoto wanapelekwa hospitali na hapo wanaweza kuonekana kwamba wamepata degedege. Lakini kusema kwamba zamani walikuwa hawapati degedege hilo sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea swali katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage.

Na. 207

**Wakulima Wadogowadogo Wanaokizunguka Kiwanda cha Miwa cha Kagera**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:

Kwa kuwa, ni ukweli usiofichika kuwa kabla ya kuuzwa kwa kiwanda cha sukari cha Kagera, wakulima wadogowadogo waliokuwa wamekizunguka kiwanda hicho walikuwa wanapata riziki zao kwa kilimo cha Miwa na kwa kuwa, kiwanda hicho kimebinafsishwa na maeneo hayo yamehodhiwa na kiwanda.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wadogowadogo kuendelea na kilimo cha miwa na kuuza miwa kiwandani hapo kama wafanyavyo wenzao wa Kilombero na Mtibwa?

(b) Je, Serikali inasemaji kuhusu mmiliki wa kiwanda cha sukari cha Kagera kuhodhi eneo lote lililokuwa linatumiwa na Wakulima wadogo na kuwaacha wananchi bila eneo la kulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Savelina S. Mwijage (Viti Maalum) Kabla ya kubinafsishwa Kiwanda cha Sukari cha Kagera kilikuwa kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 89.95, na Kampuni ya *Kagera Mills*

*Limited* asilimia 10.5. Aidha, miwa yote iliyokuwa ikisagwa kiwandani ilitoka kwenye mashamba ya kiwanda kwa sababu hakukuwa na wakulima wadogo waliokuwa wakikiuzia kiwanda hicho, kama ilivyokuwa kwa wakulima wa Kilombero na Mtibwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na mwekezaji katika Kiwanda cha Sukari cha Kagera inatekeleza mpango wa kuendeleza kilimo cha mkataba (*contract farming*). Kuanzia mwaka 2004/2005 hadi 2006/2007 jumla ya wakulima wadogo wa miwa 300 wanaoishi karibu na kiwanda hicho wamepatiwa mafunzo kuhusu kilimo bora cha miwa kupitia Chuo cha Sukari cha Kidatu. Lengo ni kuwafundisha wakulima 2000 ifikapo mwaka 2010.

Aidha, Kiwanda cha Kagera kimeagiza tani 30,000 za mbegu kwa ajili ya mashamba ya kiwanda na yale ya wakulima wadogo. Wakulima wadogo wameandaa eka 250 kwa ajili ya kilimo cha miwa na tayari eka 60 zimekwishapandwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi, miwa yote iliyokuwa ikisagwa kiwandani kabla ya ubinafsishwaji ilitoka kwenye mashamba ya kampuni na hakukuwa na wakulima wadogo waliokuwa wakikiuzia miwa kiwanda hicho. Aidha, mwekezaji wa Kiwanda cha Kagera hajahodhi eneo la wakulima wadogo kama inavyodaiwa. Baada ya ubinafsishaji wa kiwanda cha Kagera, kinachofanyika sasa ni kuwahimiza wakulima wadogo washiriki katika kilimo cha miwa na kuwapatia mafunzo kuhusu kilimo bora cha miwa, ili washiriki katika uzalishaji wa miwa na kukiuzia kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya hekta 27,500 zilizopo na zinazofaa kwa kilimo cha miwa wakulima wadogo wanamiliki hekta 7,500 wakati mwekezaji anamiliki hekta 20,000. Kinachosisitizwa ni ushirikiano mzuri kati ya mwekezaji, wakulima na Serikali ili pande zote zishiriki kikamilifu hususan katika kuweka bei nzuri ya miwa na kufanya malipo mapema kabla ya msimu.

Aidha, kwa eneo linalolimwa na wakulima, Serikali, kupitia Bodi ya Sukari na Halmashauri ya Wilaya itaangalia uwezekano wa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na barabara za kutoa mazao shambani chini ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya *(DADPs).*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba na utendaji uwepo. Baada ya hapo naomba niulize swali moja. Je, kwa kuwa hawa wananchi wakulima wadogo wadogo wameshajiandaa kuwa na semina ya kuboresha kilimo chao. Serikali katika Bajeti hii imewasaidiaje kwa sababu Serikali ya sasa hivi ya Awamu ya Nne yenye kasi mpya na nguvu mpya inajitahidi kuboresha wakulima. Naomba jibu Bajeti hii

imetenga shilingi ngapi ili kuweza kuwaboresha hawa wakulima wadogo wadogo wa miwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme utendaji upo mzuri katika Kiwanda na katika Bodi ya Sukari. Pili, kwa sasa hivi siwezi kutoa *data* kwamba tumetenga shilingi ngapi kwa ajili ya hizo semina. Lakini nimeshasema semina zipo na tutaendelea kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo na kwa kuanzia Bodi ya Sukari imeshatoa mafunzo kwa wakulima mia tatu na tayari kwa kusaidiana na kiwanda zimeshalimwa hekta 200 na 60 zimeshapandwa tayari. Ndiyo utendaji wenyewe huo, kuongeza uzalishaji. Lakini pia kama nilivyosema kwamba tunataka tuhamasishe kilimo cha *contractor farming* wakulima wale wataorodheshwa na Bodi ya Sukari ili wafahamike na Kiwanda cha Sukari pia kitawapa mikataba ili waweze kuuza miwa yao pale. Kitu ambacho tunasema tunachokikataa ni kwamba yale mashamba yalikuwa yanamilikiwa na kiwanda, hayakuwa yanamilikiwa na watu binafsi. Kwa hiyo maeneo yale yote ambayo yalikuwa yanamilikiwa na kiwanda, kiwanda kitaendelea. Lakini pia wakulima watasaidiwa katika kuongeza uzalishaji.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Bukoba katika kushughulikia suala la mradi wa miwa inafanana sana na Halmashauri yangu ya Wilaya ya Songea Vijijini ambayo imeamua kwa dhati kabisa kuanzisha zao la miwa kama zao la biashara kwa wananchi wa Kata zote 14 za Jimbo la Peramiho na kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameonyesha juhudi ya pekee ya Bodi ya Sukari pamoja na Wizara kuandaa mafunzo maalum kwa ajili ya wakulima hao wadogo wadogo. Je, katika mpango huo wa mafunzo maalum ya kuendeleza zao la miwa katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini, wakulima hao wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Jimbo la Peramiho katika Kata zote 14 nao wataingizwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ya CCM inahimiza kilimo na kuongeza mapato kwa wakulima nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba tutaangalia uwezekano wa kuingiza wakulima katika Kata zake 14 hizo katika mafunzo hayo na kuwawezesha kwa namna moja au nyingine katika kuongeza uchumi wao.

Na. 208

**Utekelezaji wa Programu ya *National Rural Water Supply and Sanitation***

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Kwa kuwa chini ya Programu ya Serikali ijulikanayo kama *National Rural Water Supply and Sanitation Programme* Vijiji vinne vya Jimbo la Mwibara vitapatiwa maji katika mwaka huu wa fedha:-

(a) Je, ni kwa nini utekelezaji wa program hiyo haujaanza Mwibara?

(b) Je, miradi hiyo ilipangiwa kuwa imekamilika ifikapo lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kajenge, Mbunge wa Jimbo la Mwibara, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Nabu Spika, Serikali imekamilisha maandalizi ya programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo utekelezaji wake kwa kipindi cha 2006 – 2010 utahitaji kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 951. Hivyo, Serikali imefanya majadiliano na wafadhili mbalimbali kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo. Mikataba kati ya Serikali na Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kutoa fedha za programu tayari imesainiwa. Mchakato wa kujadiliana na wafadhili hadi kufikia hatua ya mikataba kusainiwa umechukuliwa muda mrefu kuliko tulivyotarajia.

Hata hivyo, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa fedha kwa ajili ya miradi midogo midogo (*quick wins*) zimepatikana ambapo jumla ya Halmashauri 84 zilizokidhi masharti ikiwemo Halmashauri ya Bunda zimetumiwa fedha na zimekiri kupokea fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye utangulizi, utekelezaji wa programu hii nchini, ikiwa ni pamoja na katika vijiji vinne vya Jimbo la Mwibara umechelewa kuanza kwa sababu Serikali ilikuwa kwenye mchakato wa kutafuta fedha za kutekeleza programu hii yenye mahitaji makubwa ya fedha. Makubaliano yamefikiwa kati ya wafadhili mbalimbali na Serikali na baadhi ya mikataba imesainiwa. Hivyo utekelezaji wa programu utaanza mwaka 2007/2008.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi hii umegawanyika katika aina mbili. Aina ya kwanza ni ile miradi midogo midogo (*quickwins*) ambayo haihitaji usanifu. Aina ya pili, ni mradi ya Vijiji 10 vilivyopendekezwa kutoka katika kila Wilaya, vikiwemo vijiji hivyo vinne vya Jimbo la Mwibara. Miradi hii kabla ya kuanza ujenzi katika vijiji vilivyopendekezwa na Wilaya, upimaji na usanifu utafanyika. Baada ya hatua hiyo kukamilika, makabrasha ya zabuni yataandaliwa kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kujenga miradi. Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kuchukua miaka mitatu tangu hatua ya upimaji na usanifu hadi kukamilisha ujenzi wa miundombinu.

Hata hivyo, utekelezaji utategemea kasi na uwezo wa Halmashauri ya Wilaya katika kutekeleza miradi.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Wakati nikipitia katika vitabu vya *vote* za miradi niliona kuna baadhi ya mikoa ambayo imeshatengewa pesa kwa ajili ya mradi huo, lakini Mkoa wa Mara haujatengewa. Sasa naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kama miradi hii katika Jimbo la Mwibara na Mkoa wa Mara ni tofauti na miradi ambayo ipo katika Mikoa mingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika vitabu hivi vya Bajeti kuna *vote* katika kila mkoa na katika *vote* hizo miradi hiyo ni ruzuku ambayo inatoka Serikalini, Hazina moja kwa moja kupelekwa katika kila mkoa na hiyo haina uhusiano na Wizara yangu ya maji kwamba ndiyo imetayarisha hizo. Hizo ni *vote* kutoka Hazina na namwomba Mheshimiwa Mbunge wakati wa kujadili hotuba yetu ya Wizara ya Maji basi jambo hilo pia tutalipatia ufafanuzi zaidi kutoka kwa wenzetu wa Hazina.

Na. 209

**Umeme - Upatikanaji Umeme**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania *(TANESCO)* lilichimbia nguzo za umeme kwa takriban miaka mitano sasa kutoka Ruanda, Iyula hadi Idiwili na kutoka Vwawa – Kijiji cha Hasamba lakini hadi sasa hakuna chochote kinachoendelea:-

(a) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa maeneo hayo ambao walipewa matumaini ya kupatiwa umeme kwa muda mrefu sasa?

(b) Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususan wa Kata za Isansa, Msia, Halungu, Itaka, Nambinzo na Nyimbili wako tayari kutumia umeme kwa Maendeleo yao: Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa maeneo hayo ambayo ni maarufu kwa uzalishaji wa zao la kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NAMADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Godrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia Shirika la *TANESCO* ilibuni mpango wa kuwapatia wananchi wa maeneo ya Ruanda, Lyula, Vwawa na Hasamba umeme kwa kuweka utaratibu wa kutenga fungu kidogo kidogo kila mwaka ili kutekeleza sehemu ya kazi katika miradi miwili ya Ruanda – Lyula na Vwawa – Hasamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Ruanda – Lyula umefanyiwa tathmini na gharama yake ni Sh. 560,000,000/=. Kazi ambazo tayari zimefanyika ni pamoja na usimikaji wa nguzo za njia kubwa ya umeme ya kilovoti 33 kwa urefu wa kilomita 26. Jumla ya zaidi ya Sh. 380,000,000/= zinahitajika kwa ajili ya kukamilsha utekelezaji wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mradi wa Vwawa – Hasamba umefanyiwa tathmini. Mradi huu una gharama ya Sh. 300,000,000/=. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kusimika nguzo za njia kubwa ya umeme ya kilovoti 33 kwa urefu wa kilomita tano. Jumla ya zaidi ya Sh. 284,000,000/= zinahitajika kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa Serikali na hali mbaya ya kifedha inayoikabili *TANESCO* utekelezaji wa miradi hiyo miwili ulisimama kutekelezwa na utaendelea kutekeleza mara fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilipoanza kuweka nguzo ilikuwa na nia haswa ya kukamilisha miradi ya kupeleka umeme Ruanda, Lyula, Vwawa na Hasamba. Tunawapongeza wananchi wa maeneo yaliyowekwa nguzo bila huduma ya umeme kukamilika kwa kuwa wavumilivu hadi sasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kujua umuhimu wa kuwapatia umeme wananchi wa Kata ya Usanza, Msia, Halingu, Itaka na Nabinzo Serikali ina dhamira ya kumalizia miradi ambayo tayari imeshaanza kama niliyoitaja kabla ya kufikiria kuanzisha miradi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano wake na Wizara yetu na tunamwomba tuendelee kusaidiana kuwashauri wananchi wa maeneo mengine katika Jimbo lake ambao hawajapatiwa huduma ya umeme kwamba Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha ili iwe na uwezo wa kutekeleza miradi ya umeme iliyoanzishwa na mingi zaidi nchini.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yasiyo na matumaini sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili madogo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niseme kwamba, hawa wananchi siyo wavumilivu ndiyo sababu kwenye Kijiji cha Ihula kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita walichagua Mpinzani na siyo wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa sababu ya ahadi hizi za Serikali ambazo hazitekelezeki.

Sasa swali, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atusaidie kwamba kwa sababu hizi nguzo zimechimbiwa tangu mwaka 2003 na tangu mwaka huo Serikali imekuwa inaahidi kwamba tutatekeleza mwaka ujao wa fedha, mwaka ujao wa fedha na mimi mwenyewe nimeahidiwa hivyo kwenye Bunge hili mwaka jana. Sasa wananchi hawa wawe wavumilivu mpaka lini? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi tunatumia pia umeme wa gridi wa kununua kutoka Zambia na kwa kuwa kumekuwa na matatizo ya kukatikakatika kwa umeme sana katika Wilaya nzima ya Mbozi kwa maana ya Miji ya Tunduma, Vwawa na Mloo.

Je, Serikali inatamka nini kuhusu kutuingiza kwenye gridi ya Taifa ambako inaonekana umeme umetulia zaidi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NAMADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kaka yangu kwamba dhamira yake kama mwakilishi wa wananchi wa Mbozi Mashariki na dhamira ya wananchi wa Mbozi Mashariki na dhamira ya Serikali ni moja kuhakikisha kwamba tunatoa huduma kwa kiwango kinachokubalika kutokana na upatikanaji wa fedha kadri itakavyowezekana.

Kwa hiyo, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kushirikiana, tupo pamoja na kwa kweli inakuwa vigumu kusema uvumilivu uendelee mpaka lini, lakini ambacho naweza kumwambia ni kwamba Serikali ina mikakati sasa hivi wa kutekeleza usambazaji wa huduma vijijini kupitia wakala wa umeme vijijini.

Tuna hakika kwa sababu mradi huu ni kati ya miradi ambayo imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, gharama zake zinafahamika na kwa ushirikiano ambao Mheshimiwa Mbunge amekuwa nao na Wizara yetu nina hakika kwamba miradi yake itakuwa mstari wa mbele mara pesa zitakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwamba maeneo ya Jimbo lake yanapata huduma kutoka kwenye umeme ambao unatokea Zambia na umekuwa na matatizo. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba mpango upo na tutaendelea kuboresha huduma zetu na hasa mradi wa umeme unaotokea Zambia tutaendelea kuuboresha kwa nguvu kubwa zaidi.

Lakini niseme tu kwamba kwa jinsi ambavyo tunaendelea kutanua huduma za *National Grid* kwa maana ya hii huduma kubwa inayotoka kwenye msongo mkubwa wa Taifa itakapokuwa inazidi kuimarika uhakika wa kupata umeme kwa wananchi wa Jimbo la Mbozi Mashariki ambalo Mheshimiwa Mbunge analiwakilisha ni mkubwa hasa kwa kuzingatia mambo mawili kwamba upanuzi wa *grid* ya Taifa lakini pia usambazaji wa huduma za umeme vijijini.

Na. 210

### Mahitaji ya Umeme – Shule za Sekondari Singida

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kupeleka umeme kwenye shule za sekondari za Murigha *Girls*, Kinyeto, Ngimu, Mugori, Merya, Maghoja na Ughandi na kwa kuwa shule hizo zote ambazo ziko katika Jimbo la Singida Kaskazini hazina umeme na kwa hali hiyo imeathiri Maendeleo ya elimu kwa wanafunzi wa shule hizo:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye shule hizo na kwenye vijiji jirani na shule hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa elimu ni msingi wa Maendeleo katika jamii. Taasisi za elimu vikiwemo vyuo, mashule na vituo vya elimu ni maeneo mahsusi kwa utoaji wa elimu. Taasisi za elimu zikiwa na umeme weye uhakika zinatoa elimu kikamilifu na wanafunzi wanaweza kujisomea kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upelekaji wa umeme katika sekondari za Muvigha *Girls*, Kinyeto, Ngimu, Mugori, Merya, Maghoja na Ughandi zilizopo katika Jimbo la Singida Kaskazini umeshafanyiwa tathmini katika mpango mzima wa Serikali wa usambazaji umeme Vijijini. Tathmini iliyofanyika ya kupeleka umeme katika shule hizo na vijiji jirani inakadiriwa kufikia Sh. 1.4bn/=. Mradi huu utatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa hivi ndiyo tunapitisha Bajeti ya 2007/2008: Je, Serikali imetenga kiasi gani kwa ajili ya kazi hii? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, Serikali imetenga kiasi gani kwa kazi hii. Nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri usijibu kwa sababu Bajeti yenu inakuja leo. Tunaendelea na swali linalofuata.

*(Hapa swali Na. 211 liliondolewa mpaka baadaye ili kumpa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri kujiandaa vizuri)*

Na. 212

### Barabara ya Busisi – Nyang'hwale – Nyan'holongo

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Busisi - Nyang'hwale hadi Nyang'holongo ilifanyiwa matengenezo mwaka 2000 – 2005 na ikaweza kupitika lakini kutokana na mvua kubwa zilizonyesha kati ya Novemba, 2006 na Februari, 2007 zimesababisha tena uharibifu mkubwa kwenye barabara hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuifanyia matengenezo makubwa pamoja na madaraja ya Nyaruhwa, Wingi na Ligembe ambayo yameharibika kutokana na mvua?

(b) Kwa kuwa barabara hiyo kwa upande wa Kahama inalingana na ile ya kutoka Segese – Bumva – Mundu – Nyang'holongo iliyo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Je, Serikali iko tayari kuipandisha hadhi ili iwe ya *TANROADS* kama ilivyo kwa upande wa Nyang'holongo hadi Busisi.

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuipandisha hadi barabara ya Sengerema – Kigoma ambayo inaungana na ile ya Busisi – Nyang'holongo iwe chini ya *TANROADS* ili kuunganisha Miji ya biashara ya Kahama, Segese, Kharumwa, Busolwa, Ngoma, Sengerema hadi Mwanza?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Novemba 2006 hadi Februari, 2007, nchi yetu ilipata mvua kubwa ambayo ilileta madhara kwa upande wa mtandao wa barabara karibu nchi nzima, ikiwemo na barabara ya Busisi – Nyang'hwale hadi Nyang'holongo. Ili barabara hizi nchi nzima ziweze kupitika, zaidi ya Sh. 10,000,000,000/= zilihitajika. *(Makofi)*

Baada ya madhara hayo kujitokeza Wizara ilichukua tahadhari na kuandaa Bajeti ya dharura ya Sh. 10.3bn/= kwa nchi nzima ili kuweza kuzitengeneza barabara zote zilizoharibika na mvua ili ziweze kupitika. Barabara ya Busisi – Nyang'hwale hadi Nyang'holongo yenye urefu wa kilomita 110 ni moja ya barabara zilizo kwenye mpango wa matengenezo ya dharura ya tayari mkandarasi M/s *Tabasam General Merchant* ameanza kufanya ukarabati kwa kujenga daraja *(box culvert)* eneo la Wingi, kuchanga barabara *(light reshaping)* na kuweka changarawe maeneo korofi. Kazi hii itagharimu jumla ya Sh. 68,444,500/= na inatarajiwa kuwa imekamilika kabla ya mwisho wa mwezi Julai mwaka huu. Katika Bajeti ya mwaka 2007/2008, Wizara yangu itatenga fedha kwa ajili ya kujenga madaraja ya Nyaruhwa na Ligombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupandishwa hadhi barabara za Halmashauri ama za Wilaya kuwa za Mkoa litazingatiwa kwa kufuata vigezo vilivyomo katika Sheria

ya Barabara iliyopitisha na Bunge mwezi Aprili, 2007 zoezi ambalo kwa sasa bado linaendelea.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, lakini kabla sijauliza napenda niipongeze sana Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu ambayo Bajeti yake tulipitisha jana kwamba angalau safari hii imetenga hela za kutosha kidogo kutengeneza barabara hiyo niliyoisema. Lakini napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa *Bulyanhulu Gold Mining* wanatumia barabara hiyo kutoka Kakola kwenda Karumwa – Busolwa hadi Ngoma kwenye mgodi wao wa *Barrick* na kwa kuwa wanapitishia mitambo yao mizito sana zaidi ya tani arobaini na kwa kuwa wameshaonyesha dalili, juzi nilifanya nao mazungumzo, wameonyesha dalili ya kukubali kushirikiana na Serikali kutengeneza barabara hiyo ili iwe imara.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwasiliana na uongozi wa *Bulyanhu Gold Mining* ili kukamilisha mazungumzo hayo ili sasa kama watakubali fedha inayopatikana iweze kuimarisha kipande cha kutoka Karumwa kwenda Izunwa, Kayenze, Nyang'holongo hadi Segese? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa nilishawasiliana na Waheshimiwa Wabunge: Mbunge wa Msalala Mheshimiwa Maige na Mbunge wa Sengerema Mheshimiwa William Ngeleja kwamba tufanye maombi ya kupandishwa hadhi kipande cha kutoka Segese kuja Nyang'holongo kihudumiwe na *TANROADS* kitoke kwenye Halmashauri ya Kahama na kile kipande cha Sengerema kuja Ngoma ambacho ni *shortcut* kuja Mwanza kipandishwe hadhi kiwe cha *TANROADS* na kwa kuwa Sheria ya Barabara ambayo tumeipitisha.

Je, hiyo sheria ikishawekwa sahihi Waziri sasa atakubali moja kwa moja kupandisha barabara hizo kufuatana na maombi ya Wabunge hawa watatu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama hawa wawekezaji kwenye migodi wapo tayari kushirikiana na Serikali, ni sera yetu kwamba, tushirikiane na wenzetu hasa pale ambapo wapo tayari kutusaidia hasa kwenye masuala ya miundombinu.

Kwa hiyo, hili suala tutalifuatilie na tutamwagiza Meneja wa *TANROADS* aanze kuongea nao kama bado hawajaongea na tutafikia muafaka kujua tushirikiane vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la kupandisha hadhi barabara, tumeshasema hapa kwamba mkakati huu tunaendelea nao baada ya kusainiwa kwa sheria ile hivi karibuni tutakamilisha sasa mchakato wa kuweka sawa lile jedwali la barabara kwa vigezo ambavyo Sheria hiyo itakuwa imeviweka. Kwa hiyo, kama barabara hiyo inakidhi vigezo hivyo itapandishwa, kama haikidhi basi haitapandishwa.

Na. 213

### Kusimamia Utekelezaji wa Sheria ya Elimu na Sheria ya Serikali za Mitaa

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. LAUS O. MHINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu (*Education Act No.* 25/1978) Sehemu ya III Kifungu 9(1) na Na. 7.1982 kifungu 118(2)(j) na (i) Halmashauri za Wilaya zimepewa jukumu la kujenga, kuendesha na kusimamia Vyuo vya Ufundi (ambavyo katika Sheria Na. 25/1978 vilikuwa vikiitwa *(Regional Schools)* na kwa kuwa tangu kutungwa kwa Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 333 *(Cap 333)* ya 1953 na Sheria ya Elimu ya wakati huo *(Regional Schools)* zilimaanisha Vyuo vya Ufundi *(Trade Schools)* ni vya kuchukua wanafunzi wa shule za msingi ambao wamekosa nafasi ya sekondari:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia utekelezaji wa Sheria hizo ili ujenzi wa vyuo hivyo uende sambamba na MMEM na MMES?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kujengwa kwa vyuo hivyo kutasaidia sana wanafunzi waliokosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza kuweza kujiendeleza katika stadi mbalimbali za kazi na hivyo kupunguza tatizo la ajira kwa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshiimwa Naibu Spika, *Trade Schools* zilibadilishwa kuwa shule za sekondari za ufundi (*Technical Secondary Schools*) mwaka 1967 ambazo kwa sasa zinasimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Baada ya *Trade Schools,* Serikali ilianzisha Vituo vya Ufundi Stadi *(Vocational Training Centres)* kwa Sheria ya Mafunzo ya Ufundi Stadi *(Vocational Training Act)* ya mwaka 1974 ambavyo vilisimamiwa na Kitengo cha Mafunzo ya ufundi Stadi *(National Vocational Training Division)* Chini ya Wizara ya Kazi.

Mwaka 1994 iliundwa Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi *(VETA)* kwa Sheria ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA Act)* ya mwaka 1994. *VETA* kwa sasa ipo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mpango wa Serikali kwa sasa ni kuanzisha Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya.

Wizara iko katika hata ya kukamilisha mapitio ya Andiko la MMES ambalo pamoja na mambo mengine litazingatia upanuzi mahitaji ya mafunzo katika kila Wilaya ya usimamizi wa Vyuo vya Ufundi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa uanzishwaji wa Vyuo vya ufundi Stadi vya Wilaya, kutasaidia sana wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari, kuweza kuiendeleza katika stadi mbalimbali za kazi na hivyo kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kama inavyoelekezwa katika ilani ya uchaguzi ya CCM mwaka 2005.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Serikali pamoja na kuwahamasisha wananchi tumepata mafanikio makubwa katika ujenzi wa Sekondari nchi nzima.

Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa kuwahamasisha wananchi vilevile katika kila Wilaya waanze kujenga Vyuo vya Ufundi ili itakapofika Bajeti ijayo wananchi wawe wamejiandaa na hatimaye Serikali iweze kuunga mkono hatua hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la wananchi kushiriki katika ujenzi wa Vyuo vya Ufundi kwa njia ya kujitolea kama tulivyofanya katika suala la ujenzi wa Shule za Sekondari unakaribishwa. Mara nyingi tumekuwa tukiziomba Halmashauri zijaribu kutenga maeneo ambayo wanafikiri wanaweza kujenga wao wenyewe kwa kushirikiana na wananchi.

Lakini tunajua kuna gharama kubwa sana za ujenzi wa Vyuo vya Ufundi hasa upande wa vifaa vinavyohitajika kutumika katika Vyuo hivyo vya *VETA.* Mashine zinazotumika kufundisia na vifaa vingine ni gharama kubwa sana. Kama wananchi wamejipanga vizuri katika Halmashauri ni ruksa kuweza kufanya kazi hiyo, lakini waombe ushauri kutoka kwa Taasisi hii ya *VETA* ambayo ina ujuzi na maarifa mengi kuhusu Vyuo vya *VETA. (Makofi)*

Lakini bado nia ya Serikali ni kuendelea na mpango wake wa kuhakikisha kwamba Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila Wilaya vinajengwa kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyoelekeza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na dakika zetu zilizotumika kwa ajili ya kutoa taarifa za Hati mbalimbali. Kwa hiyo, tunakwenda Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia swali 211, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe uliza tena. *(Makofi)*

Na. 211

**Uhitaji wa Walimu Wenye Shahada**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE (K.n.y. MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI)** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo mahitaji makubwa sana ya wataalam wenye elimu ya juu (shahada) kutokana na kufunguliwa shule nyingi za sekondari kote nchini, kupanuka kwa shughuli za kilimo, afya na uchimbaji madini na viwanda:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kukidhi mahitaji hayo ya wataalam wenye elimu ya juu (shahada)?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho Serikali inaelekeza kwenye elimu ya juu ili kukabiliana na tatizo la wataalam ifikapo mwaka 2025?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba radhi kwa yaliyojitokeza. Sasa kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza idadi ya wataalam wenye Elimu ya Juu na Elimu ya Kati na kwa kuzingatia mafanikio yaliyotokana na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) na Sekondari (MMES), Wizara imeanza kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Mwaka 2005/2006 pamoja na wanafunzi wanaochukua Shahada ya Ualimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pia Vyuo Vikuu Vishiriki viwili vifuatavyo vilianzishwa navyo ni:-

- Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam (Dar es *Salaam University College of Education*)
- Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa *(Mkwawa University College Education*)

(ii) Mwaka 2006/2007 Serikali iliamua kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, wanafunzi wote waliopata udahili wa kusomea Shahada ya Ualimu katika Taasisi za Elimu ya Juu wapewe mkopo katika Vyuo Vikuu vya Umma na Binafsi. Aidha, Serikali iliamua wanafunzi wanaochukua masomo ya taaluma za Kilimo, Uhandisi, Usanifu Majengo na Tiba nao wapewe mikopo ili kukidhi mahitaji ya wataalam hao.

(iii) Chuo Kikuu Huria kimeingia Mkataba na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa kufundisha Walimu wenye leseni na wale wa *Diploma* katika ngazi ya Shahada. Jumla ya walimu 1,600 walijiunga na Chuo Kikuu Huria katika mwaka 2006/2007.

(iv) Imeamua kujenga Chuo Kikuu kipya na cha kisasa hapa Dodoma *(The University of Dodoma)*. Chuo hiki ambacho kitaendeshwa kwa stahili za *Campus Mode*

kitakapokamilika kitakuwa na wanafunzi 40,000 na kitakuwa na Vyuo *(Colleges*) sita (Sayansi za Afya na Tiba, Sayansi za Uhai na Sayansi za Rasilimali Ardhi).

(v) Imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu na Ufundi (*Higher and Technical Education Development Programme*) kwa lengo la kuwezesha asilimia 12.5 ya wanaomaliza kidato cha sita kupata nafasi ya kuendelea na masomo katika Vyuo Vikuu, Taasisi za Teknolojia na Vyuo Vikuu vya Ufundi.

(iv) Imeanda mpango maalum (*Quick win Programme*) kwa ajili ya kuendeleza Elimu ya Juu na Ufundi utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa lengo la:-

- Kuongeza udahili (*Access*);

- Kuboresha masomo yatolewayo (*Quality of education*); na

- Kuzingatia umuhimu/uhitaji (*Revelance* na Kujenga uwezo (*Capacity Building*).

(vii) Wizara itaimarisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kwa kuboresha majengo, kuimarisha maabara, karakana na mitaala itakayokidhi mahitaji ya soko huria. Aidha, Taasisi hiyo itawezesha kutoa mafunzo katika fani za Hoteli *(Hotel Management*), Utalii *(Tourism*), Madini *(Mining)* na Teknolojia ya Maabara (*Laboratory Technology*).

(viii) Itaendelea kuimarisha Vyuo vya Elimu ya Juu vya Ufundi na kuanzisha mtandao wa Taasisi za Sayansi na Teknolojia kwa kuboresha mitaala na miundombinu ili kudahili wanafunzi wengi zaidi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kwa sasa kujua kiasi halisi cha fedha kitakachoelekezwa katika Elimu ya Juu kwani Serikali itaendelea kutenga fedha za kutosha kulingana na kukua kwa uchumi nchini hadi ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa mikakati ya Serikali kuhusu Elimu ya Juu kwa kweli ni mizuri na bila shaka itapelekea ongezeko la kutosha la Vyuo vya Elimu ya Juu nchini. Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa na Vyuo vyetu Vikuu vinavyoongezeka kwa kasi vya Binafsi na vya Serikali ni yenye ubora na viwango vinavyolingana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuna Taasisi mbili. Kwanza, ni Tume ya Vyuo Vikuu ambayo inashughulikia ubora wa Vyuo Vikuu vyote ikiwa ni pamoja na mitaala, *Quality Assurance* ya mitihani. Kabla ya Chuo Kikuu hakijasajiliwa lazima *TCU* ijiridhishe

kwamba Chuo Kikuu hcho kina wataalam, kina walimu, kina mitaala ya kutosha na mambo kama hayo na *TCU* inafanya kazi yake vizuri sana.

Pili, kwa Vyuo vya Ufundi tuna *NECTA* ambayo juzi niliizungumzia ambayo pia inahakiki ubora si tu wa taaluma, lakini pia na kutathmini mitihani kwamba inakidhi soko huria lililopo. Kwa mfano, kabla hatujatoa mitaala lazima tujue katika *market* ya viwanda ni mahitaji gani yaliyopo. Kwa mfano, sasa hivi tunahitaji wataalam katika utalii na Chuo cha Mbeya *MIST* tumekiweka mahsusi ili tuweze kukipanua kiweze kutoa wataalam wa kazi katika utalii, katika *Hotel Management* na katika *Mining.* Kwa hiyo, tuna kila aina ya *Organization* ambayo inashughulikia ubora wa Elimu ya Juu, kwa Vyuo Vikuu na Elimu ya Ufundi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Sasa leo nina kazi ya kuchukua karibu dakika 10 kuwatambulisha wageni.

Kwanza kabisa kwenye *Gallery* ya Spika, kuna Ndugu Baritazar Kilasi, mume wake na Mheshimiwa Estherina Kilasi na watoto wao Valetina Kilasi, Jacquline Kilasi, Wichilausi Kilasi na marafiki zao wote wasimame. Mheshimiwa Estherina Kilasi mnajua tena ni Mjumbe wa Kamati ya Tume ya Bunge. Kwa hiyo, ndiyo maana wanakuwa ni wageni wa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Cheyo, anapenda kutambulisha kijana wao, maana yake ni mtoto wa aliyekuwa Mbunge zamani hapa Isack Cheyo na kijana mwenyewe anaitwa Isack Cheyo yeye ni Mwanasheria wa Serikali baada ya kumaliza masomo *University* ya Tumaini.

Halafu kuna Bibi yetu hapa Bibi Rahel Upande anatoka Shinyanga ni Bibi yake na Mheshimiwa Esther Nyawazwa.Karibu mama.

Halafu kuna kundi kubwa la wageni wa Mheshimiwa Mussa Zungu. Kwanza kabisa kuna Ndugu Haji Sunday Manara nafikiri ni maarufu huyu. Halafu kuna Diwani Kippi Warioba. Jerry Slaa na Kessy Kheri. Hao wageni wanatoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Halafu kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Mussa Zungu ni Viongozi wa CCM Kata ya Ilala wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kata hiyo. Mheshimiwa Alhaj Abdallah Tabo Ngwazo na Katibu wa CCM wa Kata ya Ilala Said Sinde hebu wasimame, pamoja na wajumbe wote waliokuja nao. Lakini Mwenyekiti wa Kata asimame na Katibu wa Kata. Karibu sana. *(Makofi)*

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maji Dr. Shukuru Kawambwa, ambao wanatoka Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dodoma *(DUWASA)* wote wasimame. Wakiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji na Meneja wa Biashara. Wako wengi siwezi kuwataja majina wote. *(Makofi)*

Halafu kuna wageni wengine na hao nitawataja majina mmoja mmoja. Nina wageni wa Wizara ya Nishati na Madini leo ni muhimu sana kuwataja majina. Kwanza, kuna Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika la Maendeleo ya Mafuta *TPDC.* Jenerali Robert Mboma. Kuna Mheshimiwa wa Bodi ya Shirika la Umeme *TANESCO* Balozi Fulgence Kazaura. Kuna Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Tanzania Chamber of Minerals and Energy* Balozi Hami Mpungwe.

Tunaye mwingine Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Mafuta Ndugu Yona Kirangani. Kuna Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme *TANESCO* Dr. Idris Rashid. Wanapenda kukupiga makofi kwa sababu wanasema toka umefika siku chache tu mambo yanakuwa barabara kuliko siku zilizopita. Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa Gray Mwakalukwa. Hawa nimewatambulisha kwa sababu leo Wizara yao ndiyo inahusika. Kwa hiyo, inabidi wajulikane hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na matangazo ya kazi. Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anapenda kuwatangazia wajumbe wa Kamati yake kwamba kesho tarehe 14 Julai, 2007 saa tatu asubuhi wakutane katika ukumbi 231 watakuwa na kazi ya kuchambua na kujadili taarifa za mapato na matumizi ya Halmashauri ya Mkoa wa Dar es Salaam, Kibondo na Nzega kwa mwaka 2005/2006.

Waheshimiwa Wabunge, pia napenda kutangazia kwamba kesho tarehe 14 Julai, 2007 saa tatu asubuhi kutakuwa na Semina inayohusu Sera na Mkakati wa Ajira itaanza Saa 3.00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa na itaendeshwa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenye hiyo semina. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, wageni wetu wengine wote mnakaribishwa ni haki yenu kuja kuwasikiliza wawakilishi wenu wanavyochangia hoja za Serikali kwa niaba yenu. Tunaendelea Katibu. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/2008
### Wizara ya Nishati na Madini

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kuwa Waziri wa Nishati na Madini baada ya kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko hapo awali. Pia, nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika

kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu makadirio ya matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/08. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara chini ya Mwenyekiti mahiri, Mheshimiwa William Hezekia Shelukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa ushauri wao walionipa katika sekta za nishati na madini kwa nyakati mbalimbali tulipokutana. Nawashukuru kwa mchango wao mkubwa wakati wa uchambuzi wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2007/2008. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wanaonipa katika kusimamia na kuongoza Wizara hii yenye changamoto nyingi. Nina imani kuwa kwa ushirikiano endelevu tutaweza kuzikabili changamoto hizi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uteuzi wake kuongoza taasisi hiyo ya kimataifa ni jambo la kujivunia na heshima kubwa kwa Taifa. Pia, nawapongeza wananchi wa Tunduru kwa kumchagua Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura wa Chama cha Mapinduzi kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili. Vile vile nawapongeza Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge) na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Pia, nawapongeza Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mbunge wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesyu, Mbunge wa Viti Maalumu, kwa kujiunga na Bunge hili. Aidha, nawapongeza wote waliochaguliwa na Bunge hili kuwa Wabunge katika Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka huu Bunge hili lilimpoteza Mbunge wa siku nyingi, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti aliyefariki dunia kufuatia ajali ya ndege. Aidha, mwishoni mwa mwezi Juni Bunge lako limempoteza Mbunge wa Viti Maalumu, Vijana Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Natoa pole kwako, familia zao na wote walioguswa na misiba hiyo. Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho za marehemu, Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Bukoba Vijijini kwa ushirikiano wanaonipa na kujitolea kwao katika shughuli za maendeleo jimboni. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana kwa dhati ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2006/2007. Katika mwaka 2006/2007, Wizara ilitekeleza Mpango na Bajeti yake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoyatoa alipoitembelea Wizara mwezi Januari, 2006; malengo ya

MKUKUTA; na Mpango wa Kimkakati wa Wizara wa Mwaka 2006 - 2009. Sekta ya Nishati. mwaka 2006, sekta ya nishati ya umeme ilikua kwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 5.1 mwaka 2005. Sababu ya kushuka kwa ukuaji wa sekta hii ni ukame ulioikumba nchi yetu kwa takriban miaka mitatu mfululizo na kusababisha kupungua kwa maji kwenye vituo vya uzalishaji umeme vya Mtera, Kidatu, Pangani na Nyumba ya Mungu. Hali hii ilisababisha uzalishaji umeme kutokana na vyanzo vya maji kupungua kutoka Megawati *(MW) 561* hadi *MW 120.* Kufuatia upungufu huo, Serikali ilibuni na kuanza kutekeleza Mradi wa Dharura wa Umeme kwa kukodi mitambo yenye uwezo wa MW 185 na kujenga mitambo ya kudumu yenye uwezo wa kuzalisha MW 145.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji umeme nchini ulirejea katika hali ya kawaida kufuatia mvua nyingi zilizonyesha nchini kuanzia mwezi Januari, 2007 na kujaza mabwawa yote likiwemo la Mtera linalohifadhi takriban asilimia 80 ya maji ya kuzalisha umeme nchini. Hata hivyo, tatizo la kukatika umeme mara kwa mara kwenye gridi ya Taifa limeendelea kutokana na uchakavu wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji. Gharama za kukarabati mfumo mzima wa umeme kwa kipindi cha miaka mitano ijayo zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 1.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia. Kuanzia mwezi Julai, 2006 hadi Juni, 2007, Serikali imesaini mikataba sita ya utafutaji wa mafuta. Kati ya hiyo, mikataba mitatu ni ya utafutaji wa mafuta katika kina kirefu cha maji baharini (zaidi ya mita 200) na mitatu ni kwenye mwambao wa bahari *(continental shelf)*. Jumla ya mikataba hai hadi Juni, 2007 ni 19. Majadiliano na kampuni nyingine tatu yanaendelea. Baada ya kulitangazia Bunge lako Tukufu mwezi Februari, 2007 kuhusu ugunduzi wa gesi asilia Wilayani Mkuranga, kazi ya uchambuzi na tathmini ya takwimu za ugunduzi huo ili kubaini kama gesi hiyo inaweza kuendelezwa kibiashara, inaendelea. Miradi ya Gesi Asilia ya Songo Songo na *Mnazi Bay.* Utekelezaji wa miradi chini ya mradi mkubwa wa gesi asilia ya Songo Songo unaendelea. Ujenzi wa kituo cha *MW 6* kinachojengwa katika eneo la Somanga Funga umekamilika kwa asilimia 90. Umeme utakaozalishwa katika kituo hiki utasambazwa katika miji ya Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Singino, Nangurukuru, Utete, Ikwiriri, Kibiti, na vijiji ambamo bomba la gesi asilia linapita. Mradi wa *Mnazi Bay,* unaoendeshwa na kampuni ya Artumas umeshaanza kuzalisha umeme wa *MW 4* na kuiuzia *TANESCO* kwa mkataba wa mwaka mmoja (*Interim Power Purchase Agreement*). Umeme huo unasambazwa katika miji ya Mtwara na Lindi. Matumizi ya Mafuta na Gesi Asilia. Upatikanaji wa mafuta nchini ulikuwa wa kuridhisha kwa mwaka 2006/2007. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2006/2007, bei za mafuta katika soko la dunia zilipanda sana hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 75 kwa pipa kati ya mwezi Julai na Agosti, 2006. Katika kipindi hicho, bei ya petroli hapa nchini ilifikia wastani wa shilingi 1,300 kwa lita moja. Hadi kufikia mwezi Juni, 2007 bei za mafuta ghafi kwenye soko la dunia zilifikia wastani wa Dola za Marekani 70 kwa pipa na bei za mafuta nchini zilifikia wastani wa shilingi 1,250 kwa lita.

Umeme Vijijini. Miradi ya usambazaji wa umeme vijijini iliendelea kutekelezwa ingawa kwa kasi ndogo iliyosababishwa na upungufu wa fedha. Upungufu huo ulitokana na Serikali kuelekeza rasilimali nyingi kwa ajili ya kukabiliana na matatizo mbalimbali

yaliyotokana na ukame. Aidha, Serikali ilikamilisha taratibu za ununuzi wa jenereta za kuzalisha umeme kwa ajili ya miji ya Mbinga *(2 x 1,250 kVA)* na Ludewa *(2 x 600 kVA).* Vilevile, chini ya ufadhili wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Kimataifa la Maendelo *(SIDA),* mradi wa kituo cha kupoozea nguvu ya umeme (*substation*) cha Makambako kilikamilika na umeme wa gridi kuanza kutumika katika miji ya Makambako na Njombe. Kwa ufadhili huo huo wa *SIDA,* Miradi ya Urambo na Serengeti imekamilika, ambapo Mheshimiwa Rais alizindua mradi wa Serengeti mwezi Juni, 2007. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nishati Jadidifu na Mbadala. Mradi wa umemenuru unaofadhiliwa na *SIDA* umezinduliwa katika mikoa minne ya Iringa, Tanga, Morogoro na Pwani ili kuhamasisha soko la nishati hiyo. Wafanyabiashara 48 na mafundi 47 walipewa mafunzo husika. Aidha, chini ya mradi unaofadhiliwa na *Global Enviroment Facility (GEF)* kupitia *UNDP;* mitambo ya umemenuru imefungwa katika vituo vya afya sita, zahanati sita na shule za sekondari sita mkoani Mwanza. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi mwingine wa umemenuru chini ya Tanzania *Energy Development and Access Project (TEDAP)* umeanza mkoani Rukwa. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* iliendelea kusimamia utafiti wa nishati ya upepo. Kamati ya Kitaifa ya Bayofueli iliyoundwa na Serikali mwaka 2006 imeandaa mpango wa miaka miwili wa utekelezaji, pamoja na rasimu ya mwongozo wa uendelezaji endelevu wa bayofueli.Shughuli za udhibiti wa huduma za nishati, ambazo awali zilikuwa zinafanywa na Wizara, sasa zinafanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA)* iliyoundwa kwa Sheria ya Bunge ya mwaka 2001 na ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Sekta ya Madini. Mwaka 2006 mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa ulikua asilimia 3.8 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2005. Ukuaji wa sekta hii mwaka 2006 ulikuwa asilimia 16.4 ikilinganishwa na asilimia 15.7 mwaka 2005 na hivyo kufanya sekta hii kuendelea kuwa mojawapo ya sekta zenye kasi kubwa ya ukuaji nchini. Aidha, mauzo ya madini nje ya nchi mwaka 2006 yalifikia Dola za Marekani milioni 856.8 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 711.3 mwaka 2005. Ukuaji wa sekta hii ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la bei ya dhahabu kutoka wastani wa Dola za Marekani 445 kwa wakia mwaka 2005 hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 604 kwa wakia mwaka 2006. Shughuli za utafutaji madini nchini mwaka 2006/2007 zilikuwa na mafanikio. Mojawapo ya mafanikio yaliyopatikana ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa mradi wa dhahabu wa Buzwagi ulioko Wilayani Kahama ambapo shughuli za uchimbaji zitaanza mwaka 2008. Mradi wa Nickel uliopo Kabanga Wilayani Ngara umefikia hatua ya upembuzi yakinifu. Aidha, utafiti wa kina wa madini ya *platinum* unaendelea katika eneo la Mibango Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji wa Wachimbaji Wadogo. Mwaka 2006/07, Serikali iliendelea kusaidia sekta ya uchimbaji mdogo wa madini ili kuhakikisha unakuwa bora na wa kisasa kwa kuainisha, kutenga na kugawa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Maeneo manne ya ukubwa wa kilomita za mraba 40 yameainishwa katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera. Taratibu za kuyatenga rasmi kwa ajili ya wachimbaji wadogo zinakamilishwa. Zoezi hilo litaendelea kwa Mikoa yote yenye

shughuli za uchimbaji madini nchini ili kuainisha maeneo zaidi kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Mererani ni eneo pekee kwa sasa yanakochimbwa madini ya *Tanzanite* na limekuwa na changamoto nyingi za uchimbaji wa madini ya vito. Katika mwaka 2006/2007, Serikali imeendelea na ujenzi wa uzio katika eneo hilo lililotengwa kuwa eneo zuizi (*Controlled Area*) ili kuimarisha udhibiti wa utoroshaji wa madini ya *Tanzanite*; na kuondoa watu wasiohusika katika eneo hilo. Aidha, eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 104.9 lilitengwa maalumu kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa Mererani. Eneo hilo lina jumla ya viwanja 932 ambavyo tayari vimeanza kugawiwa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mwezi Septemba, 2006 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alishiriki katika uzinduzi wa mradi wa *Mwadui Community Diamond Partnership (MCDP) New York*, Marekani. Katika mradi huo *DeBeers Group* walitoa mchango wa awali (*seed money*) wa Dola za Marekani milioni 2 kwa ajili ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa almasi Mkoani Shinyanga ili kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ya Madini. Katika mwaka 2006/2007 Serikali iliendelea na mchakato wa kupitia upya mikataba ya madini ili kuhakikisha Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali ya madini yanayozalishwa. Kutokana na majadiliano, kampuni ya *Barrick Gold Corporation* inayomiliki migodi ya Bulyanhulu, Wilayani Kahama, Tulawaka, Wilayani Biharamulo, na *North Mara,* wilayani Tarime; na kampuni ya *Resolute (Tanzania) Limited* inayomiliki mgodi wa *Golden Pride* wilayani Nzega zilikubali kutekeleza yafuatayo:-

Kuondoa nyongeza ya asilimia 15 kwenye mtaji wa uwekezaji ambao haujarejeshwa *(15% additional capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure).* Hatua hii itawezesha kampuni hizo kukomboa gharama zao za uwekezaji mapema na hivyo kuweza kulipa kodi ya mapato *(Corporation Tax).*

Kulipa kiasi cha Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa Halmashauri zinazohusika na migodi hiyo. Halmashauri zinazonufaika na malipo hayo ni Tarime, Kahama, Nzega, na Biharamulo. *(Makofi)*

Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* imekubali na imeanza kulipa Dola za Marekani milioni 7 kila mwaka kwenye Mfuko wa Uwekezaji hadi migodi yake itakapoanza kulipa kodi stahili.

Kampuni ya *Resolute (Tanzania) Limited* imeondoa kipengele kwenye mkataba wake kilichokuwa kinairuhusu kutokulipa kodi ya mapato kwa wafanyakazi wake wa kigeni. Kuondolewa kwa kipengele hiki kutailazimu kampuni hii kulipa takriban Dola za Marekani milioni 2.2 kila mwaka kama malipo ya kodi ya mapato. Katika mwaka 2006/07 kampuni hiyo imelipa Dola za Marekani milioni 2.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya *Anglo Gold* Ashanti inayomiliki mgodi wa Geita imekubali kulipa kiasi cha Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa

Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Aidha, majadiliano katika maeneo mengine ya mkataba wake yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Madini ya Mwaka 1997 iliweka mazingira yanayovutia uwekezaji kutoka ndani na nje. Katika kipindi cha miaka kumi cha utekelezaji wa Sera hiyo kumekuwepo na mafanikio makubwa kiuchumi ambapo migodi mikubwa sita ya dhahabu imeanzishwa. Pia shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini zimepanuka.

Pamoja na mafanikio hayo, mchango wa sekta ya madini umeendelea kuwa mdogo. Kutokana na sababu hiyo Sera ya Madini ya Mwaka 1997 inadurusiwa ili kuleta maendeleo endelevu ya sekta na hivyo kuweza kuchangia ipasavyo kwenye uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha madini yanaongezwa thamani kabla ya kusafirishwa nje ya nchi kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali na ajira kwa Watanzania, Wizara katika kipindi cha 2006/07 imekamilisha mchakato wa kutathmini mfumo bora wa uendeshaji wa kituo cha Arusha *Gemstone Carving Centre* kilichopo mjini Arusha. Mfumo huo unalenga kukifanya kituo hicho kuwa chuo kinachotoa stadi za mafunzo ya uongezaji thamani, hususan ukataji vito na usonara kwa wachimbaji wadogo na wajasiriamali. Shughuli zinazoendelea hivi sasa ni utoaji wa mafunzo ya stadi za uchongaji wa vinyago vya mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha kazi ya ukaguzi na udhibiti wa shughuli za migodi mikubwa ya dhahabu, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliingia mkataba wa miaka miwili na kampuni ya kigeni iitwayo Alex Stewart (*Assayers) Government Business Corporation* (*ASAGBC*) tarehe 14 Juni, 2003. Mkataba huo ulimalizika tarehe 13 Juni, 2005 na ulihuishwa kwa kipindi kingine cha miaka miwili kilichomalizika muda wake tarehe 13 Juni, 2007.

Ukaguzi na udhibiti uliofanywa katika migodi hiyo katika kipindi cha 2006/07 ulibainisha upungufu katika taarifa za gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi. Hivyo, kuna umuhimu wa Serikali kuimarisha shughuli za ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi ili kuhakikisha migodi inachangia ipasavyo kwenye ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 2006/07 Serikali imeendelea kufanya kazi za ukaguzi na udhibiti wa shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini kote nchini. Aidha, shughuli za biashara ya madini zilisimamiwa na kuhakikisha madini yanayosafirishwa nje ya nchi yanalipiwa kodi zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Wakala wa Serikali wa *Geological Survey of Tanzania* (*GST*) ulifanya upimaji wa kijiolojia, kijiofizikia, kijiokemia na uchunguzi wa awali wa madini katika maeneo ya Chunya, Sikonge na Mpanda. Aidha, *GST* imekamilisha kazi ya kuchora na kuchapisha ramani za kijioliojia za maeneo ya Biharamulo, Mpanda, Kigoma na Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GST* iliweka vituo sita vya kupima matetemeko katika maeneo ya Kibaya, Kondoa, Manyoni, Singida, Mbeya na Dodoma kwa ushirikiano na Idara ya Jiolojia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, kwa kushirikiana na *STAMICO* na *BGR* ya Ujerumani, *GST* iliendeleza utafiti wa madini ya viwanda *(industrial minerals).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/07, Kitengo cha Uchambuzi na Uthamini wa Almasi (*Tanzania Government Diamond Sorting Organisation* - *TANSORT*) kilichambua na kuthamini jumla ya karati 179,421 za almasi zenye thamani ya Dola za Marekani 20,852,358. Serikali ilipata Dola za Marekani 809,662 kama tozo ya kuzichambua almasi hizo, na Dola za Marekani 807,398 kama mrabaha. Pamoja na majukumu mengine ya Kitengo, Wizara iliendelea kusimamia mchakato wa kuhamisha Kitengo hiki kutoka *London* na kukirudisha nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/07, Shirika la Madini la Taifa (*State Mining Corporation* - STAMICO) liliendelea na shughuli za utafutaji wa madini, kutoa huduma za utafiti kwa kampuni nyingine na kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kuwaunganisha na wawekezaji wa kutoka nje. Aidha, Shirika lilipata maeneo mapya kwa ajili ya utafutaji wa madini ya *fluorite* katika eneo la Sengeri mkoani Mbeya na miamba ya chokaa *(limestone)* katika eneo la Mikindani, Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2006/07, uwezo wa utendaji kazi wa watumishi uliendelea kuimarishwa ambapo watumishi 95 walipelekwa mafunzoni. Kati ya hao watumishi 66 walishiriki katika mafunzo ya muda mfupi na 29 mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Wizara iliajiri watumishi wapya 25 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na matarajio ya watumishi 105.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuiwezesha sekta ya nishati kuwa endelevu na kuchangia kikamilifu katika uchumi wa Taifa, mipango kwa mwaka 2007/08 ni pamoja na: kuendeleza kazi ya kupeleka umeme vijijini; kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa *TANESCO*; kuimarisha mifumo ya usafirishaji na usambazaji umeme; kusimamia shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi; kuratibu na kusimamia uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala; na kukamilisha durusu ya mpango kamambe wa kuendeleza sekta ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, Wizara imepanga kukamilisha yafuatayo: Uanzishwaji wa Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency* - *REA*) pamoja na mfuko wake (*Rural Energy Fund* - *REF*); kukamilisha mkakati wa kurekebisha sekta ya umeme; kuimarisha mfumo wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kuanzisha miradi ya hifadhi ya mafuta na kuiwezesha *TPDC* kushiriki katika biashara ya mafuta; kuratibu miradi ya gesi asilia; kukamilisha maandalizi ya sheria ya biashara ya mafuta (*Petroleum Supply Act*) na sheria ya gesi na kuhamasisha matumizi bora na uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Maendeleo ya Milenia, MKUKUTA, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, mipango na mikakati mingine ya kijamii na kiuchumi hayawezi kufikiwa bila kuongeza juhudi za kupeleka huduma bora za nishati vijijini. Kwa kutambua umuhimu huo Serikali itaanzisha Mfuko wa Umeme Vijijini (*REF)*, kwa kutumia vyanzo vya mapato endelevu kufuatana na Sheria ya Nishati Vijijini (*Rural Energy Act,* 2005). Serikali imetenga shilingi bilioni 10 katika bajeti yake hii kama mtaji wa kuanzia. Ni matumaini ya Serikali kuwa washirika wetu katika maendeleo wataunga mkono juhudi hizi za Serikali zitakazowezesha wananchi walio wengi vijijini kupata umeme. Mpango wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya utaendelea kupewa kipaumbele. Katika mwaka 2007/08 umeme utafikishwa katika makao makuu ya Wilaya za Rufiji, Kilindi, Mbinga, Ludewa, Kilolo na Simanjiro na baadhi ya vijiji vya Wilaya hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua juhudi za Serikali katika kuendeleza sekta ya nishati, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaandaa Mradi wa Kuendeleza na Kupanua Wigo wa Upatikanaji na Usambazaji Umeme Nchini (*Tanzania Energy Development and Access Project* (*TEDAP*)). Katika mwaka 2007/08, Serikali itaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia na *Global Environment Facility* (*GEF)* kwa lengo la kupata mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya kuendeleza mradi huo. Mradi utalenga maeneo makuu matatu: Uwekezaji kwenye gridi ya Taifa; upelekaji umeme maeneo yasiyounganishwa kwenye gridi (*off grid*); na kuijenga *REA* kiufundi (*technical support).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha na kuongeza ufanisi kwenye sekta ya umeme nchini, Serikali inakamilisha mkakati wa kurekebisha sekta hiyo (*Power Sector Reform Strategy - PSRS*) ili kutoa mwongozo wa uendeshaji wa sekta hiyo pamoja na fursa zaidi ya ushiriki wa sekta binafsi. Kutokana na Sheria ya Umeme ya mwaka 1931 iliyofanyiwa marekebisho mara 11 kutokidhi mahitaji na mabadiliko ya sekta hiyo, mchakato uliopo ni kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya sheria mpya. Maudhui ya sheria hiyo ni pamoja na kuondoa ukiritinba (*monopoly)* katika Sheria ya sasa ya Umeme. Muswada wa Sheria hii unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi Oktoba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zimechukuliwa kuhakikisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi asilia unaongezeka ili kukidhi mahitaji. Kazi ya ufungaji wa mitambo ya *TANESCO* ya kudumu inayotumia gesi asilia yenye uwezo wa kuzalisha *MW* 100 itakamilishwa na kuanza uzalishaji umeme kabla ya mwisho wa mwaka 2007. Aidha, ujenzi wa mitambo mingine ya *MW* 45 utakamilika mwaka 2008. Aidha, katika juhudi za kupanua wigo wa vyanzo vya nishati ya umeme, mradi wa *MW* 200 kutokana na makaa ya mawe ya Kiwira utaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya muda wa kati ni kutekeleza mradi wa umeme wa *MW* 200 unaotumia gesi asilia eneo la Kinyerezi na kubadilisha mitambo ya *IPTL* ya *MW* 100 ili itumie gesi asilia badala ya mafuta. Mkakati mwingine wa muda wa kati ni kuunganisha gridi za umeme za Zambia, Tanzania na Kenya ili nchi yetu iweze kuuganishwa na mifumo ya umeme wa nchi za Kusini mwa Afrika (*South Africa Power Pool – SAPP*) na nchi za Africa Mashariki (*East Africa Power Pool – EAPP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya muda wa kati na mrefu inahusisha miradi ya umeme itokanayo na nguvu ya maji ya Mito ya Ruhudji *MW* 358, Rusumo *MW* 60, *Stiegler's Gorge MW* 2400, Rumakali *MW* 222, Mpanga *MW* 118 na Masigira *MW* 144. Muda halisi wa utekelezaji wa miradi iliyoainishwa hapo juu utabainishwa kwenye Mpango Kamambe wa Umeme wa miaka 25, unaodurusiwa sasa. Durusu ya Mpango huu itakamilika mwanzoni mwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuimarika kwa uzalishaji umeme, ubora na uhakika wa upatikanaji wake bado hauridhishi. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Japan imekamilisha matayarisho kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoozea umeme eneo la *Regent Estate* ili kuimarisha mfumo na kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika Dar es Salaam. Kituo hicho kitaanza kujengwa mwaka 2007/08. Pia Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itaendelea na maandalizi ya mradi wa kuimarisha na kupanua miundombinu ya umeme kwa miji ya Dar es Salaam, Moshi na Arusha ili kupunguza upotevu wa umeme. Aidha, gridi ya Kaskazini Magharibi ya laini ya msongo wa *KV* 220 itaendelea kutekelezwa sanjari na miradi mingine inayojitegemea kama: Laini

ya msongo wa *KV* 220 kutoka Iringa kupitia Dodoma, Singida hadi Shinyanga; Laini za Shinyanga hadi Buzwagi na Musoma hadi Tarime ambazo zitatekelezwa kwa makubaliano maalumu kati ya *TANESCO* na watumiaji wakubwa wa umeme ikiwemo migodi ya Buzwagi, Tulawaka, *North Mara* na Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, Wizara itawasilisha Bungeni miswada ya sheria ambayo ni *Petroleum Supply Act*, na *Natural Gas Supply Act*. Kukamilika kwa sheria hizi kutaimarisha usimamizi wa sekta, pia kutaiwezesha *EWURA* kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya udhibiti katika huduma hizo. Kufuatia kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, kukua kwa teknolojia na mazingira mazuri ya uwekezaji, hamasa ya utafutaji mafuta hapa nchini imeongezeka. Katika mwaka 2007/08, Wizara inatarajia kusaini mikataba mitatu ya utafutaji mafuta katikamaeneo ya Ziwa Tanganyika, Bonde la Mto Ruvu na Kitalu Na. 8 katika kina kirefu baharini. Matumizi ya gesi asilia viwandani yameongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya viwanda vinavyotumia nishati hiyo. Kutokana na ongezeko la mahitaji hayo, ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka barabara ya Nelson Mandela hadi Gongo la Mboto utaendelezwa na utakamilika mwaka 2007/08. Ujenzi wa bomba hilo utaongeza kiasi cha usambazaji gesi asilia kutoka futi za ujazo milioni 10 hadi milioni 20 kwa situ.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* kwa kushirikiana na *Pan African Energy* watatekeleza mradi wa majaribio wa usambazaji gesi asilia iliyoshindiliwa (*compressed natural gas – CNG*). Aidha, *TPDC* itaendelea na mradi wa majaribio ya kutumia gesi asilia kwenye magari nchini. Serikali itashiriki katika uendelezaji wa miradi ya gesi ya Songo Songo na Mnazi *Bay* kwa kuchangia asilimia 20 ya gharama ya miradi hiyo. Kwa kufanya hivyo, mgao wa Serikali utaongezeka kwa asilimia 20 ya mgao wa mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na uhakika wa kuwa na mafuta ya kutosha nchini, Wizara itakamilisha mchakato wa kuanzisha hifadhi ya mafuta. Wizara itawasilisha mapendekezo Serikalini ya namna ya kuendesha na kusimamia hifadhi hiyo na nia ni kuanza kutekeleza mradi huo mwaka 2007/08. Vilevile *TPDC* imekamilisha maandalizi ya mpango wa kibiashara (*Business Plan)* wa kushiriki katika biashara ya mafuta hapa nchini. Utekelezaji wa mradi huu utaanza baada ya Serikali kuuridhia. Majadiliano na *Artumas* kuhusu mkataba wa kukodisha miundombinu ya *TANESCO* yatakamilika mwaka 2007/08. Kukamilika kwa Mkataba kutaiwezesha kampuni ya *Artumas* kuendesha shughuli ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi badala ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kugunduliwa kwa gesi asilia katika kisima cha Mkuranga, imeamuliwa kuharakisha uhakiki wa kuwepo gesi asilia ya kutosha. Kwa mwaka 2007/08 takwimu za mitetemo (*seismic*) za kilomita 200 zitakusanywa ili kuainisha maeneo ambayo yatachimbwa visima vingine kwa ajili ya kutathmini kiasi cha gesi iliyopo. Serikali itaendelea kuratibu shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Jua kwa msaada wa *SIDA* utaendelea kwa kuzindua shughuli za mradi katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma na Mtwara. Pia utekelezaji wa mradi unaofadhiliwa na *UNDP/GEF* utaendelea katika mikoa ya Mara, Kagera, na Shinyanga ili kuendeleza uzoefu uliopatikana Mkoa wa Mwanza. Kwa upande mwingine, ukusanyaji wa taarifa za nishati ya upepo, jotoardhi, maporomoko madogo madogo ya maji (*small-hydro power*) utaendelea ili kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika kuzalisha umeme. Aidha,

Serikali itaendelea kuhamasisha viwanda vya sukari kuzalisha umeme kwa kutumia mabaki ya miwa. Katika mwaka 2007/08, Serikali itaendelea kuhamasisha uendelezaji wa bayofueli nchini kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na mwongozo kuhusu bayofueli. Aidha, uratibu wa uwekezaji katika kilimo cha miwa kwa ajili ya *bio-ethanol* na mibono-kaburi (*jatropha*) kwa ajili ya *bio-diesel* utaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya sekta ya madini kwa mwaka 2007/08 ni:- kuendelea kukuza uwekezaji katika sekta kwa kuweka mazingira shindani ya kuvutia wawekezaji; kuendelea kuhamasisha ujasiriamali kwenye miradi ya kuongeza thamani madini kama vile ukataji na usanifu wa madini na utengenezaji wa bidhaa za madini ya vito; kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo na teknolojia muafaka katika utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini; kuongeza maduhuli ya Serikali yatokanayo na madini; na kuimarisha masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira katika shughuli za utafutaji na uchimbaji madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara katika mwaka wa 2007/08 ni pamoja na: Kukamilisha kuziunganisha katika Mtandao wa Mfumo Mpya wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni (*MCIMS*) ofisi 22 za madini zilizoko mikoani na kitengo cha utoaji na usimamizi wa leseni kilichopo Makao Makuu ya Wizara; Kuendelea kutekeleza mikakati ya kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kuainisha, kutenga na kuwagawia maeneo kama ilivyofanyika kwenye mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara; Kuendeleza majadiliano na kampuni za uchimbaji mkubwa wa madini nchini ili ziwasaidie wachimbaji wadogo hasa walio jirani na mgodi mkubwa kwa kuwapatia utaalamu na kuwawezesha; Kuendeleza mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini pamoja na maonesho ya teknolojia bora na salama za uchimbaji na uchenjuaji dhahabu katika eneo linalozunguka Ziwa Victoria; na Kufuatilia kwa karibu mradi wa Mwadui *Community Diamond Partnership*, ambao uko kwenye hatua ya awali, kama mfano wa juhudi za Serikali katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa almasi nchini, hususan kwa kuanzia Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali ya madini, Serikali itaendeleza majadiliano na kampuni zote zenye mikataba ya madini. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikaliitakamilisha majadiliano na Kampuni ya *AngloGold Ashanti* inayomiliki mgodi wa Geita katika mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha usimamizi na kuongeza mchango wa sekta kwenye Pato la Taifa, Serikali katika Mwaka 2007/08, itakamilisha mchakato wa kudurusu Sera ya Madini ya Mwaka 1997 na kuandaa rasimu ya sera mpya ya madini. Utekelezaji wa sera hiyo mpya baada ya majadiliano kati ya Serikali na Wadau husika, utalazimu marekebisho ya baadhi ya vipengele vya Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 na Sheria ya Kodi ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/08, Serikali itaendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani ya madini hapa nchini. Kituo cha Arusha *Gemstone Carving Centre* ambacho kwa sasa kinatoa mafunzo katika fani ya uchongaji vinyago vya mawe kitaongezewa fani ya ukataji, usanifu wa madini ya vito na usonara (*lapidary and jewellery*). Lengo ni kuhakikisha kwamba kituo hicho kinakuwa chuo cha kufundisha stadi za uongezaji thamani madini ghafi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za Serikali katika kufikia lengo la kuongeza thamani ya madini ghafi ya vito kabla ya kusafirishwa nje zinaendelea. Katika mwaka 2007/08, Wizara itaendelea kuhamasisha wachimbaji na wafanyabiashara wa madini ya vito kupata vifaa vinavyohitajika. Rasimu ya Sheria ya Usonara itawasilishwa Serikalini kwa maamuzi. Aidha, Bodi ya Vito iliyoundwa mwaka 2004, itaendelea kuwezeshwa ili itekeleze majukumu yake. Baada ya kumalizika kwa mkataba kati ya *Alex Stewart (ASAGBC)* na Serikali, kazi ya ukaguzi wa uwekezaji na uendeshaji wa migodi katika mwaka 2007/08 itaendelea kufanywa na Wizara kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 1998. Katika kuhakikisha kazi hiyo inafanywa kwa ufanisi, Serikali itaendelea kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi kwa kukijengea uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, *Geological Survey of Tanzania* (*GST*) itaendeleza shughuli za upimaji wa ramani za kijiolojia katika maeneo ya Sikonge mkoani Tabora. Aidha, *GST* itaendelea na utafiti wa madini ya viwandani na uchunguzi maalumu katika maeneo ya mifumuko ya madini. Vilevile, itaboresha utunzaji na utoaji wa takwimu za kijiolojia. Wizara itaendelea kukiimarisha Chuo cha Madini ili kiweze kutoa mafunzo ya miaka mitatu ya stashahada ya ufundi sanifu katika fani za jiolojia, utafutaji na uchenjuaji madini. Katika mwaka 2007/08, Chuo kitaongeza usajili kutoka wanafunzi 33 hadi 60.

Kitengo kitaendelea kuchambua na kuthamini almasi, sanjari na kazi ya mchakato wa kukirudisha hapa nchini. Kazi zitakazofanywa ni pamoja na kukamilisha taratibu za kupata ofisi ya Kitengo, kupeleka watumishi wengine zaidi kusomea utalaamu wa kuchambua na kuthamini almasi.

Serikali itakamilisha mchakato kuhusu hatima ya *STAMICO*. Pamoja na mchakato huo, *STAMICO* itaendelea na shughuli za utafutaji wa madini. Aidha, katika utoaji wa huduma za utafiti wa madini kwa kampuni nyingine, Shirika litaimarishwa kwa kununua mtambo mpya wa kisasa wa kuchoronga miamba (*drilling rig*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi na wachimbaji wadogo kwa lengo la kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI. Aidha, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 170 katika fani mbalimbali, imepanga kuwapeleka mafunzoni baadhi ya watumishi wake ili kuwapa mbinu mpya za kuimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu yao na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/07, Wizara ya Nishati na Madini ilinufaika kwa misaada kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa Serikali za nchi za *Sweden, Norway, Denmark,* Uholanzi, Ujerumani, *Japan,* na Marekani,. Vilevile, natoa shukrani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Ulaya, Umoja wa Nchi za Ulaya, pamoja na Mashirika ya *Global Environment Facility*, *IAEA, IMF, NORAD, SIDA, UNDP, UNESCO, NDF* na *UNIDO. (Makofi)*

Naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru viongozi wenzangu ambao kwa pamoja tumeweza kufanikisha shughuli za Wizara kwa mwaka 2006/07. Kwanza napenda kuwashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim Said Msabaha, Mheshimiwa Benard Kamillius Membe (Mb), na Naibu Waziri, Mheshimiwa Lawrence Kego Masha, waliosimamia mikakati mbalimbali ya utekelezaji wa mipango katika sekta za nishati na

madini kabla yangu. Mikakati waliyoindaa imekuwa msaada mkubwa kwangu. Namshukuru Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano wake mkubwa anaonipa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara. Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu, Bwana Arthur Gwanaloli Mwakapugi; Wakuu wote wa Idara na Vitengo; viongozi wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara wakiwemo Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi na Watendaji Wakuu; Kamati zinazosimamiwa na Wizara; na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumaliza naomba uniruhusu nitangaze kwamba hapo nje kwenye viwanja vyetu tunavyokaa kufanya burudani tuna maonyesho ya Nishati ya Madini ambayo yanaonyesha shughuli mbalimbali zinazofanywa na Wizara pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yanayoonyeshwa pale ni gari linalobadilishwa na kutumia gesi asilia; umeme utokanao na nishati mbadala ya jua, ugunduzi wa gesi Mkuranga uliofanywa na *TPDC*; shughuli za uchoraji ramani kutoka kwa wakala wa Jiolojia Tanzania; huduma za uchorongaji miamba kutoka *STAMICO*; miradi ya huduma ya jamii inayotolewa na Migodi mikubwa hapa nchini; na mafunzo ya mafundi sanifu katika fani za sekta ya madini kwenye chuo cha Madini na uongezaji wa thamani za mawe. Ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wote wafike wakajionee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti ya sh. 353,959,143,900 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na mashirika yake kwa mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:- Bajeti ya Maendeleo ni sh. 312,409,584,900 ambazo kati yake sh. 196,693,000,000 ni fedha za hapa na sh.115,716,584,900 ni fedha za nje; na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni sh. 41,549,559,000 ambapo sh. 2,710,527,000 ni kwa ajili ya mishahara na sh. 38,839,032,000 ni matumizi mengineyo (*OC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MHESHIMIWA SIRAJI J. KABOYONGA (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipatia nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara,

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2007/2008 kwa Mujibu wa Kanuni Na.81 (1), Kanuni za Bunge,Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika,kama ilivyo kawaida wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara, Kamati ilizingatia vipengele vifuatavyo kuhusu Fungu 58: Wizara ya Nishati na Madini: (i) Dira/Mwelekeo wa Wizara kuhusu kushughulikia masuala ya Nishati na Madini nchini; (ii) Majukumu ya Wizara; (iii) Taarifa kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara katika Mwaka 2006/2007; (iv) Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Mwaka 2006/2007; (v) Maelezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2006/2007; na (vi) Maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo kadhaa kuhusu Utekelezaji wa Mchakato wa Bajeti uliotolewa na Kamati. Tunapenda kuipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali ilizofikia katika kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati. Hata hivyo, katika maeneo ambayo yameonekana kuhitaji juhudi za uboreshaji, Kamati imeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifahamishwa kwamba katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2006/07 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:-(i) *TANESCO* imetekeleza miradi mipya ya umeme inayojumuisha mitambo itumiayo gesi asilia toka Kampuni ya kukodi *AGGREKO* inayozalisha Megawati (*MW*) 40, *Richmond/Dowans* inayozalisha *MW* 60. Kwa sasa na inatarajiwa kuzalisha *MW* 100 pindi itakapokamilisha ufungaji wa jenereta zote ambazo tayari zipo kwenye eneo la Ubungo. Aidha, Kampuni ya *ALSTOM Power Renta*l ya Marekani imekamilisha ufungaji wa mitambo ya dizeli yenye uwezo wa kuzalisha MW. 40 huko Mwanza; (ii) Kusainiwa kwa Mkataba baina ya *Wartsila* na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa *MW* 45 wa kuzalisha umeme wa kutumia gesi asilia utakaojengwa katika eneo la Tegeta – Dar es Salaam; (iii) Kufikishwa katika eneo la mradi Ubungo na kufungwa jenereta zote 12 za mradi wa kuzalisha *MW* 100 kwa kutumia gesi asilia. Ujenzi wa eneo la kufunga *transfoma* unaendelea vizuri na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2007; (iv) Kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kupoozea nguvu ya umeme cha Makambako (Makambako *Sub-station*), mwezi Machi, 2007; (v) Utafiti wa kurekebisha mitambo ya *Independent Power Tanzania Limited* (*IPTL*) ili iweze kutumia gesi asilia unafanyika kwa awamu ambapo mpaka sasa majaribio ya awali ya mitambo (*prototype machine*) yamekwisha fanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatika kuhusu Miradi ya Shirika la Mafuta ya Petroli *(TPDC)* ni kama ifuatavyo: (i) Kuthibitika kwa upatikanaji wa gesi katika Kisima cha Mkuranga kilichochimbwa na Kampuni ya *Maurel and Prom*, ambapo majaribio yameonyesha kuwepo kwa gesi ya futi za ujazo kiasi cha milion 20 kwa siku; (ii) Kuendelea kwa shughuli za utafutaji mafuta na gesi katika maeneo ya Mandawa (Wilaya ya Kilwa) zinazofanywa na Kampuni ya *DOMINION Oil and Gas* ya Uingereza. Aidha, utafiti wa aina hii unaendelea pia kwenye *Block* Na. 5 na Na. 6 katika kina kirefu baharini unaofanywa na Kampuni ya *PETROBRAS* ya *Brazil;* (iii) Kusainiwa kwa mkataba wa kugawana mapato (*Production Sharing Agreement (PSA*) kati ya Serikali,

*PETROBRAS* na *TPDC* katika *Block* Na.6 ya kina kirefu Baharini. Mkataba mwingine kati ya Serikali, *TPDC* na Kampuni ya *STATOIL* umesainiwa kwa ajili ya *Block* Na. 2 ya kina kirefu cha Bahari. Vilevile Mkataba kati ya Serikali, *TPDC* na Kampuni ya *DOMINION Oil* umesainiwa kwa ajili ya *Block* Na. 7 kwa ajili ya utafutaji mafuta katika kina kirefu Baharini; na (iv) Kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaifa ya "Bayofuel" inayojumuisha Taasisi za Serikali, NGOs na Sekta binafsi. Kamati hiyo itaratibu mipango ya uendelezaji wa "Bayofuel" nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Madini mafanikio yafuatayo yalipatikana: (i) kuanza kulipwa kwa Kodi ya Halmashauri (*Local Government Levy*) kwa kiasi cha Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa kila Halmashauri ambako Kampuni za madini zina migodi. Halmashauri zitakazonufaika na makubaliano hayo ni pamoja na Tarime, Kahama, Nzega, Geita na Biharamulo; na (ii) Kampuni za *Barrick (T) Ltd* na *Resolute (T) Ltd* zimekubali kuilipa Serikalini Dola milioni 7 na milioni 2 sawia kila mwaka mpaka zitakapoanza kupata faida na kulipa kodi ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha nusu mwaka, Julai-Desemba, 2006 Kamati ilifahamishwa na kubaini kuwepo kwa matatizo yafuatayo:- (i) Upungufu wa Umeme; (ii) Ukame ulioikumba nchi yetu kwa miaka mitatu mfululizo uliaothiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa umeme unaotokana na maji; (iii) Uwezo wa kuzalisha umeme kutokana na mitambo inayoendeshwa kwa maji ulipungua kutoka jumla ya *MW* 561 hadi kufikia *MW* 120 kwa mwaka 2006. Upungufu huo uliilazimu Serikali kuingia mikataba ya kukodisha mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura. Miongoni mwa mikataba hiyo ni pamoja na ule wa *Richmond Development Cooperation* uliyorithiwa na *Dowans Ltd* ambayo Kamati inaona ilikuwa na upungufu. Upungufu huo wa kimkataba uliojitokeza upo katika Taarifa yetu ya Kamati ya mwaka 2006 ambayo tayari ilikwisha kuwasilishwa kwako mwezi Aprili, 2007 ambayo kwa mujibu wa Ratiba ya Vikao vya Bunge itapatiwa nafasi ya kujadiliwa kabla ya kumalizika kwa Mkutano huu wa Nane wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la umeme liliifanya nchi nzima iingie katika mgao wa umeme kutokana na kushuka kwa uzalishaji wa umeme wa maji kutoka *MW* 561 mpaka *MW* 120. Hali hii iliwaathiri watumiaji wa umeme hasa wa majumbani na kupunguza kasi ya kuwaunganishia umeme wateja wapya na kwa hiyo kupunguza mapato ya *TANESCO* kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo jingine ni ukosefu wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo iliyopitishwa na Bunge katika Bajeti ya Mwaka 2006/2007 haukwenda kama ilivyotarajiwa kutokana na kutopatikana kwa fedha zote zilizoidhinishwa ambazo chanzo chake ni mpango wa "*Multilateral Debt Relief Initiative (MDRI)*".

Bei kubwa za Mafuta, hususan ongezeko la bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia limekuwa na athari za moja kwa moja katika bei za mafuta hapa nchini. Ongezeko hilo limesababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji umeme kwenye vituo vinavyotumia mafuta kama vile *IPTL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara ina upungufu wa Watumishi katika Idara zote. Katika mwaka wa Fedha 2007/2008 watumishi wapya wapatao 252 wanahitajika kujaza nafasi zilizo wazi katika kada mbalimbali kulingana na Muundo wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya wachimbaji wa madini wadogo kwa wadogo na kati ya wakubwa na wadogo, limekuwa tatizo sugu katika sekta ya madini. Tatizo hili kwa kiasi kikubwa limesababishwa na wahusika kutofuata sheria, kanuni na taratibu za Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie Maoni na Ushauri wa Kamati. Nianze na Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*). Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi na sisi Wajumbe wa Kamati ni mashahidi kwamba mara nyingi umeme hukatika bila mamlaka husika kutoa taarifa yoyote. Hali hii huwasababishia hasara kubwa wateja wa *TANESCO* kutokana na uharibifu wa vifaa vyao muhimu vya umeme. Aidha, vyakula vilivyohifadhiwa katika majokofu navyo pia huharibika. Hali hii pia huwaathiri wafanyabiashara wa vyakula kama vile samaki na nyama. Kamati inashauri kuwa ni vema *TANESCO* ikatoa taarifa mapema kwa wananchi wa maeneo ambayo wanadhani hayatakuwa na umeme kwa sababu maalumu ili kupunguza kama si kuondoa kabisa kero hizi na hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* iliwasilisha Serikalini Mpango wake wa kujinusuru kibiashara na kuweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Kamati iliupitia na kubaini kuwa ni mzuri, lakini unahitaji fedha za nyingi. Aidha, kwa kuwa miundombinu mingi ya Shirika ya utoaji wa huduma ya umeme ni michakavu, Kamati inaishauri kuwa Serikali ilisaidie ili pamoja na kutekeleza mpango wao, Shirika liweze kubadilisha vifaa vilivyochakaa kabla ya kujitegemea rasmi. Hatua hii itasaidia kupunguza ukatikaji wa umeme wa mara kwa mara. Na kama Serikali haina fedha za kukidhi mahitaji ya *TANESCO,* Kamati inaishauri Serikali itoe dhamana kuiwezesha *TANESCO* kukopa fedha inazohitaji kutoka kwenye Mabenki na Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Independent Power Tanzania Limited (IPTL)*, pamoja na Wizara kutufahamisha kwamba urekebishaji wa mitambo ya *IPTL* kutumia gesi asilia kuonyesha mafanikio, bado Kamati haikuridhishwa na kasi inayoendelea. Kamati imeishauri Serikali mara nyingi kwamba iharakishe utaratibu wa kukinunua kituo cha uzalishaji umeme cha *IPTL* pamoja na kukigeuza ili kitumie gesi asilia badala ya mafuta mazito.

Kwa mara nyingine Kamati inasisitiza utekelezaji wa ushauri wake haraka iwezekanavyo. Wakati Kamati ikijadili na kupitia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini 2007/08 ilifahamishwa kuwa gharama yote ya mradi wa *IPTL* ni deni na kwamba deni hilo limekwisha nunuliwa na "*Standard Charter Bank*". Kwa bahati mbaya, kiasi cha deni hilo ni siri ya kibiashara kati ya *IPTL* na Benki husika. Kwa hiyo, Kamati inashauri kwamba Serikali iendelee kujadiliana na "*Standard Charter Bank"* kwa

madhumuni ya kufikia muafaka wa kukinunua kituo hicho kwa bei inayozingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Umeme Vijijini (*Rural Energy Fund (REF)*, haukuwa na fedha kwa miaka miwili iliyopita baada ya uzinduzi wake. Lakini katika mwaka wa fedha 2007/2008, Mfuko umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 10. Hata hivyo Kamati inaishauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuutunisha mfuko ili usambazaji umeme vijijini utekelezwe kwa kasi nzuri. Kamati inaishauri Wizara kubuni utaratibu na kuongeza matumizi ya umeme unaotokana na nishati ya jua vijijini hasa katika maeneo ya Shule na Zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikishwaji wa Wananchi katika Miradi mbalimbali, kumekuwa na matatizo ya kutowashirikisha vema wadau au wananchi katika hatua za awali za miradi. Kamati inaamini kuwa Wananchi wakishirikishwa katika miradi tangu hatua za awali inakuwa endelevu kwani wananchi wanaona wanawajibika moja kwa moja katika kufanikisha miradi hiyo. Hivyo Kamati inaishauri Serikali, Wizara na hasa Shirika la Umeme (*TANESCO*) kuwa na utaratibu wa kuwashirikisha Wananchi wa maeneo wanakopitisha umeme kwa kuajiri vibarua toka maeneo husika ili kuzuia hujuma mbalimbali dhidi ya Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Maendeleo ya Mafuta (*TPDC),* Kamati imefarijika baada ya kufahamishwa kuwa Serikali ipo katika mchakato wa kulipa deni la zaidi ya Dola za Marekani 1,898,562 pamoja na riba ya dola 62,929 kwa Wakili wa Mdai *M/S Hunton & Williams* kama Kamati ilivyoishauri mwaka uliopita. Deni hili lilitokana na uamuzi wa Serikali wa kusitisha mkataba wa uagizaji mafuta kati ya Shirika la Maendeleo ya Mafuta *(TPDC)* na *ADDAX* mwaka 1999/2000.

Kamati bado inaendelea kusisitiza kuwa ni vema mchakato wa ulipaji wa deni hili ukashughulikiwa haraka ili kupunguza ongezeko la deni kwa kasi kubwa kutokana na utaratibu wa kutoza riba juu ya riba *(compound interest).*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inaishauri Serikali kuwa makini zaidi wakati wa kusaini na kuvunja mikataba ya aina hii ili kuepuka gharama kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali iiwezeshe *TPDC* kifedha ili Shirika líweze kutekeleza Mpango wa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta (*Strategic Oil Reserve*) sambamba na utafiti wa mafuta na gesi asilia nchini. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba *TPDC* iruhusiwe kubakiza sehemu ya mapato (*Retention*) yatokanayo na mauzo ya gesi asilia ili kuliwezesha Shirika kushiriki katika kuwekeza katika biashara ya gesi asilia na mafuta kwa mujibu wa Mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hivi sasa limeandaa mpango wa kusambaza gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani katika Jiji la Dar es Salaam. Vilevile Shirika limeanzisha majaribio ya matumizi ya gesi asilia kwenye Magari sambamba na mafuta.

Matokeo ya majaribio ya awali yameonyesha mafanikio makubwa. Hatua inayofuata ni Shirika kuitangaza na kuisambaza teknolojia hii nchini. Mpango huu unahitaji fedha nyingi ili kuufanikisha. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kulisaidia Shirika ili lifanikishe malengo yake ya kuhamasisha matumizi ya gesi asilia kama nishati mbadala ya matumizi majumbani badala ya mkaa wa kuni, na kwa kufanya hivyo Shirika litasaidia utekelezaji wa Sera ya Serikali ya kulinda Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafutaji wa mafuta, bado lile tatizo la kufanya utafiti wa mafuta katika eneo la mwambao wa Tanga na Pemba (*Block D*) halijapatiwa ufumbuzi. Serikali mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado hazijafikia muafaka kuhusu utaratibu wa kuchimba mafuta na gesi asilia na mgawanyo wa mapato yatokanayo na rasilimali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika,Kamati inashauri kwamba kwa kuzingatia kuwa rasilimali ya mafuta na gesi asilia ni mali ya Watanzania wote, ni vizuri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ziharakishe majadiliano na kupatikana kwa muafaka kuhusu suala hilo ili kuwezesha utafiti wa mafuta katika eneo la Kitalu D kuanza bila ucheleweshaji zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Gesi Asilia wa Mnazi *Bay* (Mtwara), *TPDC* inahitajika kuwekeza kwa kiwango cha asilimia 20 katika mradi huu sawa na Dola za Marekani milioni 7.8 katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Kuwekeza kwa *TPDC* katika mradi huu kuna faida ya kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka huu 2007/08 Serikali imetenga sh. milioni 315 tu kwa uwekezaji katika Mradi wa Mnazi *Bay.* Kamati inaishauri Serikali kwamba ni vizuri ikatenga fedha za kutosha kuwekeza katika mradi huo kwani kuna athari kwa *TPDC* na Serikali kama zilivyoainishwa kwenye Mkataba wa *PSA* wa Songo Songo ambazo ni pamoja na:- Adhabu ya kulipa riba ya kila mwezi; Kupoteza haki ya kupiga kura (*voting rights*) katika Mikutano ya Uwekezaji;Kuwekwa rehani (*lien)* mgawo wa mapato ya *TPDC;*Kukosa ongezeko la mapato yanayoendana na uwekezaji wa asilimia 20 kiasi cha Dola za Marekani 30 milioni; Mwisho ni kwamba, kama *TPDC* haitawekeza tangu mwanzo, basi itapoteza nafasi hiyo kwa kipindi chote cha mradi. Hii ina maana kuwa hata mafuta yakigunduliwa katika eneo hilo mgao wa *TPDC* na Serikali hautaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya madini, Kamati ilifurahishwa na azma ya Wizara ya kuliendeleza Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO)* na kulipa uwezo zaidi Shirika la Madini la Taifa. Lakini uendelezwaji huo na uwezo vinategemea zaidi namna Shirika lenyewe litakavyojipanga hasa kwa kupeleka mapendekezo ya Mpango wa kuliendeleza Wizarani.

Kamati kwa upande wake inaishauri Wizara kwamba pamoja na dhamira nzuri ya kuliendeleza hasa baada ya kupokea mapendekezo ya *STAMICO*, ni vema Wizara ikahusika kwa karibu zaidi katika kufanikisha azma ya kulifufua Shirika hilo na kuliwekea misingi endelevu kabla ya kuliacha kujitegemea. Shirika hili linaweza kutumiwa kuendeleza Wachimbaji Madini wadogo na kuwapatia mahali pa kupatia ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Machimbo ya *Tanzanite* Mererani kumekuwa na migogoro kati ya Wachimbaji Wakubwa wa *Tanzanite One* na Wachimbaji Wadogo. Aidha, kumekuwa na malalamiko ya Wachimbaji kukutana kati ya Vitalu na Vitalu (*Blocks*) huko chini ya ardhi (kutobozana). Ili kumaliza matatizo hayo Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa maeneo wanayogawiwa wachimbaji wadogo ni madogo mno na ndiyo sababu ya kukutana chini ya ardhi, wachimbaji hawa wadogo washauriwe kujiunga katika makundi ili kwa pamoja waweze kugawiwa maeneo yenye ukubwa wa kutosha na kuondoa tatizo la kutobozana;

(ii) Sheria ya Madini ya mwaka 1998 inayomtaka mchimbaji wa madini achimbe wima (*Vertically)* iangaliwe upya kwa kuzingatia kwamba madini ya *TANZANITE* yanafuata Mkondo wa mshazari (*Horizontally)*;

(iii) Nchi nyingi Duniani kama India na Malawi hazitoi leseni za kuchimba madini ya vito kwa wageni. Kamati inashauri kwamba nchi yetu nayo itunge Sheria inayozuia Wageni kuchimba Madini ya Vito (*Gemstones*). Kazi hii waachiwe Watanzania tu. Aidha, Kamati inashauri kwamba vijengwe viwanda vya kuchoronga vito na kuanzisha Soko la vito karibu na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ili kuwaepushia matatizo ya safari ndefu wanunuzi kutoka nje ya nchi.(*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uthaminishaji wa dhahabu yetu, Serikali iliitumia Kampuni ya *Alex Stewart* baada ya kushinda zabuni. Lakini imefahamika kuwa Watendaji wengi katika Kampuni hii ni wataalamu wa Kitanzania.

Kwa kuwa wataalamu hao ni wa hapa nchini na kwa kuwa Kamati imefahamishwa kuwa Mkataba wa *Alex Stewart* umemalizika tarehe 13/06/2007 na kwa kuwa nia na mwelekeo wa Wizara ya Nishati na Madini ni kujenga uwezo wa ndani, Kamati inashauri kwamba ni vema wataalamu hao Watanzania wakafanya kazi hii iliyokuwa ikifanywa na *Alex Stewart* kuanzia sasa.(*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Madini cha Dodoma, Taasisi za Mafunzo na Utafiti ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Ni vigumu kwa nchi nyingine kuipatia mafunzo na kuifanyia utafiti nchi nyingine ili iweze kuendelea. Chuo cha Madini pamoja na kufundisha hufanya utafiti wa Madini, kwa hiyo , Kamati inaishauri Serikali kukiendeleza na kukijengea uwezo Chuo hiki kwani Wananchi wengi wanakihitaji kwa ajili ya mafunzo ya madini na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mawasilisho ya Wizara ya Nishati na Madini kuhusu Mipango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008, kwa niaba ya Bunge lako Tukufu Kamati ilipitia na kujadili kwa kina taarifa hizo; na sasa inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kukubali kupitisha kiasi kinachoombwa cha shilingi 353,959,143,900/=. Kati ya fedha hizo shilingi 41,549,559,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 312,409,584,900/= ni kwa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Pili napenda kumshukuru Mheshimiwa Nazir Karamagi, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Katibu Mkuu na Watalaamu wote wa Wizara na Taasisi zote chini ya Wizara hiyo, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano wa hali ya juu waliotoa kwa Kamati na hivyo kuiwezesha kutoa maoni na kushauri ipasavyo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri ya uchambuzi wa Makadirio ya Wizara kwa umakini mkubwa. Naomba kuwatambua kama ifuatavyo:- Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Dk.Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Muhammad A. Chomboh, Mheshimiwa Yahya K Issa, Mheshimiwa Asha M. Jecha.

Wengine ni Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Herbert J.Mntangi, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Luhanga Joelson Mpina, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro.

Mheshimiwa Saverina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Mohammed S. Sinan na Mheshimiwa Abdallah S. Sumry. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damiani Foka, pamoja na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Lina Kitosi, kwa kuihudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tulikuwa tuna mashaka na umeme, mbele ya Wizara yenyewe, halafu unazimika. Tushukuru Jenereta tulilonalo. Wiki hii umeme umekuwa hauna kanuni humu ndani. Sasa namwomba Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii. Mheshimiwa Mnyaa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kuniwezesha kusimama hapa leo hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ili kutoa maoni na ushauri kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na.43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la 2004 kuhusu mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa Fedha 2007/2008. Kwa utekelezaji Mipango ya Bajeti jumla ya Sh.353,959,143,900/- zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara ambapo Sh. 41,549,559,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 312,409,584,900/- kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nimewasilisha mezani ninaomba inukuliwe kama ilivyo katika *Hansard* hata kama sitomaliza kuisoma yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii adimu na adhimu kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Mkanyageni na Chama changu cha *CUF* walioniwezesha kufika hapa Bungeni. Nawaahidi kuwa karibu nao kwa shida na raha kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia maana wao ndio wanaosababisha niwepo hapa na kunipa fursa hii leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza viongozi wangu wa Kambi Mheshimiwa Hamad Rashid na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Slaa kwa kunipa moyo muda wote wa maandalizi ya hotuba hii. Na mwisho lakini si kwa umuhimu ni Msaidizi wangu wa Wizara hii Mheshimiwa Severina Mwijage

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mambo muhimu yaliyopangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2006/2007 ni mawili tu makubwa ambayo ni ukuaji wa Sekta ya Nishati na Ukuaji wa Sekta ya Madini ambayo yamebainishwa katika ukurasa wa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukuaji wa Sekta ya Nishati, Wizara ilikuwa imeweka malengo yafuatayo:-

(a) Kuwa na ongezeko la Uzalishaji Umeme usiotegemea maji;
(b) Mradi wa Uunganishaji wa Gridi za Zambia,Tanzania na Kenya;
(c) Uboreshaji wa Grid ya Taifa ya Umeme;
(d) Mradi wa Gesi asilia ya Songosongo;

(e) Usanbazaji Umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zisizopungua 18;
(f) Mfuko wa Nishati Vijijini ( *REA* na *REF*);
(g) Mradi wa Umeme wa Mchuchuma;
(h) Uendeshaji wa Tanesco, Utafutaji mafuta na kuwa na Bomba la mafuta kati ya DSM – MWZ;
(i) Ushiriki wa *TPDC* utakao ongeza mgao wa Serikali kutokana Uwekezaji unaofanyika; na
(j) Uendeshaji wa nishati mbadala na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukuaji wa Sekta ya Madini Wizara ilikuwa imeweka malengo yafuatayo:-

(a) Wizara hapa ilikusudia kutumia Mfumo mpya wa utoaji na usimamizi wa leseni za Madini *(Mining Cadastral Information Management System);*

(b) Kupitia upya Mikataba ya Madini;

(c) Uongezaji thamani ya Madini;

(d) Ukaguzi wa gharama za Uwekekezaji na Uendeshaji Migodi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka uliopita Bunge lako Tukufu lilipitisha matumizi ya Wizara hii jumla ya Sh. 465.202.173.000/- ambapo Sh. 32.657.178.000/- kwa matumizi ya kawaida ambayo ni asilimia saba tu ya bajeti yote na shilingi 432.544.995.000/- kwa ajili ya maendeleo ambyo ni asilimia 93 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwengine katika bajeti hiyo ya mwaka jana makadirio ya makusanyo ya mapato yalikuwa Sh. 45,051,406,000/- na hadi kufikia mwezi wa Mei 31, 2007 makusanyo yalikuwa Sh. 45,602,530,700/- sawa na asilimia 101.2 au ziada ya Sh. 551.124.700/-.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa hili naipongeza Wizara hii kwa kuvuka lengo la makusanyo ya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2007, Wizara ilikuwa imeshapokea Sh. 36,153,866,200/- kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 7.8 Tofauti na bajeti iliyopitishwa na Bunge ya Sh. 32,657,178,000/-. Kwa maana nyingine Wizara ilipokea zaidi ya kilichoombwa katika bajeti hiyo ya 2006/2007 ambalo ni ongezeko la Sh. 3,496,688,200/-.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kambi ya upinzani inahitaji maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri sababu ya kupokea ziada hiyo kinyume na bajeti yake mwenyewe aliyoomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za maendeleo zilizopatikana katika bajeti hiyo ya mwaka jana ni Sh. 106,999,165,287/- sawa na asilimia 23. Bado maendeleo yako mbali sana kupatikana kwa hali hii, kwa sababu tafsiri halisi na sahihi ya eneo hili nikwamba fedha iliyopatikana kwa ajili ya maendeleo kwa kipindi cha 2006/2007 ni asilimia 23 tu kutoka asilimia 93 ya kilichoombwa. Kwa maana nyingine ni kwamba vifungu vyote vilivyotajwa katika kifungu II (A) na (B) havikutekelezeka kwa asilimia 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kwamba katika mwaka wa fedha uliopita Tanzania tulikabiliwa na tatizo kubwa la umeme unaotegemea maji kutokana na ukame uliolikumba Taifa, hivyo kulazimisha Serikali kutafuta njia za ufumbuzi za dharura na za muda mrefu kutatua tatizo hilo la ukosefu wa umeme. Naipongeza Serikali kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliweza kuanzisha mradi wa kudumu wa kuzalisha umeme wa *100MW* kwa kutumia gesi asilia hapo Ubungo unaojengwa na kampuni ya Warsila ya *Finland* kwa gharama ya Shilingi billioni 102.372 wastani wa dola za Kimarekani milioni 79.36 . Mradi huu uko katika hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa kudumu wa Tegeta wa kuzalisha Umeme wa *45MW* unaojengwa pia na kampuni ya Warsila ya Finland ambao ulikuwa ukamilike mwezi wa June 2007 pia wa kutumia gesi asilia.Mradi huu umechelewa na kwa taarifa nilizonazo kwamba sasa hivi unategemewa kukamilika mwezi Augosti 2008. Kambi ya upinzani inamuomba Mheshimiwa Waziri atueleze nini kimetokea kilicho sababisha ucheleweshaji huu wa takriban mwaka mmoja. Mradi wa dharura wa Aggreko ambao ulikamilika muda mrefu hivi sasa unazalisha umeme wa *40MW* kwa kutumia gesi asilia. Nachukua nafasi hii kuipongeza Kampuni hii ya Aggreko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya dharura pia Serikali ilifanya juhudi za kukabiliana na Kampuni ya *Alstom Power Rentals* ya Marekani kwa kuzalisha umeme wa *MW40* kwa mkataba wa mwaka mmoja. Mitambo hiyo inatumia mafuta ya dizeli na imefungwa Mwanza na imeanza kuzalisha umeme kuanzia tarehe 19 Machi 2007. Gharama za mradi huu ni Dola za Kimarekani Milioni 116.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulinganisha gharama za mradi huu pamoja na ule wa Aggreko unaozalisha umeme wa *MW 40* vile vile lakini kwa kutumia gesi asilia uliogharimu Dola za Kimarekani milioni 61. Hii inamaanisha kuwepo kwa tofauti ya Dola za Kimarekani milioni 55. Hapana shaka ongezeko hili limesababishwa na gharama ya mafuta ya dizeli yumkini pamoja na masafa *(location)* ya Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Mheshimiwa Naibu Spika Kambi ya Upinzani inajiuliza maswali ni kwanini Serikali ikakodi ingawa kwa muda mfupi mitambo hiyo ya dizeli wakati tayari tuna uzoefu wa *IPTL*? Kwa nini tusitumie Gesi asilia ambayo inazalishwa hapa nchini na uwezekano wa kujenga *reserve tanks* za gesi na

kuisafirisha upo? Namuomba Mheshimiwa Waziri alitoe wasiwasi Bunge lako kwa matumizi ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, zipo njia tatu za kufikisha gesi asilia Mwanza au Mkoa mwengine wowote wa Tanzania. Kwanza, kwa kutumia Visima maalum vinavyoweza kuchimbwa ardhini*(Gas Wells)*. Pili, kwa kutumia *Compressed Natural Gas Tanks (CNG Tanks)* ambayo yanaweza kujengwa kama vile yaliyoko Kisiwa cha Songosongo. Tatu, kwa kutumia Bomba la moja kwa moja *(Direct pipe Line).* Njia ya kwanza na ya pili Gesi inasafirishwa kwa kutumia *Trucks/Pipe line*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tujiulize: Je, ziada ya *USD 55* Million tulizoziona hapo juu haziwezi kuchimba *gas wells*, haziwezi kununua *Special Trucks* za kusafirishia gesi. Haziwezi kujenga *CNG Tanks*. Kwa maana hiyo, Serikali itaweza kujisafisha vipi na matumizi mabaya ya namna hii? Kambi ya upinzani kwa niaba ya wananchi inahitaji maelezo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi ambao umeleta manung'uniko makubwa ndani na nje ya Tanzania ni Mradi wa dharura wa *Dowans Holding AS,* zamani ukijuilikana kama mradi wa *Richmond* wa kuzalisha umeme wa *100MW* kwa kutumia gesi asilia kwa gharama ya Shilingi Bilioni 172.9 wastani wa dola za Kimarekani millioni 134.03.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 23 June 2006 Serikali ilifungiana Mkataba na kampuni ya *Richmond Development Corporation* wa kuleta mitambo ya dharura ya kuzalisha umeme wa *100MW* ndani ya siku 150 na ilifahamika *20MW* ziwe tayari zinazalishwa mwishoni mwa mwezi Oktoba 2006 na zile zilizobakia 80MW ziwe tayari kuzalishwa mwishoni mwa mwezi Desemba, 2006. Kwa kuwa *Letter of Credit (L.C)* ilicheleweshwa na kupatikana mnamo mwezi Septemba 2006, siku 150 inasemekana zilianza kuhesabika kutoka mwezi huo na kufanya tarehe ya mwisho kupatikana *100MW* kuwa ni mwezi wa Februri 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Taasisi ya kuzuia Rushwa ya TAKURU kuingilia kati suala la Richmond na kuchunguza uwezekano wa kiwingu cha rushwa katika zoezi la kupatikana Mkandarasi huyo, lakini bado hali ya hisia tofauti haijasafishika katika taarifa hiyo ya takuru ilyotolewa tarehe 11 Mei, 2007. Baada ya kulinganisha mambo hayo yote kumi Watanzania inafaa tujiulize maswali haya yafuatayo:-

1. Miradi yote miwili inazalisha umeme wa 100MW tofauti kubwa ni muda wa kuanza kuzalisha na gharama. Kwakuwa *Richmond/Dowans* pia haujakamilika na unatarajiwa sasa kukamilika mwezi huo huo wa Agosti 2007. Je, ni halali tofauti au ziada ya Shilingi bilioni 70.528i (wastani wa USD milioni 54.67)?

2. Je, ule udharura uko wapi?

3. Je, fidia ya USD 10.000/- kwa siku za ucheleweshaji kama inavyosadikiwa ndio makubaliano ya mkataba zitaweza kufidia USD 54.67Millioni?

4. Je, ni kwa nini Serikali ilijiingiza kwenye majukumu ya kufungua *L.C* na kutoa fedha kutoka kwenye mabenki yetu ya ndani wakati tulielezwa *Richmond* ni kampuni ya kimarekani yenye uwezo,na ingelipaswa kulipwa kwa utaratibu wa kimkataba?

5. Je, Serikali ilifanya uchunguzi wa uwezo wa kiufundi, kifedha na uzoefu wa shughuli za umeme wa Kampuni hiyo ya Richmond wakati ilishindwa hata kutekeleza masharti ya mradi wa bomba la mafuta kutoka Dar hadi Mwanza mwaka 2005?

6. Vipi Serikali ilithibitisha mahusiano ya *Richmond* na *Pratt Whitney* ya Marekani na kwa vielelezo gani?

7. Kwa nini Serikali isitumie mwanya ule wa *Richmond* kushindwa kutekeleza Mkataba ambapo wakati ule wa mwezi Januari, 2007 Bwawa la Mtera lilikuwa limejaa maji na kutapishwa na umeme wetu wa vyanzo vyote vya maji ulikuwa umerudia uzalishaji katika hali nzuri badala yake wakarithishwa Mkataba Dowans?

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba suala la *IPTL* lilileta matatizo makubwa na manung'uniko makubwa miongoni mwa Watanzania ambayo ni kama haya ya *Richmond/Dowans.* Kwa bahati nzuri katika suala la *IPTL* Serikali ilisikiliza maoni ya Watanzania na kufikia hadi ya kuishitaki *IPTL*.

Kwa kuwa Serikali ilikuwa imeshanasa kimkataba njia pekee iliyotumika ni kwa *ABITRATION* na Serikali ikafanikiwa kupitia uamuzi wa *Abitration* kupunguza *USD 27 millions* katika *USD 150 millions* ambazo *IPTL* walizodai kuwa ni gharama zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa udharura uliotakikana haupo na muda wa kuzalisha *100MW* kwa muda wa siku 150 ulishindikana, na kwa kuwa mitambo hii imechukua muda wa mwaka mmoja sasa hadi kukamilika sawa na Mradi wa Serikali wa *Generator* za Ubungo *(100MW)* unaotekelezwa na mkandarasi Warsila ya Finland. Tofauti kubwa ya gharama za mradi huu nazo hazina maelezo ya kuridhisha. Hata hoja ya kuwa udharura haukuruhusu kutafuta vifaa vya bei nafuu nayo katika kipindi hiki cha mtandao haina msingi wowote. Labda kama wahusika walikuwa wazembe au hawana sifa mahususi.

Mheshimiwa Naibu Spika kimsingi iwapo Serikali haina majibu ya kuridhisha ni vyema Bunge lako Tukufu liunde Kamati Teule kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 104 kuchunguza chanzo cha matatizo. Ni vyema hatua ikichukuliwa dhidi ya

uzembe, au vinginevyo iwapo uchunguzi utathibitisha hivyo badala ya kuliingiza Taifa katika gharama kubwa kiasi hicho na hii itakuwa fundisho kwa watendaji wengine wa Serikali. Pia tutaepuka mgogoro kama ulivyotokea kwa *IPTL* uliotulazimisha hatimae kutumia fedha nyingi sana kupata ufumbuzi wa mgogoro huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukulie *(assumption)* wakati wowote mnamo mwezi Julai/Agosti, 2007 Kampuni za Dowans, *TANESCO* Ubungo (Warsila) na Artumas Mtwara/Mnazibay watazalisha 100MW, 100MW na 8MW kwa mtiririko kama huo, hivyo tutakuwa na jumla kuu ya Uzalishaji Umeme Tanzania *(Total Installed Capacity)* wa 1216 MW.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Ongezeko la matumizi ya umeme tunalolitarajia kwa siku za hivi karibuni na za baadae kwa sababu ya ongezeko la Viwanda, maeneo huru ya uzalishaji *(EPZ), SEZ,* usambazaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya, umeme vijijini na kadhalika, tunategemea mahitaji ya umeme pia yataongezeka kwa wastani usiopungua asilimia 10(10%) *(Load Growth)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Wizara ya Nishati na Madini iliyotolewa kwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara tarehe 28/3/2007 kuhusu mikakati ya kurekebisha sekta ya umeme kifungu cha 13(2) Nanukuu: "Kuongeza kasi ya kuwaunganishia umeme wananchi, Serikali ina mpango wa kuongeza idadi ya wananchi wanaopata umeme kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 ifikapo mwaka 2010." Mwisho wa kunukuu. Maana yake Serikali imekadiria kiwango cha ongezeko la matumizi ya umeme kwa asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza tutizame ongezeko la matumizi ya umeme kwa asilimia 10 tu ili tuweze kupata upeo wa kiasi gani cha umeme tunachopaswa kuzalisha nchini. (tuchukulie $n$ ni idadi ya miaka na g% asilimia ya ongezeko) $P_n = P_{2007} ( 1 + g\% )^n$. Mwaka 2010 tutahitaji kuwa na $P_{2010}$ = $1216(1 +10\%)^3$ sawa na 1618.5MW (ongezeko la uzalishaji wa 402.5MW). Mwaka 2015 tutahitaji kuwa na 2606.6MW (ongezeko la uzalishaji wa 1390MW). Mwaka 2020 *(Mini Tiger Plan)* tutahitaji kuwa na 4198 MW (ongezeko la uzalishaji wa 2982MW).

Mwaka 2025 ambapo ndio Dira ya Taifa ya Maendeleo tutahitaji kuwa na 6761 MW (ongezeko la uzalishaji wa 5545 MW) Kwa kigezo cha Serikali cha asilimia 15 ifikapo mwaka 2010 tutahitaji kuwa na uzalishaji wa 1849 MW ongezeko la 633 MW na kwa lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo Mwaka 2025 tutahitaji kuwa na 15048.5 MW (ongezeko la uzalishaji wa 13832.5MW au 13.8GW).

Matarajio ya hivi karibuni kwa vituo vya uzalishaji ambavyo tayari viko mbioni ni Kiwira (50 - 200 MW) na Tegeta 45 MW jumla 245MW ambavyo bado ni chini ya ongezeko la 633MW Serikali inavyo tarajia ifikapo 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumaini ya Taifa hili kujikwamua kiuchumi inategemea sana miradi ya Mchuchuma, Liganga, Lake Natron Soda Ash, Ujenzi wa maeneo ya Viwanda, *EPZ* na *SEZ*, Utekelezaji wa kanda za maendeleo *(Mtwara*

*Development Corridor* na ile ya *Central Corridor)* na kadhalika miradi ambayo kufanikiwa kwake kunahitaji Umeme wa kutosha na wa uhakika.

Kwa maana hiyo iko haja sasa ya kuvitumia vianzio vyote vya nishati kama vile Ruhudji 358MW, *Stiglers Gorge 2100 MW* na Mchuchuma 400MW. Jumla ni 2858 MW pamoja na miradi ya Kiwira na Tegeta (245MW) ndio tunaweza kuwa na Ongezeko la uzalishaji Umeme wa 3103 MW ambalo ni juu ya kiwango cha 2982MW ili kufikia lengo la uzalishaji wa 4198MW kwa mwaka 2020 tena kiwango cha ongezeko la matumizi ya asilimia kumi kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha Dira ya Maendeleo ya 2025 ni dhahiri kwamba tutahitaji ongezeko la umeme usiopungua 5545MW kwa ongezeko la asilimia kumi kwa mwaka au 13.*8GW* kwa ongezeko la asilimia 15 iliyokusudiwa na Serikali. Kwa maana hiyo, ili tufanikiwe ni lazima matayarisho yaanze hivi sasa kwa kuwa na *PSMP* ya uhakika itakayowezesha *Funding Programmes* za *SAPP* au nyinginezo duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kuweka tahadhari kwamba wakati chanzo chetu kimoja ni cha makaa ya mawe ya Mchuchuma baadhi ya nchi duniani tayari wanafunga Vinu vyao vya kuzalisha umeme kwa kutumia chanzo hicho kama vile *Scotland* na *Ireland* kutokana na sababu za *emission* za *carbon dioxide* kunusuru uharibifu wa *ozone*. Hivyo kubakiwa na chanzo cha Gesi Asilia ambacho Serikali inapaswa kuwekeza zaidi au kile cha *Uranium* ambacho pia kina matatizo yake duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kambi ya Upinzani ina imani kubwa na uongozi mpya wa *TANESCO* ni mategemeo yetu watazingatia ushauri huu wa kufanikisha uzalishaji umeme ili kufikia malengo ya vision 2025 kwa kuharakisha *Power System Master Plan* na utekelezaji wa *Capital Investment Plan*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati mbadala inaweza kuzalishwa hasa kutokana na mazao yalimwayo kibiashara. Mazao kamavile miwa, mawese, mibono, nazi, mihogo na kadhalika yanaweza kutumiwa katika uzalishaji wa *diesel* na *petrol*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kilimo cha mibono ambacho kama nchi yetu itawekeza linaweza kuwa zao mbadala la kibiashara katika uzalishaji wa mafuta ya *diesel*, kwa kuwa zao la tumbaku ambalo linazidi kupigwa vita duniani kote kutokana na madhara yake kwa afya wakulima watakuwa wamepata mbadala wake na wananchi wa Mikoa inayolima Tumbaku nayo itanufaika kiuchumi na zao hili jipya.

Kutokana na tafiti zilizopo gharama za kuzalisha *1MW* ya umeme ni sawa na *USD* milioni moja. Kwa kuwekeza katika kilimo cha mazao yatakayotupa mafuta ya *diesel* na *Petrol* kama mibono na miwa *(bioethanol)* ni jambo ambalo litakuwa limetukomboa na *return on investment* inaanza kuonekana katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na mkataba wa Kyoto wa kupunguza *greenhouse gas emissions* ambao Tanzania ni mwanachama inasema kuwa ifikapo mwaka 2010 asilimia 10 ya *biofuel* lazima ichanganywe na *fosil fuel*, mwaka 2015

asilimia 20 ya *biofuel* lazima ichanganywe na *fosil fuel*, mwaka 2025 asilimia 25 ya *biofuel* lazima ichanganywe na *fosil fuel.* Kwa maana nyingine, kila asilimia 100 ya *fosil fuel* lazima ichanganywe na *biofuel* kwa mtiririko tajwa hapo juu. Hii inatoa mwanga ni kwa kiasi gani hapo mbeleni soko la kilimo cha mibono na miwa litakavyokuwa kubwa na la uhakika. Lazima tuwekeze sasa ili tunufaike na soko hilo. Na hii imewekwa makusudi kwa ajili ya kulinda ozoni isiharibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi yetu kuwekeza katika kilimo cha miwa na mibono kwanza unaongeza ajira na kuongeza wigo wa kodi *(by creating taxable society).* Mabaki yatokana na mbegu za mibono baada ya kukamua mafuta ya disel unaweza kupata dawa za aina mbali mbali pamoja na *organic fertilizer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kulipongeza Shirika la *TPDC* kwa kufanikisha yafuatayo katika kipindi hiki cha mwaka mmoja.

*(a)* *Third-East African Petroleum Conference.* Shirika limeweza kuandaaa na kufanikisha Mkutano wa tatu wa *Petroleum* uliofanyika tarehe 7-9 Machi 2007 huko Ngurudoto Arusha. Mkutano huo ulijumuisha nchi za Kenya, Uganda na Tanzania na kuhudhuriwa na Makampuni mbali mbali Duniani yanayojishughulisha na biashara ya Gesi/Mafuta pamoja na yale ya nayotowa utaalamu wa kisasa na ukodishaji wa zana za utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi. Tanzania (Kenya na Uganda) iliweza kufanikiwa kujitangaza kupitia Mkutano huo pamoja na maonyesho yaliyofanyika hapo katika Hoteli ya Ngurudoto, kwa kuonyesha takwimu za *seismic* mbali mbali zinazoonyesha vivutio na uwepo wa Hydrocarbon katika maeneo ya nchi kavu na baharini.

(b) Baada ya kumalizika Mkutano huo wa Arusha, Makampuni yameongeza kasi ya kuangalia data na kupeleka maombi *TPDC* kwa maeneo machache yaliyobakia. Pia Makampuni yaliyokwisha kuwepo nayo yameongeza kasi ya utekelezaji wa *work programme* zao ili yafaidike na bei ya juu ya mafuta iliyopo sasa hivi kwenye soko la Dunia. Wawekezaji wengi wameonyesha dhamira *(expression of interest)* ya kuwekeza kwenye matumizi ya gesi pamoja na usafishaji Mafuta wakijipanga vyema endapo utafutaji unaoendelea utaleta mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa nilizonazo katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita Kampuni tano zimesaini Mkataba wa Kugawana mapato *(Production Sharing Agreement)* ambazo ni :-

*(1) Ras El-Khaimah (PSA) License-East Panda Block*
*(2) Statoil AS Block #2 Deep Sea*
*(3) Petrobas Block #8 Deep Sea*
*(4) Dominion Block #7 Deep Sea*
*(5) Dodsal Eneo las Ruvu Basin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni maendeleo makubwa kwa *TPDC* na Serikali kwa jumla na hutuna budi kulipongeza na kuwapa moyo ili mafanikio zaidi yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana *TPDC* inakabiliwa na matatizo makubwa ambayo kwa kasi kikubwa yanasababishwa na Serikali yenyewe ambayo kama hayatapatiwa ufumbuzi wa haraka yanaweza yakasababisha madhara na hasara na sio kwa *TPDC* tu bali hata Serikali yenyewe na Taifa kwa ujumla, mfano:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya utafutaji mafuta yaliyowasilishwa Wizarani na kufuata taratibu zote mnamo mwezi wa Aprili, 2002 ili yaletwe hapa Bungeni bado hayajaletwa hadi hivi leo. Mapendekezo yale hayana utata kwani yanagusa vipengele vyote vya kitaalamu ukiacha suala la mgao linaloshughulikiwa na Kamati husika za Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar ambazo hazimalizi kazi. Kutokupitishwa kwa mapendekezo yale kunawaletea Wawekezaji wetu *a crisis of confidence* na kunakwamisha kwa namna fulani juhudi za *TPDC* za kuendeleza utafutaji.

(b) Ongezeko la Mgao wa Serikali kama *TPDC* itapewa Fedha za Kuwekeza Songo Songo na *Mnazi Bay:*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* inajukumu la kuwekeza kwenye miradi ya utafutaji ili ipate mgao kwenye uzalishaji na kuongeza pato la Taifa kwa kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo ya mafuta/gesi hususan usambazaji wa gesi kwa taasisi, majumbani pamoja na usafirishaji.Mikataba ya *PSA* inahitaji *TPDC* kushughulikia kwa fedha yake *(domestic market obligation).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ya *Production Sharing Agreement* huiwezesha Serikali kupitia *TPDC* kupata mgao bila kuwekeza na endapo mwekezaji akagundua mafuta/gesi inayoweza kuzalishwa kibiashara basi *TPDC* hupewa fursa ya kuwekeza kwa kiwango cha asilima 5 hadi asilimia 20 ili kuongeza mgao wake na mgao wa Serikali. Mipango ya uendelezaji wa *additional gas* kwa mfano Mradi wa Songo Songo kiasi cha *USD* 26.1 milioni kitahitajika katika kipindi cha miaka mitatu *(3 years)* ambapo asilimia 20 ya *TPDC* kuwekeza ni *USD 5.22 million*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha na kuhuzunisha ni pale tunapoona katika bajeti ya mwaka huu Serikali imetenga Sh. 315,000,000/- wastani wa *USD* 250.000 tu za maendeleo kwa Mradi wa Songo Songo na kiasi hicho hicho kwa Mradi wa *Mnazi Bay*. Je, Serikali itasema nini fursa hii ikitutoka? Huo uzalendo uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Kamati yangu ya Uwekezaji na Biashara wamezitaja athari zote zinazoweza kupatikana kutokana na athari ya kutoweza kuwekeza. Kwa hiyo, sina haja ya kurudia. Lakini, kwa tahadharisho zaidi, *TPDC* isipowekeza mwanzo, basi itapoteza nafasi hiyo kwa kipindi chote cha mradi. Hii ina

maana kuwa hata mafuta yakigundulikana katika eneo hilo, mgawo wa *TPDC* hautoongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la mafuta, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweze kufufua kiwanda cha kusafishia mafuta ili nchi iweze kununua mafuta machafu na kuyasafisha na hivyo kuwa na uwezo wa kudhibiti bei. Lakini la muhimu zaidi ni kuwa tutaweza kuchanganya wenyewe *biofuel* pamoja na *fosil fuel*. Mabaki katika uchanganyaji na usafishaji ni lami itakayotumika katika ujenzi wa barabara zetu. Katika mchakato huo wote ni utengenezaji ajira kila mchakato wa uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ni sekta nyeti sana na ni sekta ambayo inatakiwa iliingizie Taifa letu fedha nyingi na hivyo kuinua uchumi wetu, lakini tofauti na ukweli huo sekta hiyo imekuwa ikiwanufaisha wachache na kuliacha Taifa pamoja na watu wake wakiwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Alex Stuart katika taarifa yake ya utendaji kazi ilionyesha kwa kirefu ni jinsi gani Tanzania inapoteza mabilioni ya dola za Marekani kutokana na udanganyifu unaofanywa na makampuni kadhaa ya madini mbali ya mapungufu yaliyomo katika sheria ya madini ya mwaka 1998. Ni bahati kampuni yenyewe imekuwa wazi japokuwa kulikuwa na mtafaruku uliotokea, lakini ilitoa mapendekezo kadhaa jinsi madini hasa dhahabu yanavyoweza kuinua uchumi wa nchi na watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli kuwa tunaibiwa umejidhihirisha pale makampuni ya Madini baada ya Watanzania wenye mtazamo tofauti na wale walioko madarakani kupiga kelele, makampuni ya madini yamekubali kutoa kiasi fulani kwa utashi wao mbali ya kile kilichomo katika sheria kuipa Serikali.

Kambi ya Upinzani inajiuliza hicho kiasi wanachotoa ni kwa sheria ipi? Na hii inaonyesha ni jinsi gani wanavyokula kwa mikono miwili badala ya mmoja wa kawaida. Tunaitaka Serikali ilieleze Bunge ile ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupitia upya mikataba ya madini imetekelezwa kwa kiwango gani mpaka sasa hivi ili kuwa na uhakika wa kupata kiwango cha mapato kinacholingana na uzalishaji badala ya kiwango kilichopangwa tu mezani kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini ya vito - *TANZANITE* ni madini yanayopatikana Tanzania tu, hakuna nchi yoyote dunia inayochimba madini haya. Lakini kwa mshangao na ajabu ni kuwa kati ya nchi zinazouza nje madini hayo Tanzania inashikilia nafasi ya mwisho. Kwa mfano, Katika soko la dunia mauzo ya Tanzanite mwaka 2005 yalikuwa na thamani ya Dola za kimarekani milioni 400. Hata hivyo rekodi ya Tanzania ni Dola milioni 16 tu. Tuna taarifa kuwa Kenya ilipata tuzo kwa kusafirisha *Tanzanite* nyingi duniani wakati hawana *Tanzanite*. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atoe ufafanuzi ni kwanini mataifa yasiyochimba *Tanzanite* yanapata tuzo ya kuuza madini hayo kwa wingi katika soko la dunia na sio Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha bajeti ya 2006/2007 tuliuliza maswali mengi kuhusiana na Kampuni ya MEREMETA iliyokuwa imeundwa kwa minajili ya kuiongezea nguvu kimapato Kampuni Nyumbu ya JWTZ. Kati ya majibu yaliyojibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa mujibu wa *Hansard* ni kuwa, nanukuu: "Sasa kwa ufupi, nataka niseme yafuatayo: Kwanza Meremeta amesema imeanzishwa *off-show*, hata mwanzo ndiyo ilivyokuwa na sasa iko katika *process* ya *winding up*. Kwa hiyo, kinachoendelea sasa ni katika mtiririko huo". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa fedha katika kuhitimisha bajeti yake tarehe 23 Juni, 2006 alisema yafuatayo kuhusiana na MEREMETA nanukuu:

"Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni juu ya nani ni wamiliki wa MEREMETA na Mwananchi? Kwa maelezo niliyokuwanayo ni kwamba MEREMETA ni Kampuni ya Serikali iliyoanzishwa kwa lengo la kununua dhahabu kutoka wachimbaji wadogo wadogo. Baadaye Kampuni ilianza mradi wa kuchimba dhahabu katika eneo la Buhemba Mkoani Mara." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati Mheshimiwa Waziri wa Nishati akitoa maelezo ya Serikali kuhusiana na ombi la Mheshimiwa Dr. Slaa la kutaka maelezo toka Serikalini kuhusu tuhuma za ubadhirifu katika *BOT*, alijibu yafuatayo, nanukuu:

"Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapenda kukanusha kauli hizi kwamba Kampuni ya MEREMETA imeuzwa kwa *RandGold*. Kampuni ya MEREMETA haijauzwa kwa mtu yeyote au kwa Kampuni yeyote, iwe kwa bei ya kutupwa au kwa bei ya kuruka. Kama nilivyoeleza hivi punde, MEREMETA imesitisha shughuli zake kwa mujibu wa sheria. Kutokana na hatua hiyo, mali na madeni ya MEREMETA yamehamishiwa kwenye Kampuni mpya ya *TANGOLD* ambayo inamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Mali hizo zinajumuisha pia Mgodi wa dhahabu wa Buhemba". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hizi za Serikali zinautata kwa kiasi fulani, hapa kampuni inasemekana ilikuwa iko katika hatua za mwisho za *winding-up* na Waziri mwingine anasema Serikali imeinunua. Haya kama Serikali imeinunua ilikuwa ni ya nani hapo mwanzoni na ni kwanini ilikuwa chini ya JWTZ? Haya ndio maswali hayajapata majibu tangu mwanzo na ndio msingi wa manung'uniko na malalamiko ya Watanzania, yaani kutokupata majibu ya moja kwa moja kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa Mheshimiwa Dr. Slaa ataleta hoja binafsi kuhusiana na utata huu, lakini ninaomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu kwa hayo niliyouliza. Ni ombi la Kambi ya Upinzani kwa mara nyingine tena, wakati wa marekebisho ya Kanuni, angalau Kambi ya Upinzani ipatiwe saa moja kama anavyopatiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hizi zina mambo mengi ambayo ni mengi sana hatuwezi kuyatimiza kwa nusu sasa. Kwa hiyo, hilo ni ombi kwa Kanuni mpya zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe kwa kunisikiliza kwa makini pamoja na Waheshimiwa Wabunge Wote. Ahsanteni Sana! Sasa nawasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba niwashukuru sana wote waliochangia katika hotuba hii. Katika orodha yetu ya wachangiaji, tunao wengi. Walioomba, tayari wanatosha leo na siku ya Jumatatu, waliokwishaomba, wanatosha kabisa. Mkileta wengine, hamtokuwemo kwenye orodha hii. Kwa hiyo, baada ya hapo napenda nimwite Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Athumani Janguo, sijui yupo karibu sana na yeye alitoka kwenye matibabu. Tunamwona pia Mheshimiwa Doroth Mushi, naye ametoka kwenye matibabu. Lakini yeye atachangia Jumatatu ingawa ni katika wale ambao hawajapata kuchangia hata mara moja na Mheshimiwa Jackson Makwetta. Hawa wanatosha kwa leo. Tuanze na Mheshimiwa Musalika kwanza.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Lakini, kabla sijaleta mchango wangu, napenda na mimi nitoe rambi rambi kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa, alikuwa Mbunge mwenzetu na pia kwa wajumbe wa Chama cha Ushirika cha Mwanza, *NCU* akiwemo aliyekuwa Mbunge, Mheshimiwa Kazi na wenzake wawili waliofariki kule Singida. Mungu aweke roho zao mahali pema Peponi. *Amina!*

Pia, nimtakie heri Mwenyekiti wa Nyanza ambaye amelazwa na nina taarifa kwamba anaendelea vizuri. Mungu ampe ahueni apone mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda nijielekeze kwenye hotuba ya Waziri na kabla sijasahau, napenda niseme kwamba naiunga mkono asilimia mia moja. Mheshimiwa Naibu Spika, ni sera ya Serikali ya Awamu ya Nne kupeleka umeme vijijini. Lakini pia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inasisitiza upelekaji wa haraka wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2000, *TANESCO* ilianza kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika Mgodi wa Bulyanhulu ambao uko Kahama na umeme huo ulikuwa unatoka kwenye Gridi ya Taifa sehemu ya Ibadakuli Mkoani Shinyanga. Nyaya za umeme zilipita katika kijiji cha Karumwa. Lakini awali kuanzia mwaka 1999, wananchi waliahidiwa kwamba umeme huo kama ungefika katika vijiji vyao wangepatiwa umeme ikiwamo Kalumwa na wanao ushahidi, wanayo magazeti mpaka leo wameyaweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu angalia maelezo ya Naibu Waziri ili kuweka ushahidi wa hio. Napenda ninukuu maelezo ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini wakati akijibu swali langu Na. 56 ambalo ilikuwa ni mfululizo wa maswali zaidi ya sita ya kuomba kijiji cha Karumwa kipelekewe umeme. Napenda kunukuu:

“Mipango ya awali wakati njia ya umeme wa *kilovolt 220* inajengwa ilikuwa ni kujenga Kituo cha kupoozea umeme kwa ajili ya kupeleka Karumwa, Geita na Vijiji vya vijarani. Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa fedha, mipango hiyo haikutekelezwa.”

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kupitia Bunge lako Tukufu nimeishauliza maswali mengi sana kuiomba Serikali ipeleke umeme katika kijiji cha Karumwa pamoja na vijiji vingine ambapo umeme huu unapitia. Mwaka huu peke yake nimeishauliza maswali mara mbili; nimeuliza mwezi Februari, lakini katika Bunge hili mwezi Juni, niliuliza swali hilo hilo la umeme. Pamoja na juhudi zangu zote hizo, lakini maswali yangu hayakupatiwa majibu. Mpaka leo hakuna umeme Karumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasisitiza Karumwa ni kijiji, ni mji mdogo na kuna haya yafuatayo, kuna kituo cha afya, ambacho kinahudumia wananchi kutoka Shinyanga Vijijini Wilaya ya Kahama, Sengerema na wale wa Geita wenyewe, zaidi ya watu 200,000 wanahudumiwa na kituo hicho na kina vitanda, kina daktari, kinalaza, kinafanya upasuaji.

Kwa kuwa hakuna umeme wa uhakika imetokea tatizo mwaka jana ambapo daktari kwa kuwa anategemea *generator* isiyo na uhakika wakati anamfanyia mama mmoja mjauzito upasuaji *generator* hiyo ili-*fell*. Daktari yule anaitwa Dokta Mgema akafanya *operation* pamoja na wenzake kwa kutumia kibatari kwenye Kituo cha Afya cha Kalumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, pale Karumwa kuna mnara wa *celtel* kuna shule za msingi mbili, shule ya sekondari, kituo cha walimu *TRC* kuna wafanyabiashara wenye uwezo na wapo zaidi ya 100 ambao sasa hivi wamefungiwa umeme wa jenereta ya mfanyabiashara binafsi huyu bwana aitwa Hussein Kasu nataka nimpongeze kwa sababu amekuwa akisaidia Serikali hapa. *(Makofi)*

Lakini sasa umeme huo hautoshi kwa matumizi kwa sababu hawawezi kufunga *fridgerator*, hawezi kutumia jiko, pasi hawawezi kuwasha viyoyozi na matumizi mengine ya umeme wanahitaji umeme wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba hiyo haitoshi mwaka huu kuna mradi wa kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Wilaya ya Kahama pamoja na Shinyanga, lakini maji hayo yanaanzia *Ziwa Victoria.* Sasa kwa hiyo, mradi huo unahitaji umeme. Umeme huo umetoka katika kituo hicho hicho cha Bulyanhulu na kwa hiyo, nyaya za umeme tena kwa mara nyingine zikapita pale pale Karumwa. Kwa hiyo, Kijiji cha Karumwa kimekuwa kwenye alama ya V. Pamoja na kwamba Karumwa iko kwenye V, lakini Wizara haijawa na mipango madhubuti ya kupeleka umeme pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana juzi mwezi wa nne mwaka huu wananchi wa Karumwa baada ya kuona kwamba Mbunge wamemtuma miaka saba lakini umeme haujafika wakaamua wao wenyewe waandamane. Walipoandamana na mada yao kubwa ilikuwa ni kudai umeme wapelekewe kwenye kituo kile na kwa sababu ambazo nimesema pale juu.

Lakini pia kuna mazao yao katika huu mradi mpya wa kupeleka umeme kutoka Kituo cha Bulyanhulu kwenda Nyamtukuza kwenye maji, hizi njia mpya wakati wanafanya ujenzi hawa wakandarasi waliharibu mazao ya wananchi pamoja na mashamba na bila taarifa ya wananchi hao husika. Kuna kero walifanya zaidi hawa wakandarasi ni Wachina, kuna mmoja alipoulizwa mbona mnaharibu mazao yetu hivi hivi? Wakasema kwa ukejeli na kufuru, "uliza Kwete." Matokeo yake tarehe 28/4 wananchi waliandamana. Sasa walipoandamana kudai haya Serikali ilichukua hatua za kuwakamata na kuwaweka ndani baadhi yao na kuwasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninataka kuuliza mwaka jana mwishoni nadhani mwezi wa Tisa wananchi wa Katoma Geita Mjini waliandamana kama hawa hawa na wao wakachoma gari la mgodi wa *Geita Gold Mine* kwa sababu walikuwa wameondolewa katika eneo lao bila kupatiwa fidia lakini Serikali ilisikia ikakimbia haraka sana ikiwasikiliza na sasa inarekebisha suala la fidia la wananchi wa Katoma Geita. Wakaitwa wananchi wenye hasira hakuna aliyechukuliwa hatua.

Mwaka huu nadhani mwezi wa pili wananchi wa Kakola Wilaya ya Kahama karibu na Mgodi wa Bulyanhulu nao waliandamana kwa sababu wenye mgodi hao walimwaga mchanga ikawa vumbi ambayo walihisi ina sumu. Lakini pia walikuwa wanataka kujua hatima ya kijiji chao cha Kakola ambacho hawa wawekezaji wamewakuta, Serikali ilifanya hima Mawaziri waliongozana kule na wakamaliza tatizo lao. Kijiji wamerudishiwa na mchanga ule ulizolewa napenda niwapongezi.

Lakini wananchi wa Karumwa walipoandamana juzi kudai huo umeme ambao Mbunge wao ameshasema zaidi ya miaka saba wakaonekana kwamba ni wahalifu ni wavunja sheria kwa hiyo wakakamatwa na mengine ambayo yanaendelea siyajui yamefanyika yote nikiwa Bungeni.

Sasa nauliza swali hapa, Serikali ilitumia kigezo gani kwamba wananchi wa Katoma Mjini Geita kuchoma gari kudai haki yao na wakasikilizwa? Ilikuwa siyo uvunjaji wa sheria? Ni watu wenye hasira kali. Wale wananchi wa Kakola kufunga barabara siku mbili tatu wakidai vumbi lizolewe, na kijiji cha Kakola. Wapewe! Serikali ikasikiliza. Walikuwa wenye hasira kali, hawakuchukuliwa hatua. Wale wa Karumwa kudai haki yao kwa zaidi ya miaka saba wakajulikana kwamba ni wahalifu wakachukuliwa hatua. Hivi Serikali nani amewaambia kwamba kule Nyanhwale hakuna wenye hasira? Nani amewaambia hivyo? Sasa nitataka maelezo haya utofauti wa kuwashughulikia wa Kakola na Geita na wale wa Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha maana nilikuwa nataka kusema kwamba wananchi wa Kalumwa wanahitaji huo umeme kwa sababu nilizozisema lakini siyo hivyo tu wananchi wa Nyarubele pale kuna kanisa, kuna miradi mingi pale, wananchi wa Kitongo wananchi wa Ikangala, wananchi wa Nyamtukuza ambako maji yanatoka.

Sasa wamechoka kuwa watazamaji nao wanataka wawe wachezaji wa mechi ndani ya uwanja. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri wakati una-*wind* bajeti yako utenge basi angalau fungu la kuanza kutekeleza mradi wa kupeleka umeme taratibu. *(Makofi)*

Wakati unajibu swali langu tarehe 19 Juni swali hilo hilo ulisema kwamba gharama za utekelezaji wa mradi huo ni shilingi milioni 600 kwa maana ya vijiji vya Karumwa, Ikangara, Kitongo, Nyarubele, Kakola na Nyatukuza lakini gharama za kupeleka kuanzia pale Karumwa peke yake ni milioni 79. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Waziri kwenye kitabu chake kitabu cha *volume II public expenditure* kuna hela hapa nimeziona ambazo nitaomba nitoe shillingi ili niipeleke Karumwa ili akakutane na wananchi wenye hasira akaiombe huko yeye mwenyewe, hizo kwenye *program total* kuna hela ambazo ni *other goods and services not classified* ambazo jumla yake ni milioni 336 ambazo akichukua tu hata milioni 79 kuanzia pale Karumwa mwaka huu itakuwa amemaliza maneno sawa sawa na sera ya taifa kupeleka umeme vijijini na Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya kuharakisha kupeleka umeme vijijini hususan kijiji cha Kalumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja asilimia 100. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii muhimu kwa wananchi wote wa Tanzania na nyenzo muhimu kwa maendeleo ya taifa letu hasa katika awamu hii ya nne tulipojipanga kutekeleza mipango na shughuli zetu kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Lakini kabla sijatoa mchango wangu na kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuongea katika mkutano huu, ningependa kwa niaba ya wananchi wa Kisarawe kupeleka rambirambi zangu kwa familia na jamaa wa marehemu aliyekuwa Mbunge mwenzetu Amina Chifupa kwa kuondokewa na ndugu huyo mpenzi. Msiba wao ni msiba wetu, lakini tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subira na aiweke mahali pema Peponi roho ya Marehemu Amina Chifupa. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniwezesha kufikia hii leo na kuweza kusimama hapa mbele yako baada ya matibabu yangu kule Hospitalini India. Niruhusu pia niishukuru Ofisi yako hasa Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu Foka na wasaidizi wao jinsi walivyoweza kusimamia suala la matibabu yangu. Dini yangu inaniambia usimshukuru mwenzako basi hata Mwenyezi Mungu hutamshukuru. *(Makofi)*

Vile vile napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, waliojali sana na kufuatilia habari ya afya yangu na wananchi wa Kisarawe ambao mara kwa mara walikuwa wakinipigia simu nikiwa hospitalini kwa kutaka kujua ninaendeleaje. Kwa familia yangu nilishashukuru huko nyumbani jinsi walivyothamini na kujali kwao na kunisaidia wakati wote wa mauguzi yangu. Kwenu nyote nasema ahsanteni sina la kuwalipa isipokuwa Mwenyezi Mungu ndiye atakayewalipa leo na kesho akhera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotanguliza kusema, bila ya nishati kwenye maeneo mengi nchini kwetu maendeleo yetu yatasuasua na kasi ambayo Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete anaisisitiza sana haitakuwepo. Kwa hiyo, kwa kipindi cha takriban miaka kumi sasa Waheshimiwa Wabunge wengi, karibu kila mwaka na kila bajeti wamekuwa wakisisitiza mbele ya Serikali kupeleka umeme vijijini waliko watu wengi na kwenye fursa ya kuweza kuanzisha miradi mipya. Lakini kama alivyokiri mwenyewe Mheshimiwa Waziri ni kwamba kasi ni ndogo. Mimi nasema haipo kabisa. Siyo ndogo, inawezekana labda katika Mikoa mingine umeme vijijini umefika lakini katika Mkoa wa Pwani na hasa kwenye Wilaya yangu ya Kisarawe bado umeme wa vijijini hatujauona. Ukiondoa Makao Makuu ya Wilaya na vijiji viwili tu kando kando ya barabara ya Dar es Salaam kwenda Morogoro, Wilaya ya Kisarawe haina umeme.

Katika Wilaya yangu kero kuu ni tatu ambazo ni barabara, maji na nishati. Jana sikubahatika kuchangia katika sekta ya miundombinu kwa sababu nilichelewa kuomba. Lakini niliweza kumwandikia Mheshimiwa Waziri. Jambo moja ambalo halikunipendeza ingawa namsifu sana na nampongeza kwa kazi nzuri aliyoifanya, hotuba yake ilieleza mipango kabambe ya lami karibu katika barabara zote za Tanzania, isipokuwa kwenye Jimbo langu tu. Nami nimeshamweleza na nitamwandikia na ninaamini kwamba kwenye bajeti zijazo Wilaya ya Kisarawe haitasahaulika. Maji; nafikiri nitaipata nafasi ya kuchangia kwenye sekta hiyo itakapofika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie nishati. Nishati ninasema kwa kweli haipo. Mara kwa mara tumeiomba Serikali iangalie hali ya maeneo ambayo yako nyuma sana kimaendeleo hususan kwenye nyenzo kama za nishati. Lakini inaelekea kwamba Serikali bado haijalizingatia hili. Wilaya ya Kisarawe ina kilio kikubwa sana cha maeneo yake mengi kutokuwa na umeme. Kama nilivyosema, ukiondoa zile sehemu chache na Makao Makuu ya Wilaya sehemu zilizobaki hazina umeme. Kwa hiyo, basi naiomba Serikali katika hili na Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho yake aweze kuwaeleza wananchi wa Kisarawe nini mipango yake ya kuweza kuwapatia umeme ili na wao waende sambamba na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa karibu na Jiji la Dar es Salaam kuna faida na hasara zake. Moja ya faida ni kwamba ni soko kubwa la mazao yetu; pili ni kwamba labda wanaotafuta ajira, wachache wanapata. Lakini vile vile kuna hasara zake. Hasara kubwa zaidi ni kwamba kwa sababu ya tatizo la umeme kutopatikana kwa wakati wote na kwa sababu ya bei ya juu ya umeme, watu wengi wa Dar es Salaam wanapikia mkaa na kuni ambazo zinatoka zaidi katika Wilaya za Mkoa wa Pwani. Sasa Serikali iangalie uwezekano wa kuliondoa tatizo hilo kwa sababu sasa hivi Mkoa wa Pwani unageuka jangwa; misitu yote inahama kwa kutengeneza mkaa wa kupeleka Dar es Salaam.

Vile vile Wilaya yangu inapakana na Dar es Salaam. Lakini utakuta maendeleo yanayofanya Mkoa wa Dar es Salaam huchanganywa na yale maeneo ya Mkoa wa Pwani yanayopakana nayo. Kwa mfano katika bajeti ya mwaka 1998/1999 hususan ukurasa wa 31 wa hotuba ya Waziri wa Miundombinu alikuwa ametaja vijiji vingi vya Dar es Salaam vilivyopatiwa umeme ati ni vya Kisarawe. Lakini nilipokuja kuikosoa kwamba vijiji vile

viko Dar es Salaam sikueleweka. Nadhani sasa hivi Serikali inaweza ikajisahihisha kuona kwamba kuna vijiji ambavyo viko Dar es Salaam lakini haviko Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Kwenye bajeti mbili zilizopita tuliipongeza sana Serikali kwa mpango wake wa *Energisation of Rural Transformation (ERT).* Bunge hili pia lilikwishapitisha mnamo mwaka 2005 sheria na mpango wa umeme vijijini kwa njia ya *BOT*. lakini hadi leo mpango huu haujatekelezwa. Watu wa Kisarawe tunauliza hivi Serikali inatuweka wapi wakati sisi tukiamini kwamba ndiyo utakaotusaidia kuanzisha viwanda vidogo vidogo na kuendeleza shughuli zingine za maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niikumbushe Serikali kwamba wakati wa kampeni ya mwaka 2005 wananchi wa Kisarawe walifurahi sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais alipoahidi kuwapatia umeme hususan kutokea Mlandizi Wilaya ya Kibaha kuingia Mzenga, Maneromango na kutokea Kisarawe, Masaki hadi Maneromango. Lakini ahadi hii mpaka hivi sasa haionyeshi dalili ya kutekelezwa. Katika kufuatilia kwangu kwa kuongea na Waziri aliyekuwepo, alinithibitishia kwamba mwaka huu kungekuwa na mradi wa kufanya angalau *survey* ya kupeleka umeme ili kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais. Inaelekea ahadi hii bado haijaweza kutimizwa kwa sababu nusu mwaka wa 2007 imekwisha na dalili hizo hazionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa umeme katika Wilaya ya Kisarawe na sehemu nyingine za Mkoa wa Pwani unasababisha athari nyingi zikiwemo kushindwa kuendeleza hata viwanda vidogo vidogo, kushindwa kusindika matunda na vyakula vyetu vingine mbalimbali kuoza kwa mazao kwa sababu ya matunda hayo kukosa vipoozeo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali haitaharakisha upatikanaji wa umeme vijijini maeneo yetu yatageuka kuwa jangwa na dira ya maendeleo ya Chama cha Mapinduzi, kufikia mwaka 2025 itakuwa haiwezekani kufikiwa katika maeneo haya. Vile vile hata katika *millennium development goals* hatuwezi kuzifikia kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana kuona katika hotuba hii kwamba mwaka huu mpango na sheria ya umeme vijijini vitapatiwa msukumo wa Serikali kwa kuanzishwa mfuko maalum wa umeme huo na Serikali kuchangia shilingi bilioni 10. Kama tulivyoambiwa na Mwasilishaji wa Taarifa ya Kamati iliyoshughulikia Wizara hii, fedha hiyo haitoshi. Pamoja na udogo wake tunaiomba Serikali ihakikishe kuwa Mkoa wa Pwani hasa Wilaya ya Kisarawe zinaingizwa kwenye mpango huu mapema, napenda kurudia mapema, tukichelewa tutaendelea kila wakati kubaki nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sina haja ya kengele ya pili kunifikia. Ni tegemeo langu kwamba Mheshimiwa Waziri amesikia na Serikali imesikia na kwamba wataliangalia suala hili kwa makini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Janguo kilio chako kimefika.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii na pili ningependa nitumie nafasi hii kuwashukuru nyote kwa dua zenu, sala zenu, ubani wenu kwa kushiriki kumsindikiza ndugu yetu Mheshimiwa Amina Chifupa. Alikuwa mjukuu wangu, anatoka Njombe Lupembe, kwa sababu kama alivyosema ndugu Komba jana tunaomba yaishie pale. Kwa mtu uliyefiwa kuendelea kusema juu ya mtu uliyempoteza ni kama kufumua kidonda kinachopona. Tunakosa maneno ya kuelezea kwa ndugu zetu kwa yote waliyotutendea.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo ili nisisahau hapa nimesimama kuunga mkono hoja ya Wizara hii. Katika kuunga mkono ningependa nipongeze hili shirika la *TANESCO* wengi na sisi tunajua mabingwa wa kutoa makosa lakini sijui kama kuna shirika la aina hii katika Bara la Afrika lililofanyakazi kama hii, ni shirika la *TANESCO* katika mazingira magumu. Nashukuru na ninashangaa bado linaishi lakini natumaini wajibu wetu kama Wabunge ni kutusaidia lisimame ili lisife kama Shirika la Ndege.

Kuna wakati karne ya 18 na 19 bara la Afrika liliitwa Bara la Giza kwa sababu habari zake zilikuwa hazijulikana Ulaya, ilikuwa wakati wote liko vitani, wakati lina shida ya njaa, umaskini kupigana vita lakini ilikuwa kama ni *metaphor* neno lile kutumika lakini kama leo ungetembea usiku kwa mabara yote ya dunia kwa ndege bado ungeona Bara la Afrika ndiyo bara lililo na giza kuliko mabara yote katika dunia leo kwa kukosa umeme. Kwa hiyo, neno lile Bara la Giza mpaka leo bado linafaa tena. Ni Bara la giza kwa maana ya kukosa mwanga kwa sababu ya ujinga kwa sababu ya kuendelea kupigana sisi wenyewe, kwa sababu ya magonjwa, kwa sababu ya umaskini. Sasa karne hii bado hakuna mwanga unakwenda kulala saa mbili, hamuwezi mkaonana tutaendeleaje? Mkongwe wa Ukomunisti nadhani *Marx* au *Lenin* alisema hakuna maendeleo vijijini bila umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo maana yake ni kusambaza umeme. Sasa juzi hapa mimi nilikuwa Wilaya moja nilidhani mimi niko hali mbaya zaidi lakini nikatambua kwamba mimi ni afadhali kidogo. Sasa mimi nimesimama hapa kushukuru vile vile kwa sababu ya Serikali wakati huu pamoja na matatizo kwa kushusha umeme pale Makambako. Kushusha umeme wa grid ulikuwa unapita tu kama reli ya *TAZARA* inapita humu Kilombero mpaka huko Zambia lakini hakuna barabara za katikati kusaidia kupeleka mizigo ili itumike. Juzi wameshusha na kwa kufanya hivyo nadhani robo tatu ya Wilaya yangu itakuwa na huo mstari wa umeme unaotoka Kusini Magharibi, Kusini Kaskazini, Kaskazini Magharibi.

Sasa nilikuwa napendekeza kwamba labda mfuko wa umeme wakishirikiana na Wilaya kama wanavyofanya barabara kuwe na mifuko ya umeme ya kata ili vijiji shule, zahanati, zipate umeme. Vinginevyo itapita hivi hivi tu, inapita waya na watu wanabaki pale pale. Hatua hii ingesaidia sana na nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, utusaidie hili kwa sababu shule nyingi za sekondari au vijiji viko pembeni tu mwa huu waya wenye umeme. Katika ule mkataba tulisema pale unapopita basi vijiji vya jirani vitapewa

umeme. Sasa tungepeleka kwenye shule za sekondari zilizo katika vijiji vile. Leo huwezi kuendesha elimu yoyote bila umeme. Leo usipojua kusoma na kuandika ni kujua kompyuta. Nyie wote mliosoma zamani kama hamjui ni *semi illiterate* hata mimi kwa maana hiyo kwa sababu kama hujui kutumia kompyuta utachotaje elimu kutoka nje. Kwa hiyo, nilidhani umeme ni nyenzo ya lazima katika hospitali, zahanati, hata maji na kuharakisha maendeleo. *(Makofi)*

Ndugu zangu wengine juzi tulipokwenda kumzika Amina nadhani mliona pale palipo na umeme pana tofauti na mahali pasipo na umeme. Palipo na umeme pana dalili za maendeleo na kasi ya maendeleo inakwenda. Pasipo na umeme mnaona dalili tu kwamba ni giza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mkristo lakini huwa sielewi kama kweli sisi tutakuja kufufuka na kuwa kama hawa wenzetu. Pale Makambako ni *hub* ya maendeleo kwa maana ndiyo *hub* ya barabara, *hub* ya mawasiliano ya simu na hivi sasa ni *hub* ya umeme. Lakini watu tumejenga ule mji ni mji ambao ni mji wa vijiweni tu hakuna viwanda, hakuna kitu *loopen proletarians* wamekaa pale.

Sasa kwa mtindo huu na kwa Njombe ilivyo sasa hivi imeendelea kilimo tunadhani tunaweza kwenda kwenye *Agro industrialization* kwenye viwanda kuna mbao, kuna matunda, unaweza sasa uka-*create employment* kwa vijana kutengeneza vifaa kwa sababu pana hii nyenzo muhimu yaani umeme.

Tuna maji ametaja Waziri Makali, Ruhuji unaanzia kule sasa kama hatuchukui hatua kama alivyosema Mheshimiwa Janguo hapa kule kwenye source ya umeme ambao ndiyo *renewable energy* kule mngepeleka umeme ili kuzuia ukataji wa miti ili umeme uendelee. Vinginevyo kuzuia mkaa Dar es Salaam wakati huna njia nyingine kwa kweli unakuwa kama huelewi unachokifanya. Wasipeleke mkaa halafu utapikia chakula kitu gani. Hebu fikiria maisha ya Mtanzania bila nishati.

Nadhani *we are myopic* tungesema kila Mji wa Tanzania katika nishati Dodoma uwe na eka 10,000 za miti, Iringa 10,000 za miti yaani nishati, kila Mji, kila Kijiji hii ndiyo lugha ingeeleweka. Baada ya muda kutakuwa na ukombozi. Lakini hii lugha hakuna, panda miti, miti hii inakwenda chini au inakwenda juu mbona haionekani. Kila Mji, kila Kijiji kiwe na shamba la Nishati. Kwa njia hiyo nchi itakwenda. Lakini tukiendelea na maneno hayo nchi hii itabaki nyuma. *We are talking too much!* Hii ni nchi ya watu *rhetoric,* yaani kila mtu ana maneno mazuri lakini *(no action)* hakuna vitendo. Wewe je, mimi nina eka karibu karibu 15 za miti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Na mimi ni shahidi. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Nadhani hata Naibu Spika anaweza kushuhudia. sasa kila mmoja aliye na miti zaidi ya eka 40 anyooshe mkono hapa hakuna.

Kwa hiyo nadhani haya ndiyo baadhi ya matatizo tuliyo nayo Watanzania, *we talk too much* vitu ambavyo vina majawabu hakuna. Kabla ya kumalizia naomba baada ya

mabadiliko ya umeme unaoelekea Lupembe kutoka Njombe tunapewa kwenye kiwanda cha Chai, sasa unapelekwa ng'ambo yaani kwenda kuelekea Songea kwenye kijiji cha Kiloshi, tunaomba upitie Mgololo watani wetu wanataka kujenga kiwanda cha chai badala kujenga mahali pengine popote pasipo na faida. Hilo ni ombi moja.

La pili, vijiji kati ya Igongolo *we pritend you know it* Igongolo na Ibumila, vijiji hapa kati kati ni vingi sana watu ni wengi sana. Pale ndiyo penye maendeleo makubwa. Lakini hakuna umeme. Na kwa sababu inapita kwenye kijiji cha Ikando, basi *extend northwards* kusudi vile vijiji vyote viweze kupata umeme. Baada ya kusema hivyo, kama ulivyosema, umakali iko Nyanda za Juu, Ruaha Nyanda za Juu, Ruhuji Nyanda za Juu *any* nguvu ambayo ni *releable* na ni *re-newable* ni nguvu ya maji, kama tungeweza kuzuia maji yasikauke, ndiyo ya kuaminika zaidi. Ya pili ni ya upepo, hii gesi, petroli na nyingine hii, hii siyo *re-newable* hii inakwisha nayo vile vile. Lakini hiyo nyingine haiishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuelekeze nguvu yetu katika maeneo ambayo kwa kweli tunaweza tukasaidia nchi yetu. Tusipokuwa na mikakati hiyo, bara hili kama lilivyokuwa likiitwa miaka michache iliyopita, litaitwa Bara la Giza tena. Kwa hiyo, tafuteni kwanza maendeleo ya umeme na mengine yote yatafuata. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Sasa nawashukuru sana waliozungumza, wameniokolea nafasi ya mtu mmoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Ndiyo atakuwa msemaji wa mwisho mchana huu.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda nishukuru sana kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda niungane na Watanzania wenzangu kwa kuweza kutoa salamu za pole na rambirambi kufuatia vifo vya wapendwa wetu wakiwemo Mbunge mwenzetu marehemu Amina Chifupa na vile vile Wabunge ambao walikuwa Wabunge wa Bunge hili kipindi kilichopita, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Chubi, na vile vile watu ambao walifariki kwenye ajali pamoja na Mheshimiwa Stephen Kazi, Ndugu William Kasubi na Mzee Ndono. Vile vile napenda nitumie fursa hii kumtakia kila la kheri na aweze kupona Mama Bulugu ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Mkoani Mwanza Nyanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania siku zote lazima tufike mahali tukubaliane kwamba kama kitu kinakwenda vizuri tupongeze. Lakini kama hakiendi vizuri vile vile tushauriane tukosoane. Mimi napenda kwanza niwapongeze Mawaziri wa Wizara hii nikianza na Mheshimiwa Nazir Karamagi. Ni Waziri ambaye ameonyesha ushupavu wa kazi yake na mimi namfahamu kwa sababu tumesoma wote, wakati anamaliza *Masters* na mimi naingia *Masters* kwenye Chuo hicho hicho.

Vile vile Naibu wake Mheshimiwa Ngeleja, wameonyesha umahiri mkubwa sana katika Wizara hii. Lakini Wizara hii ni Wizara ambayo ni ngumu sana. Ni Wizara ambayo Watanzania lazima tukubali, lazima tubadilishe *mind set* yetu twende na wakati. Katika Wizara hii umeme ni siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni uchumi. Kila Mheshimiwa Mbunge hapa ukimgusa suala la umeme linamgusa kwa njia moja au nyingine. Sisi tunasema kwamba tunataka nchi hii sasa ibadilike iweze kupaa. Hatuwezi kupaa kama kijijini bado watu wanatumia nishati ambayo haifai. Ni lazima tubadilishe mfumo mzima wa matumizi ya nishati yetu, tubadilishe mfumo mzima namna ya kuweza kuweka mchakato mzuri wa kukuza uchumi katika ngazi ya vijijini. Leo hii vijana wanasoma shule wanatumia vibatari, huu ni mfumo wa kizamani. Lazima tuweke mkakati madhubuti ambao utaweza kubadilisha sura nzima ya Watanzania waweze kupata elimu na kukuza vipato vyao kwa kutumia *resources* ambazo ziko katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka sasa wa tatu, ninazungumzia umeme kwa vijiji vyangu katika Jimbo la Busega. Kuna vijiji ambavyo viko kilomita 12 ukiwa barabara ya kutoka Nyanguge kwenda Musoma. Kuna vijiji viko vinne, ni kisiwa. Huku kuna umeme kutokea Bunda mpaka Ramadi lakini kutokea tena Nyashimo kwenda mpaka Mwanza kuna umeme. *Gap* ni kilomita 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa tatu ninauliza juu ya kupatikana umeme katika maeneo haya. Naahidiwa kweli na Serikali. Ninaambiwa kwamba pesa zikipatikana katika bajeti hii tunakupa umeme. 2004 ikapita kapa. Mwaka 2005 kapa, mwaka 2006 na yenyewe imepita kapa na kwa kweli hata Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye uko hapo sasa hivi, uliweza kuuliza swali hapa Bungeni kwa niaba yangu na ukajibiwa na majibu ninayo kwamba katika bajeti ambayo imekwisha mwaka huu

walipaswa kupata umeme, vijiji vya Kalemela, Nyamikoma, Kabita, Nyakaboja, hawajapata umeme mpaka leo hii. *(Makofi)*

Nilikuwa naomba katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anisaidie sasa kuniambia kwamba hawa wananchi watapata umeme lini. Lakini tuna kinu cha kuchambulia pamba cha Ngasamo, hiki ni kinu muhimu sana kwa sababu kinachangia sehemu kubwa sana ya pato katika nchi hii na hasa katika sekta ya pamba. Hiki kinu kimeshindwa kufanya kazi kwa sababu hakina nishati, hakina umeme wa kukiendesha.

Vile vile tuna hospitali ya Mkula, ni hospitali kubwa sana ambayo inahudumia wananchi wengi, wananchi wa Wilaya ya Bariadi na Mkoa wa Shinyanga na wananchi wa Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara, wananchi wa Wilaya ya Magu, wanaitegemea sana Hospitali hii na ndiko ambako hata ni nyumbani kwao na Mbunge ambaye anazungumza leo hii. Hakuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku kila nikizungumza nina makabrasha hapa mengi tu ya ahadi ya Serikali. Sasa naomba leo hii Mheshimiwa Waziri anisaidie kuniambia sasa kwamba hiki kilio cha wananchi wataendelea kulia mpaka lini?

Juzi hapa katika Mkutano huu wa Bunge Serikali iliahidi kwamba imetenga fedha milioni 93 kwa ajili ya kuweka umeme katika maeneo haya niliyoyataja baadhi walau kwa kuanzia. Sasa nilikuwa naomba kweli hii kazi ifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwakumbushe Watanzania, Watanzania hatujiamini lakini tuna uwezo mkubwa sana na hata unaposafiri nje kidogo ya nchi mfano nchi jirani tu hapa Rwanda, wanasema kwamba mipango mingi wameichukua Tanzania ambapo sisi tumekuwa tukiisema tunasema, tunasema, tunasema, utekelezaji haupo. Wenzetu wanachukua sisi tunadhani kwamba hii nchi itajengwa na watu kutoka nje, haiwezekani! Leo hii *TANESCO* ameingia Dr. Idrisa Rashidi kwa muda mchache tumeona *TANESCO* imefanya *turn around* hivi Watanzania kama hawa lazima tuwa-*support*. *(Makofi)*

Tumekaa na *Net Group Solution* hapa kwa miaka miwili ilichokifanya ni kutuingiza katika mkenge wa hali ya juu sana. Matokeo yake watu wanayaona sasa hivi. Sasa ifikie mahali Watanzania ambao wanaweza kuwa na uwezo wapewe nafasi waendeshe nchi hii. *(Makofi)*

Sisi tuaminiane tusidhani kwamba wanaotoka nje ndiyo wanaoweza kujenga nchi hii. Ni sisi ndiyo tuna mustakabali wa kujenga nchi na si mtu kutoka nje. Hebu tutumie uwezo wa watu wetu. Mimi kwa kweli naomba Wabunge wenzangu, watu kama Idrisa Rashidi tuwaunge mkono. *TANESCO* ina hali mbaya sana. Lakini bila kuwaunga mkono na kuwapa jitihada za makusudi kabisa hawawezi kutatua matatizo ambayo yanatukabili. Mimi naomba Serikali ikiwezekana hata kama ni kukopa pesa tunakopa pesa ku-*finance* miradi ya umeme vijijini ambayo tutaona *impact* yake ni bora tufanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa nyingi tunakopa huioni inafanya kazi gani. Tumepata pesa kwa ajili ya MMEM na MMES tumeona matokeo yake vijijini. Shule za

msingi zimejengwa, lakini sasa tufanye jitihada za makusudi tutafute fedha kwa kweli tu-*finance* sekta ya umeme. Kwa sababu unaposema unataka kukuza uchumi ni pamoja na kuhakikisha kwamba umeme unapatikana ili uweze kuchochea maendeleo ya uchumi katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa dhati sana, na kwa kweli katika bajeti ya Wizara hii tuwaunge mkono Mawaziri hawa. Bajeti yao ni nzuri na mipango yao ni mizuri. Lakini hawawezi kutekeleza kama hatuwezi kuwa-*support* lazima tuwa-*support.*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wajibu wetu sote kwa pamoja, kuweza kusaidia katika sekta hii. Lakini kingine nitapenda nipate maelezo kidogo katika suala zima la madini. Tumeona katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Sekta ya madini imekua kutoka asilimia 15.7 mpaka asilimia 16.4 kwa mwaka juzi na mwaka jana. Na tumeona kabisa kwamba mapato yameongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 711 mpaka dola milioni 856.8. Hii ni dalili nzuri sana.

Tumeona vile vile bei ya dhahabu imepanda kwa mfano kutoka dola za Kimarekani 445 mpaka dola za Kimarekani 604. Hii ni nzuri! Lakini hoja yangu ya msingi Watanzania wanashirikishwa namna gani katika mfumo mzima huu wa kumiliki migodi. Kwa sababu hii kitendawili tumeona kwamba migodi mingi inamilikiwa na watu kutoka nje kwa asilimia 100. Watanzania tunasubiri kupata kodi na mapato mengine. Lakini hawa watu wanapowekeza kutokana na Sheria yetu ya Madini wanapowekeza tunawapa nafasi ya kuruhusu ile *capital allowance* kwa ajili ya mitaji yao. Wanawekeza kwa miaka 7, 10, 15, 25 bila kulipa kodi ya mapato.

Tunategemea sisi tupate kodi zingine zinazotokana pengine na *statory deductions* na *service and goods, taxis* na kadhalika. Lakini haitoshi ni kwa vipi Watanzania tunawashirikisha katika kumiliki migodi hii hilo ni ndiyo suala langu la msingi. Kwa sababu hii migodi inakwisha, baada ya muda hatimaye itakwisha. Watanzania tutabakia tunasema nini. Halafu cha ajabu ni kwamba mimi nimefanya kazi kwenye kampuni ya Migodi kwa miaka minne. Kuanzia kwenye *exploration* mpaka kwenye *mining.* Hii ni hadithi, leo hii mgodi unauuza unasema unauza mgodi ambao uko Geita, Mgodi wa Geita unauzwa kwa mwekezaji aliyeko labda nje ya nchi. Na unauzwa kwenye *stock exchange* yule anapata pesa wakati nchi haipati hata senti tano kutokana na *transfer* wa ile *property* hakuna *stamp duty.*

Yaani mtu anauza kwa mfano mgodi wa Geita ulizwa kwa dola milioni 232 kutoka S*amarks* kwenda Ashanti. Hii *transfer* hata senti tano Serikali haikupata. Sasa ninachosema ni kwamba tufike mahali Watanzania haya tuyaangalie haiwezekani watu waka-*own property* zetu *a hundred percent* bila nchi kuweza kunufaika moja kwa moja.

Ninachoshauri ni kwamba katika majadiliano ya kuhusu suala la mikataba hili tujaribu kuliangalia sana, huko tuendako Watanzania tutakuja kulia kama kilio cha mbwa. Mbwa akipigwa analia kweli.

Sasa hivi tunataka tufikie pale. Ninachoomba hili libadilike. Halafu sasa mimi hili haliingii akilini unaposema kwamba huyu mwekezaji tunamwambia achangie dola

laki mbili tena tunamwomba kama hisani. Achangie dola laki mbili kwenye Halmashauri ambayo mgodi uko pale.

Nimesikitika kwamba mgodi wa Geita mpaka sasa hivi eti bado wanaombwa waweze kuchangia. Hawajakubali bado hivi tunakwenda wapi jamani. Tunakwenda wapi jamani? *We want to change, there is no way out.* Halafu unakuta kwamba katika hili mwekezaji ametoa *a good will tax* dola milioni saba. Ametoa kwa kujisikia yeye mwenyewe kwamba naweza nichangia dola milioni saba hivi kama hana faida atatoa dola milioni saba? *Are we serious?* Hapa kuna kodi hapa tunaiachia hapa kuna mapato mengi sana tunalia tupate umeme hebu watu tuwakamue walipe hii kodi i-*finance* miradi ambayo ina maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafuta kama *TPDC* hatuwezi kuipa uwezo wa kuweza ku-*control* kuagiza mafuta hapa nchini, Mama Meghji amesema kwamba atawadhibiti waletaji mafuta hawatapandisha bei. Mimi naona hii ni hadithi ndefu sana. Lazima tufikie kwamba nchi tuwe na *control mechanism* hawa watu ambao wanaagiza mafuta kuwe angalau na waagizaji wawili au watatu basi ndiyo waagize mafuta yote halafu tuweze tuka-*control* kwa sababu mtu anapoagiza kutoka nje huwezi ukam-*control* juu ya *price.* Atakuwa amenunua katika *source* bei yangu ni hii hapa. Utam-*control* vipi. Nilikuwa nashauri kwamba hebu tushirikiane vizuri. *EWURA* watusaidie. Naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naungana na wenzangu wote waliotoa rambi rambi kwa sababu ya muda na kwa sababu nilikwishatoa rambi rambi naomba niendelee. La kwanza namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie taarifa mbili ya kwanza ripoti ya Dr. Kipokola ambayo ilifanywa baada ya Bunge hili na Wabunge wako kulalamika sana juu ya mwenendo mzima wa Sekta ya Madini, Serikali ikaunda Tume ya Dr. Kipokola na mpaka leo hatujaona taarifa yake humu Bungeni, naomba hilo liwe la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba taarifa ya Alex Stwart nayo vile vile tuipate ili tuweze kuifanyia kazi. Nimetangulia kusema hayo kwa sababu mapendekezo ya ripoti hizo zote mbili leo yangekuwa yametuletea mabadiliko makubwa katika sekta ya madini. Lakini mpaka sasa hazijaletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni kwamba nilitegemea katika hotuba ya Waziri kuna miradi ambayo Serikali ama Serikali yenyewe moja kwa moja au kupitia *BoT* wamenunua hisa. Sasa nilitegemea Waziri katika taarifa yake ataeleza na hakusema chochote.

Sasa kwanza sina hakika kama *Mwananchi Gold* ni *private company or ni public company* lakini ninavyofahamu ni kwamba tarehe 17 mwezi saba 2005 *BoT* ilitoa dola 95,000 sijui zilikuwa za nini. Halafu ikatoa *allowance* dola 7,920 na halafu ikatoa tena *advance* ya laki tano, ikatoa *transfer to Embassy* ya Kinshasa dola milioni moja na laki tano. Halafu ikatoa na mkopo dola laki nane ikawa jumla ni dola milioni 2.87. Nilitaka kujua tu hizo pesa zimekopeshwaje zimetolewaje, na kama ni *devidend* ya Serikali au ni

nini labda mtueleze na tuone ni manufaa gani yalipatikana katika *investment* hii iliyofanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa *Mwananchi Gold* mpaka sasa umeshapata kama shilingi bilioni 6.9 ikiwa ni pamoja na tarehe 30 mwezi wa sita zilipatiwa 3.4 billioni. Naomba taarifa hii Mheshimiwa Waziri nayo atupatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningeomba Waziri anieleze ni kwa namna gani wameshindwa kufikia makubaliano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa sababu ninavyofahamu suala la mafuta ni suala la muungano na kama Bara wameendelea kutafuta mafuta, ni dhahiri kwamba waliishirikisha Zanzibar wakijua mapato yatakayopatikana katika mradi mzima. Ni vipi sehemu moja ya Jamhuri tayari mradi unafanya kazi. Sehemu ya pili ya Jamhuri mradi haufanyi kazi. Sasa lazima kuna makubaliano mliokubaliana au vinginevyo ndiyo maana imekuwa vigumu kupata *solution* ya tatizo la Zanzibar kwa sababu hawajui matokeo ya miradi inayoendelea upande wa Bara.

Sasa mimi nafikiri Serikali itueleze ni vipi imefikia uwezekano wa kuendelea na ma-*block* mengine kufanya kazi wakati suala hili la muungano lakini ule wa Zanzibar ikawa kuna *negotiation, negotiation* zinazoendelea ambazo hazimaliziki. Ningependa kupata maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne ni suala zima la madini. Nchi yetu hii ina maeneo mengi sana ya madini. Nakubaliana kabisa na shemeji yangu Mheshimiwa Chegeni kwamba kama Watanzania hatukuweza kuwarithisha rasilimali hii tutapata matatizo makubwa sana mbele ya safari.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuanzia sasa warithishwe raslimali zao kwani inasikitisha sana kwamba sasa tunayaanzia makampuni mengine yanayokuja, wakati tuna tatizo la sheria tuna tatizo la mikataba na makampuni mapya bado yanaendelea kuendelea na makosa yale yale ambayo tunayafanya.

Ndiyo maana tunakwenda kuwabembeleza kuwabembeleza. Wenzetu Congo wameweka miezi minne wamepitia mikataba wamemaliza na watu wamepewa haki zao. Nchi imejua haki zake. Sisi tunaogopa nini, tunawabembeleza hawa chini ya rasilimali zetu. Sisi hatuelewi kwa kweli. Sasa mimi ushauri wangu ardhi yote yenye rasilimali Tanzania kwanza warithishwe Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Wakishapata hati hizo hati ziwe *registered* kwenye *Tanzania Investment Centre* anayetaka kuja kufanya *investment* aambiwe kwenye benki yetu pale kwamba kama unataka mgodi wa aina fulani mwenyewe ni Mtanzania fulani. Serikali imwezeshe huyo Mtanzania angalau kufanya ule uchunguzi wa kwanza ili awe na *data* ya kuweza kuuza mradi wenyewe.

Hiyo njia peke yake utawaridhisha Watanzania marasilimali ya nchi hii vinginevyo tutaendelea na *royalty* ya asilimia 3 nchi inabaki mashimo, na watu

wanaendelea na umaskini na watu hawataondokana na umaskini. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba lazima Watanzania warithishwe mali hii kwa kugawiwa wao kwanza maeneo. Ndiyo ujasiriamali sijui unaitwa. Wapewe maeneo Watanzania, halafu yawe *registered Tanzania investment centre* kama vile tunavyofanya kwa ardhi. Halafu *investor* anapokuja aende *Tanzania Investment Centre* wewe unataka kuwekeza kwenye nini, basi mwenye *nikle* ni Mtanzania ni fulani na fulani na fulani.

Serikali wasaidie kupata zile *information* za kuweza kuuza ule mradi wao, lakini vinginevyo mimi nawajua *investors* wa madini hapa wanakuja wanawaandikisha na Watanzania wanakwenda kwenye *Stock Exchange* wana *make billions and billions of money* Watanzania wanabaki maskini hapa ndani ya nchi. Hilo lilikuwa la kwanza katika suala la madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa ni watu wa bahati mbaya sana. Bahati mbaya ni kwamba kila siku kila hotuba tunayosema, tunawaendeleza, tunawaendeleza, hakuna takwimu yoyote iliyotolewa hapa ndani ya Bunge kusema kutokana na mwaka huu tulivyowaendeleza wachimbaji wadogo wadogo wameweza kupata kilo fulani za dhahabu hakuna. Kwa hiyo, ni maneno tu ya kila siku wanaendelezwa. Wao wakikaribia kwenye migodi mikubwa ni rahisi sana kupeleka mbwa na *FFU*. Lakini wenye migodi mikubwa hata kama hawajalipa kodi hata siku moja toka walipokaa pale hakuna chombo chochote kinachofuatilia.

Mfano mzuri wa *Williamson Diamond*. Wale ndugu zangu wa Kisukuma pale wanaotafuta almas miaka yote wanapelekewa FFU lakini Williamson Diamond toka 1994 mpaka leo haijalipa d*evidend* wala hajalipa kodi. Hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri haikusema chochote juu habari hii. Alichosemea ni *royalty* inayopatikana kutokana na almas inayochambuliwa London. Na huko kuna pesa nyingine hata haijachukuliwa mpaka leo. Sasa nasema hawa wachimbaji wadogo wadogo kama hawajarasilimishwa rasilimali hizi na wakapewa hati na wakasaidiwa utafiti, hawawezi kabisa kuondoka na matatizo ambayo wanapata ambayo wanapata hivi sasa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naomba kabisa suala la wachimbaji wadogo wadogo tupate kabisa tathmini sahihi na mimi naamini kabisa ripoti ya Dr. Kipokola ilifanya kazi kubwa sana. Lakini nasema ripoti hizo zinaishia kwenye *shelves* na tunaendelea na matatizo hayohayo kila siku. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, nikitaka vile vile Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho atupatie majibu ya *Williamson Diamond* na hisa zetu tumepata nini mpaka leo na kama tunaendelea tu kwa kuridhia mkataba ambao haupo tena umesha-*expire* ule mkataba haujawa *re-newed* mpaka leo au ndiyo katika huu utaratibu wa kupitia ule mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la mikataba. Inasikitisha Tume mbili zimechaguliwa ya Dr. Kipokola na Alex Stwart, yote kazi yake moja ni kupitia mikataba. Tulitegemea katika Bunge hili sasa baada ya kutumia dola 65 milioni kwa Alex Stwart tungeambiwa faida iliyopatikana kutokana na *investment* hiyo iliyofanywa. Serikali

imekaa kimya. Fedha za wananchi zimekwenda, tunawaongezea gharama za maisha wananchi. Badala ya *royalty* ya asilimia 3 tunapata 1.9 katika miaka minne tuliyokaa hapa. *(Makofi)*

Tunalipeleka wapi taifa letu, tunawasemea nini wananchi wa kawaida, maskini za Mungu wana tatizo la afya, wana tatizo la elimu. Wana matatizo ya usafiri. Gharama za maisha zinapanda. Rasilimali zinatumika bila ya utaratibu nzuri. Tunataka kabisa kabisa Waziri atupe maelezo ya kina. Katika *investment* ya *65 million dollars* kwa Alex Stuwart Serikali na Watanzania wamefaidika nini? Tunaomba kabisa hili mtueleze. Haiwezekani tukawa kila tuna makampuni makubwa na tena mmewatumia asilimia 90 ya Wafanyakazi wa Tanzania. Na hili ndiyo tatizo la Tanzania tulilo nalo sisi. Baada ya kuwapa uwezo watu wetu na wana uwezo mkubwa tunasema wanakuja watu kunenepesha mashirika.

Hivi wale wa *South Africa* walinenepesha kweli TANESCO. Walilikondesha wakaliacha maskini kabisa. Leo Dr. Rashid anakuja kufufua maiti. Sasa huyu Mtanzania hapewi fursa na juzi tulikuwa na semina nzuri pale Ubungo, tukawalaumu Watanzania wanao-*manage* mashirika haya eti kwamba hawafanyi vizuri. Utafanyaje vizuri wakati hupewi mtaji wa kufanyia kazi? *(Makofi)*

Suala la kwanza ni mtaji, huna mtaji, halafu kuna siasa zinaingizwa kila wakati unafuatiliwa wewe mtendaji *TPFC* hawa hapa hawana hela za kufanyia kazi. Mradi mdogo tu wa kusambaza gesi kutumia Dar es Salaam shilingi bilioni 1.5 hawana. Huwaachi hata *retantion scheme* wakafanya kazi! Lakini tutakuja hapa Bungeni tutawalaumu na mwisho tutamalizikia kama ilivyo leo treni haifiki hapa tena hata Dar es Salaam, *management* ya Kiafrika lakini kwa sababu watu hatukuwapa uwezo wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa tunazowapa wageni wanapo-*manage* mashirika yetu ni tofauti ni fursa tunazowapa Watanzania wanao-*manage* mashirika yetu, wana uwezo mkubwa. Lakini bado hatujawapa fursa sawa sawa. Ninaomba sana kabisa kwa Serikali. Wakati umefika wa kuwaachia Watanzania tumejenga uzoefu miaka hii 46 wako Watanzania wana uwezo mkubwa wa kuendesha mashirika haya. Lakini huwezi kumkabidhi mtu chombo hujampa zana za kufanyia kazi. Hilo naliomba sana tulifanye. Sasa baada ya kumalizia hayo naomba tena nirudie kumwomba Waziri ule utata wa maswali tuliyoyauliza ndani ya hotuba yetu naomba atupe ufafanuzi. Nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru kwa kuniachia dakika mbili tatu, niweze kukamilisha. Tukirudi mchana ataanza Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Marombwa wajiandae hao.

Waheshimiwa Wabunge jana tulipokuwa tunamalizia hotuba ya Miundombinu, ilionekana muda ulikuwa hautoshi, kwa hiyo Spika akatumia Kifungu cha 81 kifungu

kidogo cha 6 kwamba tunaingia kwenye *guilotine* yaani mafungu yote yanasomwa kwa fungu la juu sana.

Sasa Kanuni zetu zinasema hivi, hicho kifungu 81(6) kwamba hali kadhalika wakati Bunge liko katika Kamati ya Matumizi isipokuwa kama itatolewa hoja ya kuongeza muda kwa kikao cha Kamati hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 21 Kanuni ndogo ya nne, ya kanuni hizi. Zikibaki dakika 10 tu kabla ya muda wa kuahirisha Bunge kwa siku hiyo na Kamati bado haijamaliza kufikiria mafungu yoyote yaliyohusika, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yote yaliyoruhusiwa katika Aya (b) na (c) za Kanuni ambapo hapo atahoji kuhusu mafungu yaliyosalia kama yalivyo. Ndivyo ilivyofanyika jana.

Sasa kama mngekuwa makini au mngetaka mngetumia Kifungu cha 21 Na. 4 ambacho kinakuambia Mbunge akisimama naomba kutoa hoja muda uongezwe. Kwa hiyo, akiungwa mkono, Spika anaondoka kwenye Kamati anarudi kukaa hapa ili awahoji kama mnakubali. Mkikubali, Kanuni inasema muda utakaoongezwa ni dakika 30. Sasa unayetoa hoja lazima uwe makini kama ukiangalia hali halisi, kama watakupinga, basi nadhani usiulize. Kama jana ile ungefanya hivyo hivyo, mimi nadhani ungepingwa, kwa sababu ile Wizara ilikuwa *very popular.* Kwa hiyo, ni vizuri kupima wakati unapotumia vifungu vya namna hiyo. Ninawapa hicho kisehemu cha semina ya kila siku kusudi muweze kuwa nayo. *(Makofi)*

Baada ya hapo, nasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuendeleza mjadala wetu kwa kipindi cha asubuhi, sasa tutaendelea na shughuli ya kujadili hoja iliyowekwa mbele yetu leo asubuhi. Orodha niliyokuwa nayo inanionesha msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, ajiandae.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kuiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati yangu kabisa, nikiiangalia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, nikiingalia dhamira njema ya Viongozi wetu Wakuu na ari mpya ya Serikali yetu, napata matumaini makubwa kwamba, tutafika tunapotaka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira njema na ari kubwa kabisa ya uongozi wetu wa kisiasa kama havikwenda sambamba na uwajibikaji wa watendaji wetu, wanaweza wakatupa *Ph.D* ambayo si nzuri. Maana wanasema kuna ile *Philosophy Degree* unapewa, ipo *poor hair distribution* na kuna *pull him down,* wanaweza wakatuvuta nyuma. Katika uongozi kuna falsafa kuu za aina mbili; upande mmoja wanasema jeshi lenye nguvu zaidi ni lile la swala linaloongozwa na kamanda simba, kwa nini wanafikiria lina nguvu? Kwa sababu swala atalazimika kutii kila anachoambiwa kwa kuhofu kuliwa na samba. Mtaalamu mwingine akasema jeshi la namna hiyo halina nguvu ni jeshi la hatari maana litakuwa na nidhamu ya uwoga, jeshi zuri ni lile linaloongozwa na samba, maana wote dhamira yao ni moja. Sasa kwa bahati mbaya sana, nina wasiwasi sana na baadhi ya watendaji wetu, wataniwia radhi sana kwamba wanakwamisha ari, nguvu na kasi mpya tuliyokuja nayo katika Serikali yetu ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitatoa mifano, kilio cha Mbunge wa Same, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela ni ushahidi, Serikali inapeleka pesa ijenge barabara, Watendaji kwa sababu zao tu na raha zao, wakaamua kutokuijenga barabara ile. Hata mimi nilizungumza hapa wakati ninachangia Ofisi ya Waziri Mkuu, matatizo haya yapo, sitaki kurudia lile lile. Lakini mfano hai kabisa naomba niutoe pamoja na kutangaza *interest* zangu, mimi ni Mkurugenzi wa Bodi ya *ARTUMAS. Memorandum of Understanding* kati ya *ARTUMAS* na Serikali yetu ilifikiwa mwaka 2001. Kwa miaka mitatu mfululizo mpaka 2004 hakuna kiongozi yeyote ndani ya Wizara ya Nishati na Madini kuanzia aliyekuwa Katibu Mkuu, ambaye hakuwa tayari kukutana na Kampuni ya *ARTUMAS* kwa miaka mitatu, mpaka ilipofikia 2004, bado majadiliano yalikuwa ni ya kusuasua sana na viongozi wetu wa juu wakiuliza tatizo ni nini, sababu zilikuwa zinatolewa kwamba, *ARTUMAS* haina mtaji, haina utaalamu na imejaa utapeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ARTUMAS* kwa nia moja, pamoja na maneno hayo ya kukatisha tama, wakaendelea na shughuli zao kwa msingi wa maelewano tu na siyo mkataba. Hivi leo Mtwara kuna umeme, *ARTUMAS* wamechoronga visima vinne na kati ya hivi; visima vitatu vina gesi ambayo Serikali imeshapewa taarifa hiyo, yenye ujazo wa *3TCF* na wanaendelea kuchimba kisima kingine. Kuna uwezekano wa kupatikana kwa mafuta na *ARTUMAS* kwa jitihada hizi za kufanya kazi kubwa kama hiyo bila mkataba ni kampuni ya ajabu sana Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *IPTL* tulisaini nao mkataba kabla hawajaanza kazi. *SONGAS* tulisaini nao mkataba kabla hawajaanza kazi, hawa wameshaanza na wamechimba visima vinne bado hawajapewa mkataba, tatizo ni nini? Wataalamu wanapokuja hapa mimi nafikiri wanakuja kusikiliza maoni ya Wabunge ili waweze kuyafanyia kazi na kuwashauri Mawaziri wetu. Kama siyo sababu hiyo, wanakuja kufanya nini hapa, maana kila siku wanasema hayo hayo, mimi wakati mwingine ninawaonea huruma Mawaziri wanapojibu maswali maana maswali yanakuwa ni yale yale na majibu yanakuwa ni hayo hayo kwa sababu wenzetu hawataki kwenda na kasi mpya tuliyonayo viongozi wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapokaa huko kwenye vijiwe kuna maneno ya ajabu sana na mengine tungeyasikia tungelalamika, hawa wanasiasa tu watakuja watapita miaka mitano karibu bwana. Ikiwa ni dhamira ya kila mfanyakazi, ikiwa ni dhamira ya kila mwanasiasa kuwahudumia wananchi wetu, haya mengine yataisha lakini inaelekea kuna watu wengine wanapenda kuweka kwanza maslahi yao mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana tulipokuwa kwenye kikao kimoja kule Bagamoyo, ilibidi Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha wakati ule aniteue mimi na Mheshimiwa Raynald A. Mrope kwenye *government negotiating team,* walau kumshauri yeye. Mtu mmoja alifikia kusema mkataba huo hausainiwi labda *over my dead body,* maneno haya ni ya ajabu sana na hata nilipoenda ofisini kwa Waziri wa Fedha kuzungumza juu ya suala hili la *ARTUMAS,* ameitwa mtaalamu mmoja pale ninamwambia hivi wewe huoni raha kwamba *TANESCO* kwa kupewa umeme miezi mitatu hii wame-*save* dola milioni mbili, ambazo wangenunua mafuta? Akasema si pesa zao wenyewe. Pesa zao wenyewe wakati Hazina kila mwaka ilikuwa inatoa ruzuku kwa *TANESCO* halafu unasema pesa zao wenyewe! Kwa kuacha kununua mafuta tukatumia gesi yetu hatuoni kwamba, tunatengeneza urari mzuri wa vitu tunavyoagiza na tunavyo-*export* sisi; hatuoni kwamba huo ni urari mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka kusema, kampuni hii tusiidharau kiasi hicho. Kampuni kubwa ya Kimarekani inayoitwa *ANADARCO* imeamua kuingia mkataba na *ARTUMAS,* wakashirikiane kufanya utafiti wa mafuta na gesi Msumbiji kuanzia mwezi wa 10 mwaka huu. *Mnazi Bay* ni mpakani mwa Msumbiji tunatenganishwa na mto tu, mafuta siyo jiwe kwamba lilipo lipo hapo hapo, bali mafuta yapo ndani ya mwamba, inawezekana kule wakachoronga wakauwahi mwamba ule ule ambao uko Msimbat, wakawa wa kwanza kupata. Tatizo letu na *ARTUMAS* ni nini au kuna tatizo na watu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara? Kwa sababu kama ulikuwa mkataba umeshasainiwa, leo umeme ungekuwa unawaka Mtwara yenyewe, ungekuwa unawaka Tandahimba, Newala, Masasi, Nachingwea, Rwangwa na Liwale wanataka kufika vilevile na Mchinga ungekuwa una wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 tulitangaziwa hapa kwamba, umeme utafika Mchinga, haujafika kwa sababu hata Lindi haujafika; sasa tatizo ni nini? Tatizo ni Kampuni ya *ATMAS* au tatizo ni la watu wa Mtwara na Lindi? Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake kwamba, umeme huu utaanza kupatikana katika mwaka huu wa fedha 2007/2008. Kauli hii haiko wazi, imefunikwa funikwa na mawingu; 2007/2008 ndio kitu gani? Maana jana Mheshimiwa Andrew J. Chenge, alituambia barabara itakamilika Desemba, ndio tunataka mtuambie umeme utapatikana na mkataba utasainiwa tarehe fulani siyo mwaka 2007/2008; maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafurahishwa sana na Waziri wa Nishati na Madini anatuunga mkono sana katika hili, *TPDC* inatuunga mkono sana katika hili na *TANESCO* yenyewe inatuunga mkono sana katika hili, huyu mwenye tatizo huko Wizara ya Fedha ni nani na ujasiri huo anaupata wapi? Rais na Waziri Mkuu wamekwenda, wote wanataka umeme, wanatangaza jukwaani halafu mtu mmoja tu jamani na bado yupo, yaani unafikia mahali mpaka unataka kuingiwa na unyama kwamba, mimi kama

nakutana naye mtaani peke yetu wawili, basi nitamkandamiza tu, unafikia hatua hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa sababu inaumiza, jambo hili linaumiza sana. Mimi nasema tuna nafasi nzuri, gesi tuliyonayo sasa hivi hii *3TFC* ina uwezo wa kutoa *megawatts* 300. *Megawatts* 300 zikiunganishwa kwenye *Grid* ya Taifa tutakuwa tumepunguza mzigo mkubwa sana kwa *TANESCO*, tutakuwa tumeondosha tatizo la kukatikakatika kwa umeme, lakini tutakuwa vilevile tumeongeza miundombinu ya kuweza kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa ana-*windup* kesho kutwa, atutie matumaini Watanzania, siyo watu wa Lindi na Mtwara tu, bali Watanzania wote kwamba, mkataba huu unachelewa kwa sababu gani na utatiwa saini lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna nyingine tukiwaacha hawa wataalamu kinachoweza kutokea ni kwamba, tunakuwa kama wachungaji wa ng'ombe, anakuwa na fimbo yake ng'ombe hawana mwendo badala ya kuwatandika wale wa mbele wanaochelewesha msafara, anawachapa walio huku nyuma, hawa wa nyuma watapita wapi na wa mbele ndio wavivu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafika huko tukianza kucharaza wanaochelewesha msafara huko mbele, kama ni wafanyakazi wazuri wahamishwe wapelekwe sehemu nyingine maana mtu akikaa mahali pamoja muda mrefu, anafikiria yeye pale ni mfalme. Itafikia mahali Wabunge wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, tutalazimika kwenda kumwona Waziri Mkuu, tumwambie masikitiko yetu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na Ukurasa wa 31, Ibara ya 71 ya Hotuba ya Waziri kwamba, sasa *TPDC* watapewa uwezo, jamani uwezo wa *other charges* hauwezi kuisukuma *TPDC* kufanya majukumu yake. *TPDC* ya sasa si *Songosongo* tu, wala si Mkuranga tu na si *Mnazi Bay* tu, watu wengi wanajitokeza kuja kutafuta mafuta na gesi, kama *TPDC* hatukuiwezesha kwa mpango wa *retention scheme,* wakategemea kwenda kunyoosha mikono Hazina, *TPDC* haitafanya kazi inayotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuwa *shareholders,* lakini ikishapatikana hiyo gesi au hayo mafuta, basi ndio inapigwa hesabu halafu ndio tunapewa ile *share* yetu. Katika utaratibu wa namna hiyo, hatuisadii *TPDC,* tunakosa hata nguvu ya kauli ndani ya vikao. Huwezi kuwa unaingia ubia na mtu, halafu yeye anatoa pesa zake wewe unaenda tu kuleta kelele, mdomo mtupu, lazima tuisaidie *TPDC*. *(Makofi)*

Mwisho, sisi tukisema maneno kama haya ya kuiambia Serikali yetu halafu tukiunga mkono, kuna rafiki zetu wengine wanapata kichefuchefu, umeikosoa halafu unaunga mkono asilimia mia maana yake nini? Mwanadamu amepewa macho ambayo hayana hiari, yataangalia lenye kufurahisha na kuhuzunisha, lenye kupendeza na kukirihisha, lakini Mungu ametupa akili kujua katika haya lipi nilichukue. Kwa hiyo,

wanataka sisi tuwe kama inzi kwa sababu yeye ni mchafu wa jalalani, basi akitua kwenye ugali ameshaacha virusi anayekula anaumwa. Haiwezekani, kitu kizuri lazima ukiseme na ndio binadamu anatakiwa kwenye kasoro atengeneze, kwenye umadhubuti asifu ili mwende mbele, lakini jicho baya linaona mabaya tu, zuri hata moja halionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dada yangu mmoja hapa ananiambia na wananchi wanasema hivyo na Kiswahili chake, kwa sababu ni kigeni kidogo, alifikia kusema kwamba watu wengine tuna viherehere hapa, tunaijibia Serikali na ninyi mmemjibia hapa Kiongozi wa Upinzani. Kila aliyesimama amezungumza hilo hilo, Alex Stewart, *Richmond,* yaani ni wimbo umeimbwa mpaka sasa hivi haunogi, hata ukiimbwa masikio yameshiba, maana wimbo ni huo huo. Sasa naomba katika hili, tuwe tunavumiliana, ninyi zungumzeni ya kwenu na sisi tunazungumza ya kwetu, wananchi ndio waamuzi na kwa ndege hii inavyopaa hivi, mimi nafikiri kihoro tayari kimeingia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia ya kihoro kama kifua chako chepesi kinakuuwa. Kihoro unakuwa na maneno hayana kichwa wala miguu na kihoro kikizidi sana paka wako mwenyewe unaweza kumfikiria chui ukamwogopa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo tu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni nafasi yangu ya kwanza kuchangia, kwa hiyo ninaomba nitoe pole sana kwa wale wote ambao wamefiwa na ndugu zao na hasa Waheshimiwa Wabunge, kuanzia Marehemu Juma Jamaldin Akukweti, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, pamoja na wale waliokuwa Wabunge zamani, Marehemu Stephen Kazi na Marehemu Omar Chubi, pamoja na wengine wote waliofariki na wale ambao wameumia. *Inshallah* Mwenyezi Mungu, atawasaidia watapona haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia katika misimamo miwili tu na la kwanza walichonituma wananachi wangu tangu mwaka 1998, ninazungumzia mpaka sasa na la pili nitazungumzia juu ya mambo ya Kitaifa kama nitapata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu 1998, ninaomba ndugu zangu wa *TANESCO* na Wizara ya Nishati na Madini, watupatie umeme Jimbo la Morogoro Kusini na haswa haswa niweze kusema Wilaya ya Morogoro Vijijini. Nilikuwa ninaenda polepole nikizungumza nao na walinishauri tuwaandikie barua, nimeandika barua *TANESCO* na wao wakanijibu kwamba, kwa utaratibu huu wa kukutafitia umeme, tutakuja kufanya *survey.* Wamekuja wamefanya *survey* wakaniambia kwamba, gharama za kukuletea umeme mpaka Matombo kutoka Morogoro ni shilingi bilioni mbili. Tungoje kidogo Serikali itakapokuwa na uwezo. Huo ulikuwa mwaka 1998. Mwaka 2001 jibu likawa hilo hilo, Serikali itakapokuwa na uwezo. Sasa nimekatishwa tamaa nilipokuja kuona Mradi wa Umeme Vijijini, Serikali imetenga shilingi milioni kumi. Kwa hiyo, umeme kufika Tarafa ya Matombo, Tarafa ya Mvuha, Tarafa ya Kisaki, Bwakila naona inakuwa vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nieleze kwa nini tunahitaji umeme, hatuhitaji umeme sisi kwa sababu tunataka mwanga tu, tunahitaji umeme kwa sababu tunahitaji kujitegemea Wilaya ya Morogoro Vijijini kwa miradi mikubwa ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesaidiwa kiwanda cha kutengeneza mafuta ya jetropa na Waingereza wakaja tukaenda na wananchi *Kisaki Station,* tukatafuta ardhi tukapata na tukahamasisha watu sasa kulima na wao tukakubaliana watatengeneza kiwanda tu watalima kidogo ili wananchi wawe na soko la mazao yao. Muingereza yule alipotoka Uingereza kuja hapa, alifurahi sana lakini akauliza swali moja tu hiki kiwanda kitaendeshwa na nini, nguvu gani na nishati nitakayoitumia? Akasema mimi nasikitika niko tayari kutumia pesa zangu zote lakini kama hakuna umeme siwezi kuwekeza. Viwanda kuendeshwa na *diesel* sasa hivi havipo tena. Tumekaa tumeduwaa, nikawaendea ndugu zangu wa *TANESCO* jamani Mikumi inapakana na Selous katikati ya Kijiji cha *Kisaki Station*, tunaomba umeme utoke Mikumi uje Kisaki. Jibu nililopewa sijui la kiutaalamu, mimi sijui kwamba wanyama wanakimbia umeme unavuma, kwa hiyo, Mheshimiwa hapo haiwezekani. Sasa ukiwa Mbunge ukipata jibu kama hili hata kulieleza kwa wananchi ni kichefuchefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikatoka hapo nikaenda kuwabembeleza wawekezaji waliowekeza Kiwanda cha Sukari pale Kilombero na wao wakaja wakaangalia kutoka Kisaki wakaenda mpaka Mngazi, Dutumi, Mvuha na mpaka Kata ya Selembala wakasema, naam hili ni pori la kulima miwa tuko tayari, tutaweka kiwanda Kisaki lakini umeme utakapofika. Kwa hiyo ni viwanda hewa tu vipo pale. Wako tayari kuwekeza lakini umeme utakapokuwa umeletwa na Serikali. Huu ni kama vile mchezo wa kuigiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna rafiki yangu Canada, akaniambia nimempata mwekezaji wa Kiwanda cha Sukari, una mahali? Nikamwambia mwambie aje, nikampokea Dar es Salaam nikaenda kumwonesha Mtibwa na Kilombero, halafu nikampeleka kwangu ambapo hakuna kiwanda. Waswahili husema mtu kwao. Nikamwambia hapa una nafasi chagua ardhi, akatembelea sehemu yote akasema niko tayari na mimi nitaweka kiwanda Bwakila lakini mbona umeme hakuna! Viwanda hivi vitaendeshwa vipi jenereta itakuwa ghali sana, miwa haitakuwa na thamani kwa wakulima, akaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaja mwekezaji wa Kiwanda cha Pamba, Dutumi pana kiwanda cha kuchambua pamba tangu zamani sasa kimesimama kwa sababu yule mwekezaji ameondoka lakini vilevile mitambo ile ya *diesel* imechoka. Yeye bila kuchunguza nini kipo, ameingia Mkataba na Chama cha Ushirika cha Mkoa, akaja Dutumi na alipofika Dutumi akafurahi sana lakini alipoingia ndani kwenye kiwanda kile, akasema sasa mbona hapa sioni nyaya zozote za umeme! Umeme unapatikana wapi hapa? Nikamwambia hakuna, akasema basi mimi naondoka mpaka umeme utakapofika. Sasa unaweza kuona siyo umeme ambao wananchi wanaotaka kutumia nyumbani ni umeme wa uwekezaji ili Wilaya iweze kuwa inajitegemea kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bado tunaota umeme sijui utakuja lini lakini nawaomba ndugu zangu wa *TANESCO*, ninamwomba Waziri afikirie sana hili. Jimbo la Morogoro Kusini lina mito 13 inayoenda mwaka mzima na hiyo ndiyo mito ambayo

inaingia Mto Ruvu. Watu wa Dar es Salaam wanaotaka kuweka bwawa Kidunda ili wapate maji kwa mtiririko, sisi tuko juu, ninyi mko chini, tutayachafua maji. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi lazima tugawane, vitu hivi lazima tugawane Kitaifa, tunaweka Bwawa la Kidunda, tunahamisha kata nzima ili wenzetu wa Dar es Salaam wapate maji kwa wingi, faida yetu ni nini, kulipwa fidia ya kuhama? Hapana, lazima vingine tutengenezewe kwa manufaa ya wilaya. Nimeuliza swali hapa nikajibiwa vizuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, juu ya Hospitali ya Wilaya na nikaambiwa tafuteni ardhi mpate. Tumetafuta ardhi tumepata na tuko tayari sasa wananchi wa Morogoro Kusini kujitolea kuanza kujenga Hospitali ya Wilaya pale Mvuha na tunatafuta kibali cha kuchangishana lakini Hospitali ya Wilaya utaiendesha kwa vibatari jamani? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamchukua mtaalamu mmoja akasema mimi niko tayari kukupa *theatre* nzima ya ku-*operate* hospitali, hebu nipeleke kwenye kituo chako kimoja cha afya, nione kipi kinafaa. Nikampeleka Dutumi, akafurahi akasema hapa mimi naweza kuwekeza lakini sasa *operation theatre* bila umeme? Akaniambia Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, ukishakuwa tayari na umeme, niambie nitakuja kukuletea. Kwa sababu wananchi wale walifurahi sana kwa ghadhabu.

Mimi mwenyewe nikatumia hii posho yangu, nikafunga umeme kituo kile na nikanunua *jenereta lista* nikawasha umeme mpaka sasa uko pale umeme wa jenereta, unaendeshwa na wananchi. Kwa maajabu kabisa, nimeomba mkurugenzi asaidie tu kuchangia kuwafungia umeme daktari na manesi wake wafanye *wiring* ili nao watumie umeme ule, mpaka kesho inakuwa ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *missionaries* waliokuwa Matombo, waliendesha umeme sehemu moja inaitwa Mayungi kwenye Mto Mfizigo, kuweza kupata umeme unaoendeshwa kwa maji. Mimi nimesoma *Middle School* hiyo na sasa ni *Secondary School,* walipoondoka hao akaja m-*missionary* mmoja, sina haja ya kumtaja. Yeye ameona bora kupata, akauza mitambo ile kwenye *scrape metal*. Kwa hiyo, akauza kile kiwanda kizima cha kutengeneza samani, yeye kakiuza. Nikawaomba *TANESCO* waende pale wakaangalie uwezekano wa kutoa umeme kwenye Tarafa moja tu ya Matombo. Umeme huo ungeenda Matombo, Tawa, Mtombozi, Lundi, ungeenda kwenye kata zote za tarafa ile moja ya Matombo, ambayo ina watu 250,000. Hayo ndiyo majina ya kwetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* wakaitikia wakaenda wakafanya *study,* wamenyamaza kimya mpaka kesho. Kama hiyo haitoshi Rais Jakaya Kikwete wakati wa kampeni alifika *Kisaki Station,* kwa mara ya kwanza huyu ni Rais wa kwanza katika kufika Kisaki kule kwa kampeni. *(Makofi)*

Tunamshukuru sana kwa tendo hili. Wakamwomba kitu kimoja tu. Waliomba *generator* hii kubwa ya *TAZARA* iliyokuwepo *Kisaki Station.* Sisi tupo wengi, ituuzie umeme, sio itugawie bure, ituuzie umeme. Rais mtarajiwa wakati ule alitamka jamani

shirika moja la umma, haliwezi kuzuia shirika lingine la umma kutoa huduma, tutafuatilia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, nafikiri muda umekwisha.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Kwanza, nawapongeza kwa hotuba yao nzuri na fupi na kwa kweli inaeleweka.

Pili, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa taarifa kwenye ukurasa wa sita kuhusu mabadiliko ya uendeshaji wa *TANESCO* kwamba, *TANESCO* sasa inaye Mkurugenzi Mtendaji mpya, Dr. Idrisa Rashid. Mimi ninamfahamu huyu ni mtendaji mzuri na amekuwa Gavana wa Benki yetu, nina hakika sasa *TANESCO* wamepata mtu ambaye ni makini sana. Sina mashaka *TANESCO* sasa itabadilika na mimi namtakia kila la kheri, *TANESCO* ibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tulipita kipindi kigumu sana cha matatizo ya umeme. Serikali ilijitihidi, nawapa hongera kwa kazi hii kubwa wakati ule wa ukame. Kwa kweli kazi ilikuwa kubwa lazima tukubali, Serikali imefanya kazi kubwa na wananchi vilevile walionesha uvumilivu, tunawapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni silaha muhimu sana ya maendeleo. Sasa hivi tunajenga shule kwenye maeneo ya Kata na tunajenga Zahanati. Umeme ni silaha muhimu sana ya maendeleo kwa sababu elimu inahitaji teknolojia na teknolojia inahitaji umeme. Mambo yote haya lazima tuyapeleke kwa pamoja na ni maeneo mengi tu tunahitaji umeme kwa ajili ya huduma za nyumbani, viwandani na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na umeme sio anasa. Kwanza, tunajua kwamba, sasa hivi tuna tatizo la mazingira kwa hiyo, ule utaratibu wa kupeleka umeme vijijini kama hatutauwekea mkazo, tutapata matatizo makubwa kwa sababu wananchi hawatakuwa na mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo ahadi ya Serikali inayosema kwamba, vijiji ambavyo viko kwenye njia kuu ya umeme wa gridi vitapatiwa umeme. Ahadi hii ni ya muda mrefu na kwa kweli ahadi hii katika kipindi fulani ilianza kutekelezwa. Tulikuwa tukija hapa wakati wa bajeti, tunaambiwa vijiji ambavyo vitapatiwa umeme katika kipindi cha mwaka unaofuata. Jambo hili lisimama hasa walipoingia wale wanaoitwa *NetGroup Solution.* Hawa watu wametupa matatizo makubwa sana na nashukuru wameondoka kabisa, acha tubaki na *TANESCO* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu ule katika miaka miwili, mitatu, hakuna vijiji ambavyo vilikuwa vinaandikwa. Vijiji ambavyo nimeviona kwenye kitabu hiki ambacho kimetolewa na Wizara ni vile ambavyo vilikuwa chini ya Miradi Maalum. Kwa mfano, kwa Babati vilikuwa chini ya Mradi unaoitwa *Electricity Four*. Ni vijiji vya zamani tu vimeshapata umeme na ni miradi ambayo ilikuwa inamalizika. Kwa hiyo, hakuna programu ambayo katika miaka hii michache, imekuwepo ya kupeleka umeme vijijini. Tunaomba ratiba kamili na imani ya kweli ya wananchi juu ya hili, inaanza kupungua kama hawaoni kwamba kila mwaka tunayo mikakati ya kupeleka umeme vijijini kwa Programu Maalum. Kwa hiyo, ninachoshauri tuwe na Programu Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hata Miradi ya Umeme mwaka 1996 tulipoomba tuliulizwa Wabunge wa kila Jimbo na ndio maana hata mimi nakumbuka katika Jimbo langu wakati ule, Babati Mashariki, umeme ulikwenda eneo la Magugu, Galapo mpaka Minjingu na maeneo mengine. Sasa programu ya namna hii imepotea, tunaomba kuwe na ratiba ili kweli tuweze kuwa na vijiji ambavyo kila mwaka vinapatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua kwamba umeme ni silaha ya maendeleo, mimi kule kwangu maeneo haya ya Magugaa, Galapo, Babati na maeneo mengine ambayo yalipata umeme vizuri, maendeleo yao ni makubwa sana na vijiji vile vimebadilika na vipato vya wananchi vimebadilika kweli kweli. Nataka nisisitize hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia umeme katika Jimbo langu na usambazaji wa umeme kwenye Mji wa Babati. Sisi Babati tuna bahati kwa sababu tuna kituo kikubwa cha umeme tena wa gridi. Kile kituo cha Babati kina uwezo wa kuzalisha *megawatt* 34.4 na kinagawa umeme kwenda Mbulu, Karatu, Kondoa na Babati yenyewe. Lakini matumizi ya maeneo yote haya niliyoyataja ni *megawatt* 4.95 mpaka mwaka 2006. Matumizi haya ni kidogo sana.

Umeme tunao lakini tatizo ni kwamba, hatuna programu ya kusambaza umeme. Tunataka tuutumie huu umeme. *Megawatt* 34.4 ni umeme wa kutosha na mkubwa sana lakini Kondoa, Babati, Mbulu na maeneo mengine tunatumia tu *megawatt* 4.95. Kwa hiyo, umeme upo pale tatizo ni usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali isambaze umeme huo kwenye mji, vitongoji, mitaa ya Mji wa Babati na vijiji vinavyozunguka mji huo kwa sababu umeme upo tatizo ni kusambaza tu. Sasa kuna faida gani ya kuweka *substation* kubwa pale ambayo ina *megawatt* 34.4, lakini umeme haupo kwenye vijiji vinavyozunguka mji. Pengine hata kwenye hii miji niliyoitaja ya Mbulu, Karatu na mingine, kungekuwa na Programu Maalum. Naomba hiyo programu iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vijiji ambavyo hata kipindi kilichopita nilivisemea vya Managa, Himiti, Bonga na Haraa, vipatiwe umeme na Serikali ikanijibu kwenye swali langu Na.399 kama sikosei la tarehe 14 Agosti, 2006. Nilikuwa najaribu

kuangalia kama kuna programu yoyote kwenye vitabu hivi, sijaona. Nilisema vijiji hivi viko kwenye njia kuu ya Barabara ya Kaskazini *(The Great North Road),* inayotoka Babati kuja Dodoma. Vijiji hivi kilomita kuanzia tano mahali umeme ulipoishia mpaka 15 tu na umeme upo mwingi kabisa pale kwenye *substation* ya Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema vijiji hivi vina shughuli za kiuchumi, kwa sababu ndivyo vinavyolisha Mji wa Babati. Ndio vijiji ambavyo vinalima mbaazi ambazo tunapeleka mpaka India, ukienda kule Bonga, Haraa, kuna kahawa na mazao mengine. Tunalima alizeti, mahindi, maharagwe, ndizi za kutosha zinatoka maeneo ya Himiti, Bonga, Haraa zinalisha Mji wa Babati. Kwa hiyo, vijiji hivi vina shughuli kubwa tu ya kiuchumi na umeme upo kama nilivyosema ni kilomita chache, 15 tu hivi mpaka kijiji cha mwisho. Sasa kama tunashindwa kupeleka umeme kwenye vijiji vilivyo karibu na *substation* ambayo ina umeme wa kutosha sembuse huko kwingine Matombo alikosema Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, ambako zinahitajika karibu shilingi bilioni mbili? Mimi hakuhitajiki fedha hizo kwa sababu umeme uko pale. Hivi ndivyo namna ambavyo tungeweza kuendeleza vijiji vyetu na miji yetu. Kwa hiyo, naomba vijiji hivi vipatiwe umeme safari hii, wala sina ugomvi na mtu yeyote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo haya niliyoyataja, ziko shule za sekondari, sasa hivi ziko shule mbili pale, kuna kituo kikubwa cha afya, kuna taasisi za mashirika ya dini, ziko taasisi nyingi tu kwenye maeneo haya kati ya kilomita hizi 15. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali mjitahidi muweke basi kwenye programu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambako ni muhimu umeme ukaenda ni kwenye vijiji ambavyo viko karibu kwa mfano, Kijiji cha Sigino, Kiongozi ambako kule nako tumefungua Sekondari, kuna zahanati ambayo tunatarajia baadaye itakuwa Kituo cha Afya. Vilevile kwenye mitaa ya Mji wa Babati na Kata ya Nangara tuna kijiji cha Hala, kwenye Mji wa Babati tuna eneo la Maisaka B, iko ndani ya mji kabisa lakini sehemu kubwa ya mtaa huo ni giza. Kwa upande wa Nangara tuna Mtaa wa Maweni, Ari na Balowa. Mtaa wa Balowa uko karibu kabisa na umeme, pengine ni mita chache tu mpaka Maweni pale na labda kilomita moja tu na umeme uko wa kutosha Babati lakini hausambazwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la mwisho, niangalie vitabu. Kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 25 na 26 niangalie kidogo tu, amezungumzia kuhusu suala la kazi zilizopangwa kutekelezwa katika kipindi kinachokuja. Imeandikwa pale kukamilisha uanzishwaji wa wakala wa nishati. Kukamilisha uanzishwaji ndio kazi ya mwaka mzima, tufafika kweli? Halafu pale chini wakala wa nishati vijijini, mchakato wa kupata uongozi wa wakala wa nishati vijijini uko kwenye hatua ya mwisho. Hiyo tu ndio kazi ya mwaka mzima? Miradi ya awali ya wakala inaandaliwa, jamani tutachelewa mno. Wanasema Serikali itaanzisha vyanzo vya mapato endelevu kwa ajili ya nishati vijijini. Ningependa kufahamu mmesema kwamba, shilingi bilioni kumi itakuwa kama mtaji wa kuanzia na kwamba, itakuwa kama ruzuku kwa wawekezaji. Tunataka eneo hili tulifahamu sana. Ningependa eneo hili tulijadili vizuri, tusije tena tukapata wawekezaji ambao hawatatusaidia na umeme hautakwenda

vijijini. Tungeomba Wizara hii itueleze vizuri kuhusu hizi shilingi bilioni kumi za ruzuku kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana muda ukawa umekwisha kabisa, lakini kwenye kitabu ukurasa wa 89, kwenye *subvote* 3001, vifungu vidogo vya *rural electrification,* pamoja na *rural energy agency,* tungependa kujua vile vifungu vitatumika kwenye maeneo gani? Fedha zimewekwa pale za kutosha, kuna shilingi bilioni tisa na kuna nyingine shilingi milioni 850, tungependa kujua programu zake zikoje? Itakuwa vizuri mkitusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimeona kwenye ukurasa wa 90, kifungu kidogo cha 3121 - *ERT Village Electrification*. Kile kifungu mwaka jana kilipangiwa shilingi bilioni 13, kwenye *actual expenditure* hatuioni pale na mwaka huu imewekewa sifuri. Tungependa kujua hizi shilingi bilioni 13 zimetumika wapi na kama bado zipo basi hebu tujue na programu zake. Nia yangu ni kutaka kuona hizi programu za kupeleka umeme vijijini, vinginevyo tusipokuwa na programu, hatutaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, basi niseme naunga mkono hoja na namtakia Waziri kila la kheri, pamoja na Naibu wake. Ningeomba nao wakati fulani, wapite Babati waone kile kituo kina umeme mwingi na wa kutosha, tatizo letu ni usambazaji. Tunaomba hilo tu, wananchi wapo tayari pale hawana matatizo na wananchi wa Babati sio maskini, wataweka umeme, watautumia, usambazwe tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa vile ndio mara yangu ya kwanza kuchangia toka msiba wa Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, napenda kuchukua fursa hii, kuipa pole sana familia yake na kwa ufupi ni kwamba, tunaendelea kuwa pamoja katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza kidogo japokuwa Mheshimiwa bosi wangu wa zamani alisema kwamba, sisi hatupendi kupongeza pale panapostahili kupongezwa lakini ukweli ni kwamba, tunapongeza pale panapostahili kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Kitabu cha Waziri nikaona kuna miradi ya kudumu ambayo itatumia gesi asilia, ambayo itazalisha *megawatt* 100 na *megawatt* 45. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikija katika suala zima la umeme wa dharura, japokuwa bosi wangu wa zamani amesema tusizungumzie *Richmond*, lakini tutaizungumzia tu hadi pale tutakaporidhika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia takwimu za kwenye Kamati na takwimu mbalimbali za Ripoti ya Kamati, zinaonesha kwamba, kuna kampuni tatu ambazo zinatoa umeme wa dharura. Kuna *Agreco, Alston Power* na *Richmonds*/*Dorwans,* naamini hawa ni mapacha kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia gaharama ambazo zimetumika kwenye huu umeme ambao haukuwa na tija, nasema haukuwa na tija kwa sababu nikisoma Ripoti ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa tano anasema kwamba: "Mheshimiwa Spika, uzalishaji umeme nchini, ulirejea katika hali ya kawaida kufuatia mvua nyingi zilizonyesha nchini kuanzia Januari, 2007 na kujaza mabwawa yote ikiwemo la Mtera, linalohifadhi takriban asilimia 80 ya maji ya kuzalisha umeme nchini." Kwa hiyo, taarifa hii ya Waziri inatuonesha fika kwamba, haya mabilioni au mamilioni ya dola tuliyoyatumia ambapo ukiangalia inakaribia dola milioni mia tatu au ni zaidi ya bilioni 300 tulizidondosha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili litakuwa fundisho, kwa sababu ni muhimu tuwe tunajaribu kuona mbele. Tujue kabisa Tanzania labda *next year* kutakuwa na ukame hivyo, tunatakiwa tujiandae mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyopongeza hapo awali, najua kwamba, huu umeme wa kudumu utakuwa ndio suluhisho na naamini kabisa haya matatizo hayatajitokeza tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea hapo hapo, kuhusiana na mapungufu yetu kwa sababu ni lazima tueleweshane ili tuweze kusonga mbele. Kampuni ya *Richmond* ambayo sitataka kuizungumzia ripoti yake, nadhani italetwa hapa tutaijadili, ilipewa mkataba wa *almost* dola milioni 134. Lakini kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ni kwamba, mpaka sasa hivi ni *megawatt* 60 ambazo zimezalishwa na ni muhimu tukumbuke kwamba, *deadline* pamoja na mengine mengi, pamoja na zile *deadline* nyingine ambazo zilikuwa zimerushwa ilikuwa ni February, 2007. Ni miezi mitano imepita na tunajua kwamba, kuna *penalty* ambazo zilikuwa zinatakiwa zitozwe. Sijui kama *penalty* zimetozwa au vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikija suala lingine la uwezo wa kampuni, je, kampuni tunazozipa miradi zina uwezo au hazina? Nilijaribu kufanya utafiti wangu nikagundua kwamba, kampuni ya *Richmond* ilishapewa *tender* nyingine ya kujenga bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Ulikuwa ni mradi mdogo sana na wakapewa miezi 18 wakashindwa kuutekeleza. Sasa unakuwa unajiuliza, inakuwaje hii kampuni ambayo ilipewa mradi mdogo ikashindwa kuutekeleza ndani ya kipindi cha miezi 18, ikaja ikapewa mradi mwingine mkubwa ambapo ikaambiwa ndani ya siku 150 vile vifaa viwe vimekuja? Unapokuwa na mazingira kama haya, ndio unakuta maneno yanasemwa mtaani wanasema hapana inawezekana hii *Richmond* kuna mkono wa kigogo, inakuwaje inakuwa yenyewe? Inawezekana sio kweli lakini unakuta kampuni inapokuwa dhaifu halafu inaendelea kupewa tenda, inazua utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia huu mradi sasa hivi uko mkononi mwa *Tanzania Green Company*, Kampuni ya Chama cha Mapinduzi. Sina neno na hilo ila naamini kwamba, *Tanzania Green* ita-*perform* na tutaona matunda, hatutegemei yaliyotokea *Richmond* yatatokea kwenye *Tanzania Green Company. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kulizungumza hili, sina nia mbaya ila ni katika kujenga. Katika dhana nzima ya mikataba, mimi bado ni Mwanasheria *junior* sana, lakini sidhani kama ina mantiki, Watanzania tunapoingia kwenye mikataba, tuki-*breach* sisi ndio tunakuwa tunapata maumivu. Tunajua ni mikataba mingapi ambayo sasa hivi unakuta tunalipia pesa kutokana na kwamba, kuna makosa kadhaa ambayo tulifanya? Lakini huyo *Richmond* ni *obvious* kwamba, alikiuka mkataba. Sasa sisi tuli-*benefit* nini kutokana na hii Kampuni ya *Richmond* kukiuka mkataba? Hatujui, tunapata maumivu tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba, ndani ya mkataba kuna kipengele cha *transfer.* Sasa kama tunaingia kwenye mkataba ambapo mmoja akikosa anamhamishia mtu mwingine, sidhani kama ina-*make sense* na sijui kama kuna mkataba wa aina hiyo, ambao mtu mwenye akili timamu atauingia. Haya ni maswali ambayo huwa najiuliza halafu sipati majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ule mkataba ambao naamini baada ya *Darwans* kuja, naye amehamishiwa yale majukumu yote aliyokuwa nayo *Richmond* ni kwamba, ilikuwa inatakiwa itozwe dola 10,000 kwa kila siku ambayo wana-*delay* kuzalisha umeme. Taarifa ya Kamati inaonesha wamezalisha 60 mkataba ilikuwa ni 100. Nataka Mheshimiwa Waziri, aniambie kama wameshakusanya kiasi gani na zimekuwa *allocated* wapi? Tujue kuna kitu tusije tukaja kumjulishiwa kwenye zile *figure* nyingine. Kwa hiyo, nataka tu aniambie, amekusanya ngapi na zimekwenda wapi au kama zipo kwenye hii bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala zima hili la nishati ya umeme na ahadi za Mheshimiwa Rais. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na siku moja tulikuwa kwenye Wizara ya Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru na kwa nia njema tu nikajaribu kumdodosa kwa sababu namheshimu sana mzee wetu, mtaalam na ni mtaalam wa propaganda kama vile tunavyoambiwa nje huko. Kwa hiyo, namfagilia sana. Nikajaribu kumhoji, nikamwuliaa Mheshimiwa unajua Mheshimiwa Rais ametoa ahadi nyingi sana, kuna zile za ilani, kuna zile za papo kwa papo, kuna zile nyingine anakuja hapa anazitoa. Akasema ndiyo ahadi zote alizozitoa Rais, lazima zitatekelezeka na zote wanazi-*compile* pamoja ndani ya miaka mitano. Nikasema *okay fine*. Vilevile kuna Mawaziri wetu tumekuwa tukiwauliza wanasema kwamba, wanazi-*compile*. Sasa kwa kuwa tuko kwenye sehemu ya umeme, naomba tu nikumbushie ahadi moja ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa na Mheshimiwa Waziri, nadhani wakati anajinijibu ataweza kuniambia utekelezaji wake unakuaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 29 Agosti, 2005 wakati Mheshimiwa Rais, anagombea alipokuwa Wilaya ya Mbinga Ruvuma, alisema kwamba, Serikali yake ndani ya miaka mitano itahakikisha kila Makao Makuu ya Wilaya ina umeme. Akaendelea kusema ndani ya kipindi hicho hicho cha miaka mitano, nyumba zote nchini zitakuwa na umeme wa uhakika na hata ikiwezekana, kila tendegu ninaamini kwamba tendegu ni zile nyumba za nyasi kama sikosei?

**WABUNGE FULANI:** Siyo hizo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Vyovyote vile, lakini nyumba zote za Tanzania zitakuwa na umeme. Kwa hiyo, *by implication* ni kwamba, asilimia 100 ya nyumba za Tanzania zitakuwa na umeme *by* 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia, jamani mimi nazungumzia ahadi za Mheshimiwa Rais, naamini na ninyi mnazo mnaweza kufanya *reference*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima J. Mdee, ongea na Mwenyekiti.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanani-*disturb*.

**MWENYEKITI:** Wewe ongea na Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi rekodi ambazo ziko pia kwa Mheshimiwa Waziri, zinaonesha kwamba ni asilimia kumi ya Watanzania wanaotumia umeme. Ninashangaa vilevile kwa taarifa ambayo nimeisoma ambapo inaonesha wanategemea *by 2010,* iwe asilimia 25. Kwa hiyo, anaonekana anaji-*contradict* na kile ambacho Mheshimiwa Rais, alikuwa anakisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikiangalia kwenye Mfuko wa Umeme Vijijini umetengewa shilingi milioni kumi tu.

**WABUNGE FULANI:** Shilingi bilioni kumi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *Okay* shilingi bilioni kumi, lakini *still* ni ndogo mno, kama kweli tuna lengo la kuweka umeme katika kila nyumba Tanzania na ukizingatia kwamba, asilimia kubwa ya Tanzania ni vijiji. Nataka Mheshimiwa Waziri, anieleze utekelezaji wa ahadi hizi au kinachofanyika! Ilikuwa ni siasa, yaani mkifika kwenye kampeni mnasema tu, utekelezaji ukija yanapangwa mengine. Kwa hiyo, nilikuwa nataka anieleweshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili vilevile kutokana na hali ya sasa ya umeme ilivyo. Sasa hivi ukitaka kuwekewa umeme unalipa zile *charges* za kawaida, ukimaliza unalipia gharama za nguzo na waya. Sasa tukijiuliza huyo Mtanzania wa kawaida, ambaye tunasema tutampa umeme, sijui kama anaweza ku-*afford* mbali ya kujilipia gharama ya kutaka kuwekewa umeme, kujinunulia tena vile vifaa vyote vya kusogeza umeme. Kwa hiyo, nadhani kuna umuhimu wa kuangalia na kujua tunaweza kuwasaidia vipi wananchi wetu katika hiyo hali ya umaskini wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la madini. Kwenye Ripoti ya *CAG,* ukurasa wa 40, naona muda hautaniruhusu kwa hiyo, sitaweza kusoma, kuna upotevu wa karibu shilingi bilioni 70 kutokana na ratili za almasi ambazo zilikuwa hazijulikani zimeuzwa vipi, yaani ripoti yake haipo. Vilevile tukiangalia ile Ripoti ya Alex Stewart, kuna shilinig trilioni 1.3 zimepotea kwenye madini. Maana yake kuna matatizo na lazima niseme. Wanasema tumesema sana lakini lazima tuendelee kusema hadi tupewe majibu yanayoridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikija katika suala zima hili la mikataba, nakumbuka siku moja niliwahi kuuliza swali linalouhusiana na Kampuni ya *Williamson Diamond,* nikaambiwa kwamba, haijalipa kodi kuanzia mwaka 1980 moja kati ya yale makampuni yake. Lakini nikabahatika kuupata mkataba, msiniulize nimeupataje, lakini katika huo mkataba, kulikuwa na mkataba wa mwaka 1994, ambapo walikubaliana kwamba, baada ya miaka mitano kutoka pale, yule jamaa aanze kulipa kodi hiyo, yaani kuanzia mwaka 1999. Kwa hiyo, mimi mategemeo yangu ilikuwa nitapewa taarifa ya huyo mtu akianza kulipa kodi kuanzia 1999, lakini nikaambiwa hadi 2007 tokea mwaka 1980 hazijalipwa. Kwa hiyo, inaleta utata sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala zima la nishati ya mafuta kama muda utaniruhusu. Nakumbuka wakati Waziri wa Fedha hapa analeta hoja ya kuongeza bei tukasema kwamba, lazima mafuta yatapanda, tukajibiwa kama tulivyojibiwa kwa mbwembwe, lakini ndio hivyo mwezi haujaisha bei za mafuta zimepanda tena zimepanda *by far* na zitaendelea kupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa tunaambiwa kwamba, wataweka bei lakini ndio soko huria. Naamini Mzee wa Falsafa za Marx anaamini kwamba, ndio tumeingia kwenye soko huria, hatuko kwenye ujamaa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* hapa labda *TPDC* iwezeshwe kama watu wengine walivyopendekeza, Serikali yenyewe inunue mafuta ndio hapo itaweza ku-*control, otherwise* ni siasa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nami nachukua fursa hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya Nishati na Madini, wakiongozwa na Katibu Mkuu wao, Ndugu Arthur Gwanaloli Mwakapugi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia ndani sana, Wabunge wengi ambao wamekuwa wakichangia Wizara hii, ukiangalia sana sana wanazungumzia eneo moja kubwa, hasa hili eneo la nishati ya umeme. Eneo hili linazungumziwa sana kwa sababu ndio eneo ambalo linaonekana linahitajika kwa hali ya sasa kwa wananchi wetu hasa katika shughuli za kimaendeleo na hasa katika hali ya dunia ya sasa inavyokwenda, katika mabadiliko ya kiuchumi. Kwa hiyo, hili eneo la umeme ni nyeti sana na hasa ukilinganisha na hali ya dunia na hali ya sasa tulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme si anasa tena bali ni kitu muhimu sana kwa sababu teknolojia kubwa inahitajika kutumia umeme. Kwa hiyo, leo huwezi ukamwambia mwananchi anahitaji mabadiliko bila kuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa hatua za kufanya mabadiliko hasa ya kusitisha mkataba wa Kampuni ya *NetGroup Solution* ya kutoka *South Africa* na hivyo kurudisha shirika letu mikononi mwetu sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kwa kumteua Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hili, Ndugu Idris Rashid, tunamfahamu vizuri toka alipokuwa *NMB* na baadaye akawa Benki Kuu. Kwa hiyo, tunaamini kwa kazi nzuri uliyofanya na *record* yako nzuri, Shirika letu la Umeme litaendelea na litakuwa zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na uhodari wake, Mkurugenzi huyu Mtendaji, inampasa aelewe kwamba, pamoja na hali ilivyo, tumewaondoa *NetGroup Solution* lakini tuna tatizo moja ndani ya Kampuni ambalo lilikuwepo na ambalo bado lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi anapoingia kazini na anapoendelea na kazi, ahakikishe anapambana na ufisadi uliopo ndani ya Shirika la *TANESCO* na hasa hii Nishati ambayo ni haki ya Watanzania kugeuzwa kuwa ni *deal* kubwa kiasi kwamba, mtu ukihitaji umeme hata mahali ambapo kuna kila kitu unapata taabu kwelikweli kuupata huu umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme nimezungumza kwamba ni haki ya kila mtu na hasa kwa Mtanzania, hii ni Nishati ambayo kila Mtanzania anastahili aipate na ni haki yake ya msingi kabisa. Bahati nzuri Shirika letu linajiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia iliyopo ni kwamba, tunapokwenda shirika linahitaji wateja na wateja wanahitaji umeme, bado kuna watendaji wachache ndani ya Shirika wanaonyanyasa wateja na hili si jambo jema kabisa na wanawanyanyasa kweli.

Tunakubali kampuni inaweza ikawa na upungufu wa vifaa na vitu kadha wa kadha, lakini ile tabia ambayo bado wako watu wachache ambao wanaamini bila kufanya ufisadi wa kuhitaji hongo na hawawezi kufanya kitu. Sasa nasema hii ni kazi yako wewe Mkurugenzi Mtendaji, kudhibiti ili kusafisha hili shirika na kurudisha moyo kwa Watanzania ili kujua kwamba hili shirika linafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kitabu hiki cha bajeti ya Wizara na katika kuangalia ule mpango wa kimkakati wa Wizara wa mwaka 2006/2009, moja ya majukumu makubwa ambayo Wizara imejielekeza kwa mwaka ulioishia mwaka huu wa fedha mwaka 2006/2007 ni kupeleka umeme vijijini, kuboresha na kupanua Gridi ya Taifa na kuendeleza miradi ya vyanzo mbadala katika uzalishaji wa umeme. Mimi nibakie hapa katika eneo la kwanza hili linaloambiwa kupeleka umeme vijijini na hili limetajwa ndani ya ilani, yaani ilani ya chama chetu. Kwa sababu katika ilani ya chama chetu na wakati tunagombea, tulikwenda tukaeleza tulisema kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne itatilia mkazo pale umeme unapopita. Ukipita umeme wa gridi au ukipita ule umeme uliopozwa, basi vile vijiji vitapata umeme bila kuwa na sharti lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa sana. Bahati nzuri katika eneo langu na vijiji kadha wa kadha ambavyo vimepitiwa na umeme huo wa Gridi ya Taifa na ule uliopozwa upo na nimejaribu kufuatilia mara kadhaa pale Wilayani kwangu Iramba na hata Mkoani na baadaye nikafika mpaka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo naamini kabisa pengine tunakuwa na vijiji vingine ambavyo hata *transformer* zipo ambazo zinafanyia kazi, kwa mfano, kampuni za kutengeneza barabara na kadhalika, wananchi hawapatiwi ile fursa ya kuingiza umeme majumbani kwa kutumia transforma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kufuatilia kwa mfano, Kijiji cha Maluga na Kitusha. Hiki Kijiji cha Kitusha ili ufike Kijiji kingine kinachoitwa Kyalonsangi ambacho kipo Kinampanda ni eneo lilelile ambalo tunaweza tukasema huu mtaa mwingine na huu mtaa mwingine, lakini hawa watu wameomba umeme waingiziwe ndani na wamejitokeza na walishaweka mtandao ndani ya nyumba zao, watu watapao karibu 30 lakini nimejaribu kwa kila hali lakini hawajawahi kupatiwa huo umeme. Kwa hiyo, tunapozungumza na kuoanisha na mkakati wetu wa mwaka 2006/2007 kwamba, lazima vijiji vile vilivyopitishiwa umeme uliopoozwa, viingiziwe umeme. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara na namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hili suala lilishafika mpaka kwake mara kadhaa, atakapofanya majumuisho, aniambie kwamba ili watu wale wa pale Kitusha na wale wa Maluga; ni lini sasa mtapeleka umeme kwa sababu na wao wanahitaji? Si kwamba umeme haupo, upo kwa hiyo, naomba sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kadhalika niendelee niseme kwamba, kuna kijiji kingine cha Kibigiri, hiki Kijiji cha Kibigiri kina *transformer* na hii *transformer* inafanya kazi ya kusukuma maji kupeleka Kijiji cha Nselembwe kwa umbali wa kilomita tano. Hii *transformer* haina kazi nyingine, *transformer* inaweza ikafanya kazi nyingine ya kuweza kuingizia watu umeme. Lakini tatizo linalokuja hapa, watu wanaambiwa kwamba, waingize umeme kwa gharama zao, ikiwa ni pamoja na kununua nguzo, nyaya na mambo kadha wa kadha, ambayo yanahusu utendaji na ufundi kwa *TANESCO* yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, wako watu ambao wanajitolea wanaweza kuingiza umeme kwa kiasi hicho, lakini mbona Shirika halizingatii kuweza kuwaacha hawa watu kuingia mkataba na wakapeleka umeme bure wakamwacha atumie umeme mpaka ile hela yake itakapokwisha. Kwa hiyo, ina maana unaponunua nguzo, nguzo siyo mali yako ni mali ya *TANESCO*, nyaya pia ni mali za *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninachoweza kukizungumza hapa, naomba sana wale watu ambao wana uwezo wa kuweza kuingiza umeme ndani majumbani na wametumia gharama zao kama zile za nguzo, nyaya na kadhalika, gharama zao basi zifidiwe kupitia na ule umeme ambao utaingizwa mle ndani na wautumie umeme bure mpaka hela yao iishe ile waliyonunulia vifaa ambavyo ni mali ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vijiji vingine ambavyo vyote hivi naviombea umeme navyo ni Kijiji cha Simbalungwala, ambavyo vyote vimepitiwa na umeme huu uliopozwa, Mkulu, Zinziligi na Shule ya Sekondari iliyopo Kibaya, Songambele na Kata ya Ndago. Nimeomba sana na mwaka jana niliomba hilo. Kwa hiyo, naomba kwamba watakapokuwa wanafanya majumuisho hili waniambie kwamba ni

lini sasa wataweka *priority* na ili watu wa kule na wao waweze kufaidi nishati hii muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nizungumzie Kituo cha Afya cha Shelui, hiki Kituo cha Afya cha Shelui kipo eneo la Kijiji cha Mgongo na tulijaribu kwa kiwango fulani, tukawa tumeomba umeme na wakatuambia watatuletea umeme mwaka jana, lakini hadi sasa bado hatujaletewa umeme. Tukaambiwa hatua ya mwisho kwamba, tuchangie shilingi 56 milioni, wananchi wa kule hawana uwezo wa kuchangia hizo pesa na tunaomba mtakapokuwa mnajumuisha hili, mtoe kipaumbele na kuweza kutupatia umeme katika Kituo hicho cha Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Sekta ya Madini, kwa uchache kidogo. Ndani ya Jimbo langu ninao ule Ukanda wa Mlima Sekenke na kwa bahati nzuri Mlima Sekenke kama ulivyo Mlima Sekenke, tuna dhahabu katika eneo hilo. Eneo hili lina wachimbaji wadogo wadogo, ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa muda mrefu lakini nilikuwa naomba sasa pamoja na wale wachimbaji wamekuwa wakiomba vibali na wamekuwa wakiomba pengine wapatiwe leseni kuweza kumiliki maeneo hayo. Naamini kwamba, wanaweza wakaja wawekezaji na watakapofika wawekezaji wale watu wanaweza kuondolewa na wakaonekana hawakuwa na maana yoyote. Lakini wamekuwa pale kwa muda mrefu na wamekuwa wakifanya shughuli zao kwa hiyo, naomba Wizara itakapofikia, kwa sababu maombi yao yako Wizarani, naomba sana wananchi hawa wapewe hizo leseni ili waweze kumiliki hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nizungumzie eneo la Kipuma na Misuna nayo ni vivyo hivyo. Hapo tuna Madini yanayoitwa *Zilcons* na wananchi wanafanya shughuli za uchimbaji na wanaendelea kwa muda mrefu. Vivyo hivyo wamekuwa wakihangaika mara kadhaa wakiwa wanahitaji kumilikishwa lile eneo ili wafanye shughuli zao kiuhalali nao waonekane kama ni wananchi ambao wanamiliki hayo maeneo. Kwa hiyo na hili pia ningeiomba sana kwamba, Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake atoe kipaumbele katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa naangalia hili Shirika la *TPDC* katika ukurasa wa 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Sasa namwita Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi ajiandae na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti atafuatia.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nitoe taarifa kwa Shirika la *TANESCO* hapa nimepewa taarifa na Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah,

Mbunge wa Mafia kwamba, Meneja wa *TANESCO* Mafia, anaitwa Abdul-rahman Salehe, amefariki leo saa tisa mchana Dar es Salaam, *ina lillahi waina ilaihi rajiuna.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri kwanza, kwa kuikubali na kuinga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Kwa upande wangu mimi nataka kuchangia eneo moja tu kubwa, ambalo linahusiana na hotuba yake ukurasa wa saba inahusiana na gesi asilia ya Songosongo, ambayo katika ukurasa ule unaeleza vizuri tu kwamba, gesi ile ina lengo la kuhakikisha kuwa maeneo ya Wilaya ya Kilwa, Rufiji na Mkuranga ndiyo watakaofaidika sana na gesi ya Songosongo kwa kupatiwa umeme, hii ilikuwa mwaka jana lakini mpaka sasa hivi umeme huo haujawaka katika maeneo hayo.

Sasa mimi nichangie katika eneo la kwanza kabisa, kuhusiana na mkandarasi anayejenga kile Kituo cha Umeme pale Somanga Bungu. Mkandarasi yule amecheleweshа kituo kile kwa muda wa miezi kumi sasa. Mwaka jana katika bajeti, Waziri wa Nishati wakati ule Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha, alitupeleka pale Wabunge wa Mkoa wa Pwani, pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Lindi, kwenda kuona maendeleo ya ujenzi wa kile kituo. Lakini tulivyokwenda pale hali ilikuwa ni mbaya, ujenzi ulikuwa unasuasua na inavyoonekana, wakandarasi wengi sana ambao wanafanya kazi katika Mikoa ya Kusini, hawana uangalizi wa kutosha kwa wale wanaowapatia kazi.

Kama mradi umechelewa kwa muda wa miezi kumi mpaka sasa tunatarajia nini? Wananchi tumewaambia muda mrefu kwamba, umeme utapatikana baada ya miezi michache lakini mpaka sasa kinachoendelea hakijulikani. Sasa ninaomba tu Viongozi wa *TANESCO* na Viongozi wa Wizara hii ya Nishati na Madini, hebu waangalieni Wakandarasi wenu wanaofanya kazi Mikoa ya Kusini hawawajibiki ipasavyo.

Tumieni nguvu zenu na Sheria za Mikataba ili kuhakikisha kuwa, watu hawa wanafanya kazi inayotakiwa siyo wanafanya kazi wanavyotaka wao wenyewe, ni lazima wafanye kazi kulingana na mikataba ilivyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie kuhusiana na walioathirika na kupitiwa na nguzo za umeme. Nilipokuwa nachangia Hotuba ya Waziri Mkuu, nililizungumza hilo kwamba, kuna wananchi wa Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Rufiji, ambao wameathirika na kupitiwa na nguzo hizi za umeme. Wananchi hao wamekatiwa mazao yao na walikatiwa mazao kwa Mkataba wa kwamba, watalipwa fidia mara tu baada ya kazi ile ya kuhakiki mali zao zilizokatwa itakapokamilika. Mimi nilifuatilia kwa karibu na ninamshukuru sana Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, yeye kila mara nilikuwa naye, alikuwa ananipatia mwelekeo mzuri wa namna gani *TANESCO* inavyotaka kuwalipa hawa wananchi fidia za mali zao ambazo wamekatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilichokuwepo ni kitendawili, mpaka sasa wananchi wengi hawajalipwa fedha zao kutokana na mazao waliyokatiwa na hawa watu wa *TANESCO*. Nilipokuwa Dar es Salaam mwezi Mei, 2007 nilikwenda Makao Makuu ya *TANESCO* nikawaona watu wa *SONGAS,* wakanipatia maelekezo mazuri tu kwamba,

kilichokuwa kinachelewesha ni vile vitabu kusainiwa na Wakuu wa Wilaya, pamoja na Wakuu wa Mikoa. Vitabu hivyo vimesainiwa na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pia, lakini pamoja na kusainiwa huko malipo yao bado hayajatekelezwa. Nikamfuata tena Mheshimiwa Naibu Waziri kumweleza hilo na yeye nashukuru leo alinipatia jibu moja zuri kutoka *SONGAS* na ninaomba ninukuu hilo jibu. Alisema kuwa: "Malipo ya fidia yatafanywa na Serikali kupitia Mradi wa Songosongo ulio chini ya Wizara ya Nishati na Madini hivyo, suala la ulipaji wa fidia linategemea bajeti ya Wizara."

Haya majibu ameyapata Mheshimiwa Naibu Waziri, kutoka kule kwenye Mradi wa Songosongo, lakini pale chini akaendelea kusema tena: "Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Uongozi wa Wizara uliwaandikia Hazina ili kutenga pesa kwa ajili ya fidia hiyo, lakini hadi sasa halijapatikana jibu. Hazina haijatoa jibu ni namna gani hawa watu watalipwa hiyo fidia. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2007/2008, Mradi wa Songosongo waliomba shilingi 4.7 bilioni hata hivyo ni shilingi milioni 500 tu ambazo wamekubaliwa. Fedha hizi hazitatosha kwa shughuli zote zilizopangwa kuendeleza mradi ikiwemo ulipaji wa fidia tajwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikorosho ya wananchi ambayo ilikatwa ndiyo iliyokuwa inawapatia fedha hawa watu, wengine wamekatiwa mikorosho mpaka 40, wengine 50 na mkorosho mmoja unaweza ukatoa gunia moja, mikorosho 50 kwa mwaka inaweza ikatoa karibu magunia 50. Baada ya kukatiwa Serikali haijatoa fedha kwa ajili ya kuwalipa wale watu, unataka wale watu wanaendelea kuwa maskini mpaka lini? Kwa nini tunawaonea hawa watu?

Kama Serikali ilikuwa haina fedha za kuwalipa hawa watu waliokuwa na mikorosho hii, wangeliamua kabisa kuachilia mbali wasubiri muda mwingine mara Serikali itakapopata fedha ndipo waweze kuwakatia watu mikorosho na minazi yao na nyumba zao za kuishi, kwa sababu siyo mikorosho na minazi tu, bali na nyumba za kuishi nazo pia zimeathiriwa.

Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, sisi wanasiasa kule Rufiji tumezungumza sana suala hili. Mimi na Mkuu wangu wa Wilaya ya Rufiji, tumekwenda kuwaomba wananchi wale ili hizi nguzo za umeme ziweze kupita, tumekwenda kuwaomba radhi kwa kushirikiana na *DC*. Tuliahidi kwamba, baada ya muda mfupi tu fedha hizi zitapatikana, sasa hivi mimi na Mkuu wa Wilaya, tunaonekana waongo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, pale Kibiti ndiyo Makao Makuu ya Jimbo langu, nikipita mimi ninazomewa kwa sababu niliwashawishi wananchi kukata miti na kwamba wangelipwa fidia. Ninazomewa kwa sababu sionekani kama ninatekeleza wajibu wangu kama niliwaomba waweze kukatiwa; kwa nini wasiweze kupewa fidia zao?

Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, utakapokuwa unafanya majumuisho basi mojawapo ya hatua ya kujumuisha hotuba yako iwe kwenda kuwaona wananchi wa Wilaya ya Rufiji, kuanzia Bungu mpaka unafika Kilwa, uwaambie wale wananchi kwamba, Serikali kwa sasa haina fedha mpaka hapo fedha zitakapopatikana ndipo

mtaweza kupata hizi fedha. Sisi tumesema hilo wanatuona waongo. Tunakuomba wewe mwishoni kabisa utusemee hilo, bila hivyo sisi Wabunge hatuna kitu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuzuii shilingi lakini tunachokuomba ni hicho, yaani ulizungumzie hilo na pia uende kule uzungumze na wananchi, kueleza ahadi ya Serikali ni lini wananchi hawa watapata fidia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusiana na kitabu chako Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kwamba, umeme utawaka. Sasa katika maeneo haya mwaka jana tuliahidiwa utawaka, nashukuru nguzo zimekwishawekwa na nyaya zimeshaanza kutandikwa, basi atuambie tu ni lini maeneo ya Kibiti, Bungu, Ikwiriri pale ingawa jenereta lipo, maeneo ya Utete mpaka maeneo ya Muhoro mpaka Kilwa; ni lini umeme huu utawaka katika bajeti ya mwaka huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na ombi. Wakati alipokuwa kwenye ziara Wilayani Rufiji, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyekuwepo sasa, aliombwa na wananchi wa Wilaya ya Rufiji kwamba, katika Wilaya ya Rufiji ili kutekeleza MKUKUTA, kuna eneo lile la *Delta*, ambalo asilimia karibuni 90 ya wananchi wake ni wavuvi, kuna kiwanda kimoja cha kutengeneza barafu pamoja na kuhifadhia samaki. Kile kiwanda ni kikubwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliniomba mimi nilijibu swali hili ni namna gani tutafikisha ujumbe huo kwa Waziri mhusika na mimi niliupeleka kidogo kwa Waziri, lakini nitaupeleka vizuri zaidi.

Ninachokiomba, kiwanda kile kikipelekewa umeme, kitatoa ajira kubwa sana kwa wananchi wa maeneo ya *Delta,* watakuwa na uwezo wa kuvua samaki wao, watakuwa na uwezo wa kutengeneza barafu, kwani sasa hivi barafu za kuhifadhia samaki zinatoka Dar es Salaam. Lakini wakitengenezewa pale Nyamisati, uwezekano mkubwa sana wa kuweza kupata barafu na kuweza kuvua samaki kwa wingi utakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba wewe na Mheshimiwa Waziri, ombi letu hili la kwanza ulifikirie. Siyo mbali sana, umeme unaweza kuuchukua kutoka Bungu mpaka Nyamisati au unaweza kwenda *Mchukwi Mission* ukachukua umeme mpaka Nyamisati, *Mchukwi Mission* ni karibu zaidi. Tunaomba sana hilo nalo Mheshimiwa Waziri, alifikirie kwenye Wizara yake, nitalipeleka vizuri zaidi kwa maandishi.

La pili, ni kupeleka umeme Gereza la Mng'aru. Katika Mkoa wa Pwani, gereza kubwa kabisa ni Gereza la Mng'aru, ni kubwa na ni Gereza la Kilimo, lina eneo la zaidi ya hekta 30,000, kwa kweli ni eneo kubwa. Wafungwa wapo wengi pale hivyo basi, tukiwapelekea umeme, uzalishaji nao utakuwa mkubwa katika lile gereza ni kilomita saba tu kutoka Kibiti mpaka kufika kwenye lile gereza, siyo mbali.

La tatu, ninaomba Wizara ya Maji ishirikiane na Wizara hii ya Nishati na Madini. Kuna miradi mingi ya maji mwaka huu kwa mfano, pale Kibiti tuna miradi hiyo, tuna miradi maeneo ya Ikwiriri, kuna visima vimechimbwa. Sasa mpango wa awali ulikuwa ni kuweka majenereza, matumizi ya jenereta ni makubwa sana. Kuna vijiji ambavyo vimewekewa jenereta katika Jimbo langu, kimojawapo ni Kijiji cha Kimbuga, lakini

kutokana na *running coast* za ile jenereta, imefikia ndoo moja shilingi 50. Sasa kwa mkazi wa kawaida na mwananchi wa kawaida, kutoa shilingi 50 kwa ndoo ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, ingawa Kanuni zinanikataza kutoa ruhusa yoyote ya kuongeza muda ndani ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti atafutia na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, ajiandae.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi ili walau na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba hii ya Nishati na Madini, kama ilivyowasilishwa leo asubuhi na Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nichukue nafasi hii, nimshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, pamoja na Wataalamu wao, kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo inasomeka na inaeleweka. Kimsingi haina matatizo, napenda niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo mawili au matatu makubwa. Jambo la kwanza ninaomba nizungumzie yale ambayo kwa sehemu fulani nilipata nafasi ya kuuliza katika swali langu la asubuhi. Naomba nizungumzie viporo vya miradi ya umeme katika Wilaya ya Mbozi.

Tulikuwa na miradi mitatu mikubwa ya viporo; Mradi wa kwanza ni kutoka Rwanda kwenda Iyula mpaka Idiwili; Mradi wa pili ni kutoka Vwawa kwenda Hasamba; na Mradi wa tatu ni wa kutoka Kijiji cha Mahenje kwenda Kijiji cha Igunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hili kwa kweli kwa masikitiko sana kwamba, nguzo za kupeleka umeme katika maeneo haya zilianza kuwekwa tangu mwaka 2002/2003. Mbunge aliyepita mzee wangum Mheshimiwa Edson Halinga, alizungumzia sana juu ya suala hili na aliahidiwa sana, lakini kila mwaka ulipofika hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako, ninaomba uniruhusu nirejee swali moja ambalo aliwahi kuliuliza humu Bungeni mwaka 2003, liko kwenye *Hansard*, lilikuwa ni swali namba 127 na liliulizwa tarehe 27 Juni, 2003. Kwa ruhusa yako swali lilikuwa linasomeka hivi: "Kwa nini umeme haufiki Iyula, pamoja na kwamba nguzo zilishawekwa?" Hilo ndiyo lilikuwa swali.

Majibu ya Serikali yalikuwa kama ifuatavyo: "Mheshimiwa Spika, kazi ya kusimamisha nguzo katika Kijiji cha Iyula imeshaanza na inaendele vizuri ili kukipatia umeme Kijiji cha Iyula."

Kwa kifupi hayo ndiyo yalikuwa majibu ya Serikali mwaka 2003, lakini mpaka leo nguzo toka zilivyowekwa wakati ule, hakuna kilichoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekwenda kwenye mikutano kijiji kile tangu nimechaguliwa zaidi ya mara tatu. Kila nikienda swali la kwanza pale ni umeme wetu mnatuletea lini kwa sababu walishaahidiwa. Asubuhi nilizungumza na inawezakana nilizungumza kwa jazba, lakini ndiyo ukweli. Wengine wanataka kuzungumza humu Bungeni kwa kulia, pengine huko kulikuwa ndiyo kulia kwangu.

Kijiji kile kwa kweli siyo kijiji niseme ni mji kwa sababu ni *centre* ambayo ina watu karibu 5,000. Kuna Shule ya Sekondari hapo, Shule ya Msingi, Kituo cha Afya, Mahakama na huduma nyinginezo nyingi kwa sababu ni *centre.*

Tulipoteza kijiji hicho kwa vyama vingine vya upinzani kwa sababu ya kero kubwa ya umeme, kila ukienda umeme hakuna, kila ukienda umeme hakuna.

Sasa tukizungumza haya humu Bungeni ni kwa sababu ya uchungu. Nilipotoka huko miezi miwili iliyopita walisema, tunaomba tupelekee salaam Serikalini kwamba bado tunasubiri umeme. Mwaka jana mimi niliuliza swali humu Bungeni na aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati huo, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha alijibu alisema, tutakamilisha viporo vya umeme vyote vilivyobaki katika Wilaya ya Mbozi katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Kwa masikitiko makubwa nasema hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, unaweza ukaona kuanzia Mheshimiwa Mzee wangu Edson Halinga amesema hilo hilo, mwaka jana nimesema lakini hakuna kilichofanyika, sasa tuseme nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa humu ndani, tunajua sasa *TANESCO* ni ya kwetu, tumepata Mkurugenzi mahiri, wenzangu wamesema na mimi nafahamu mtu aliyekuwa *level* hiyo na kumpa *TANESCO* bila shaka vilio hivi vya Wabunge atavisikiliza na kuvifanyia kazi. Tunazungumza humu Bungeni kwa niaba ya wananchi wetu. Tunaomba Serikali itusikilize na itoe matamko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme jibu la asubuhi kwenye swali langu la nyongeza, ninaposema basi nielezeni umeme huu utafika lini, Naibu Waziri, mdogo wangu na rafiki yangu sana Mheshimiwa William Ngeleja alisema siwezi kutoa ahadi ni lini. Majibu kama hayo yanakatisha tamaa. Kama tulikuwa na mradi toka mwaka 2003, leo Serikali haiwezi kusema tutawapatia umeme lini. Majibu haya yanakatisha tamaa. Kwa kweli mimi namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atueleze ni lini sasa baada ya miaka mitano hiyo umeme sasa Iyula mpaka Idiwili, umeme Mahenge - Igunda na Vwawa-Hasamba utafika lini. Naiomba sana Serikali itusaidie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze jambo la pili. Nilizungumza pia asubuhi kwenye swali langu. Sisi tunapata umeme kutoka Zambia na umeme ule tunautumia katika Mji wa Tunduma ambao ni mji wa mpakani, mahali nyeti na mahali ambapo kwa kweli ni *sensitive* sana kwa sababu ni mpaka wa nchi na pako *active* wakati wote unaweza kusema saa 24. Umeme huu unatumika Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi pale Vwawa lakini pia katika Mji wa kibiashara ambao unainukia sana pale Mloo. Lakini umeme huu tumekuwa na matatizo nao makubwa sana. Umeme huu hukatikatika mara kwa mara bila taarifa wakati mwingi nami nimelazimika kuufuata uongozi wa *TANESCO* Wilayani nikazungumza na Meneja wa pale, anaitwa mama Mashimba akasema wakati mwingine hata yeye anashindwa kutoa taarifa kwa sababu umeme huu unatoa Zambia, hana mawasiliano kwamba wanakata lini na saa ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii inasikitisha, mimi nimetembea, nimekwenda *Mbozi Mission* kuna hospitali kubwa zamani ndiyo ilikuwa *District Designated Hospital* lakini sasa hivi tuna hospitali ya Wilaya pale Vwawa. Wilaya hii ni kubwa, inategemewa na watu wengi. Lakini pia hata hospitali yetu ya Serikali pale Vwawa, tuna viwanda vya kahawa pale Mloo viwili. Sasa ukizungumza kukatikatika kwa umeme ni hatari sana kwa sehemu kama za hospitali. Madaktari wanaweza kuwa *theatre,* umeme unakatika ghafla na jenereta zetu tunazijua ndiyo hivyo, nyingi haziko *reliable,* siyo za kuzitumaini sana. Umeme ukikatika itachukua dakika ishirini mpaka nusu saa ndiyo jenereta iwashwe. Sasa kama madaktari walikuwa *theatre* kuna uhai tena wa watu humu ndani jamani! Hakuna uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hii ni miji ya kibiashara, watu wanafanya biashara zao. Sasa ukishakatakata umeme, kwanza, kuna hatari ya kuharibu vyombo vyao vinavyotumika kwa ajili ya kutunzia baadhi ya mali hasa mafriji, *deep freezers* na kadhalika. Lakini sisi tunasema umeme wa gridi upo Mbeya, kwa nini sisi Mbozi tusiunganishwe kwenye umeme wa gridi? Umeme wa kwetu ume-*stabilize*, sisi bado tumebaki tuko kwenye *rank* ile ile, tuko kwenye enzi zile zile za kugawiwa umeme na wakati mwingine umeme huu tunaupata kama nilivyosema bila uhakika wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali na Waziri atakapokuwa anajibu atueleze kwa nini umeme ambao tunaununua Zambia unatusumbua kiasi hicho. Tunaomba atueleze na hizi ni adha ambazo tunazipata sana wakati tunapokwenda kwenye mikutano. Hivi karibuni yalifanywa majaribio tulikuwa *connected* kwenye Gridi ya Taifa kwa maana ya pale Wilaya ya Mbozi sehemu ambayo haijapata umeme na tulikuwa hatuna matatizo yoyote, umeme ulikuwa mzuri, lakini kwa sababu ambazo hatukuzielewa tukarudishwa tena kwenye umeme wa kawaida ambao tunaununua Zambia. Kwa hiyo, tunaomba tuelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la umeme wa jua *(solar)*. Tumeambiwa kwamba katika kupeleka umeme kijijini tutumie pia na umeme wa aina nyingine mojawapo ni umeme wa *solar,* lakini nikawa najiuliza hivi huu umeme wa *solar* ni wananchi wetu wangapi wa kawaida huko vijijini ambao wanamudu kwa bei zilizopo sasa hivi.

Naomba kwa ruhusa yako mimi nimetembelea mabanda yale pale, nikaambiwa bei za *solar* kama unataka kuweka nyumbani kwako nikajiuliza hivi kama mkulima wa kawaida ambaye kipato chake kwa mwaka hakizidi shilingi 500,000/= anaweza gharama hizi za umeme wa *solar?* Wanasema hivi, *solar power system* kwa ajili ya taa nne tu, pamoja na kusikiliza redio ni shilingi 1,050,000/=, lakini *solar power system* kwa ajili ya kuwasha taa sita mpaka nane, *TV* pamoja na redio ni milioni mbili karibu na laki tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya tatu, *solar power system* kwa ajili ya kufunga taa kumi na tano, *TV set,* feni pamoja na redio karibu shilingi milioni tano. Lakini pia hata kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ambacho mimi nimepata kabrasha lile ambalo linaonyesha takwimu, hata ukiangalia pia ukurasa wa 23 kwa wale ambao wamepata makabrasha haya bado inaonyesha wanasema *capital cost* kwa ajili ya *solar* ni kati ya dola 4,000 mpaka 10,000 ambazo hazipingani sana na karatasi ambazo tumepewa kule nje. Ni Watanzania wangapi ambao tunategemea waweke umeme vijijini kwa bei hizi zilizopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba Serikali, tunaposema umeme mbadala tuangalie na maisha ya Watanzania kule vijijini wanaweza hizi gharama, tuangalie kipato cha Mtanzania ndipo tusisitize kwamba mnaweza sasa mkanunua pengine hii *solar*. Vinginevyo tutakuwa tunajizungumzia sisi wenyewe humu ndani. Mimi kama Mbunge nina uwezo wa kununua, Serikali inanilipa vizuri naishukuru, naweza nikaweka hata kama siyo vizuri lakini naweza kuweka *solar* hii kwa kujibana. Lakini baba yangu, mjomba wangu na shangazi zangu ambao wapo vijijini wanalima wanaweza? Na hawa ndiyo tunaowawakilisha hapa Bungeni, hawa ndiyo tuwasemee, hawawezi. Naomba Serikali iliangalie sana suala hili. *(Makofi)*

suala lingine ambalo nataka kuzungumza kwa ufupi sana na wenzangu wamelizungumzia, naiomba Serikali kupitia Wizara hii isisitize kupitia mamlaka hii ya *EWURA,* bei za mafuta sasa hivi tunaumia. Hapa Dodoma lita moja ya petroli ni kati ya shilingi 1,530/= mpaka shilingi 1,600/= hapa Dodoma na sisi sijui kama Serikali itarekebisha gharama hizi, sijui kama Serikali itatulipa gharama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niseme naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu. Kwanza, nami niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Amina Chifupa. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wengine wote wa Wizara hii ya Nishati na Madini kwa hotuba nzuri ambayo kwa kweli wameitoa kwa kifupi, ni nzuri, imepangiliwa vizuri, wanastahili pongezi, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema pia nikawapa pole Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kati ya Wizara ngumu ni pamoja na hiyo. Inafahamika, tumekuwa tukivutana hapa lakini baada ya wao kuingia pale nimewaona Waheshimiwa kwa leo katika michango yao kidogo inakwenda na ule ubinadamu, nadhani mnakwenda vizuri, naomba mwendelee na hatua hiyo ili angalau mtufikishe huko tulikotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu itahusu maeneo matatu, mafuta, madini na umeme. Tuanzie kwenye mafuta, suala la mafuta tumekubaliana hapa vizuri kabisa tuongeze kiasi kidogo ili tuweze kujenga barabara, hilo halina ubishi, isipokuwa ndugu zetu wafanyabiashara inafika mahali sasa wanataka labda wapate utajiri wa haraka haraka kwa kuwanyuka wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina imani Serikali italiona hilo ili angalau basi wapate kidogo na watu waweze kusafiri, bado tatizo ni kubwa kweli. Nazungumzia mafuta kwa sababu sisi wananchi wa Mwanza, Shinyanga, Tabora tuna matatizo sasa hivi kutokana na suala zima la treni kutofika Dar es Salaam. Tatizo hilo linatufanya sasa hivi simenti kwa Mwanza tununue zaidi ya shilingi 17,000/=, 18,000/= mpaka 20,000/=. Kwa maana hiyo kama treni itaendelea kuwa na tatizo la namna hii, tatizo litarudi zaidi ya hapa. Nilitaka niulizie hapa suala moja. Kumekuwa na tetesi ya bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza sijasikia Mheshimiwa Waziri akilielezea. Huo ndio ukombozi wa watu wa Mwanza na Shinyanga, liko wapi hilo bomba? Kwenye majumuisho ningependa nione Waziri analifafanua vizuri zaidi ili tuweze kuona mambo yanavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba niingie kwenye madini. Nilipata fursa ya kupitia kitabu hiki, kimewagusia wachimbaji wadogo wadogo vizuri sana. Naomba ninukuu sehemu kidogo tu, wamesema: "Uchimbaji mdogo wa madini ni kwa ajili ya Watanzania tu na hufanyika takribani katika Mikoa yote nchini kwa lengo la kutaka kuinua kipato chao. Madini yanayochimbwa na wananchi wadogo ni pamoja na dhahabu, almasi, vito, jasi, chumvi, miamba ya chokaa, madini ya ujenzi na uzalishaji wa kokoto." Namba mbili: "Umuhimu wa kuendeleza uchimbaji mdogo hapa nchini unazingatia sababu zifuatazo:-

(a) Ni chanzo kimojawapo kikubwa cha kipato na ajira kwa wananchi waishio vijijini na hivyo huchangia katika mapambano dhidi ya umaskini na katika kupunguza kasi ya vijana kuhamia mijini". Hiyo ni *point* ya muhimu kweli.

(b) "Fedha wanazopata wachimbaji wadogo kwa kuuza madini yao zinaingia moja kwa moja katika mzunguko ndani ya nchi ikilinganishwa na fedha za mauzo za migodi mikubwa ambapo sehemu kubwa ya mapato yao hutumika nje ya nchi.

(c) Wachimbaji wadogo wanaweza kuwa walipaji wakuu wa kodi kupitia kodi zilizowekwa ndani ya bidhaa yaani *indirect taxes* kwa mfano katika vinywaji na vyombo vya usafiri.

(d) Wachimbaji wadogo ndiyo wagunduzi wakubwa wa madini."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nizungumzie hasa hili la mwisho la wachimbaji wadogo ndiyo wagunduzi wa madini. Kwenye eneo langu kipo kijiji cha Buhunda, wananchi wa kawaida walifanikisha kugundua madini ya dhahabu, wakaanza kupata madini pale, wakaanza kwenda kuuza. Ghafla wakabatiza na jina la pale ikawa kwa jina la Kisukuma *ishokelahela* kwa maana ni kurudia pesa pale, ukichota tu ule mchanga unakwenda kule unapembua, unapata pesa, unarudia tena. Wakavamiwa na *East Africa Mining* tangu mwaka 1994. Wakaambiwa sasa mwondoke eneo lile likawa la kwao wale na hawachangii chochote. Sasa hawa wachimbaji wadogo wadogo wamegundua wao, wamepata wao, wananyang'anywa tena ule mradi maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili lifanyiwe kazi kwa kina kweli, hawachangii chochote kile. Lakini kwa bahati nzuri wamekuja wengine wanaitwa *Sub-Sahara* wao wapo kwenye eneo la Lubili, wao wanaendelea, juzi juzi katika ujenzi wa sekondari tukawaomba wachangie katika ujenzi wa shule ya sekondari ya Lubili. Kwa kweli hawakuwa na matatizo wakatuma watu wao, wakaja kuangalia vile vyumba vitatu, kwa gharama zao wamepaua, wameleta mbao na fundi wao, wamekamilisha, tunaomba tuwapongeze sana wananchi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni watu ambao wapo kwenye utafiti kwenye eneo ambalo sisi wananchi hatujaona chochote na wametuchangia zaidi ya shilingi 5,000,000/=, lakini huyu ambaye ametuondoa kwenye eneo ambalo tunapata hajachangia hata shilingi moja, tunaonewa, liangaliwe, hilo ni tatizo ambalo kwa kweli linatunyima raha kwamba wachimbaji wadogo wadogo sasa wanakuwa kwenye kipindi kigumu sana ukilinganisha na maneno mazuri niliyoyasoma hapa ambayo yapo kwenye kitabu cha bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye umeme. Mheshimiwa James Musalika, wakati anachangia alizungumzia mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga. Mradi ule kati ya miradi ambayo kwa kweli imeniweka pabaya ni pamoja na huo. Mara ulipofika tu ule mradi walikuja kufanya upembuzi, wakaamua kwamba umeme watachukulia kwenye kijiji cha Inonelwa kupita Buhingo, Seke, Nyamainza, Mbarama, Isesa mpaka Nyanghomango kule Ihelele. Wakaniomba mimi niende nao angalau kwenda kuzungumza na wananchi wakubali wasimike nguzo zao bila kuwa na fidia yoyote. Wananchi waliona kwamba hii ni neema, walikubali kwa maana ya kwamba wangepata umeme. Yule Mkandarasi aliyepewa ile kazi ya kusimika nguzo na kupeleka umeme kule Ihelele akaja na nguzo amesimika kwenye maeneo yote niliyoyataja mpaka amefikisha Ihelele, ameleta nyaya za kufikisha umeme mpaka huko ziko na nyingine ziko nyumbani kwangu na vifaa vingine vyote, vikombe nini viko pale na nina *transformer* moja pale nyumbani kwangu. Lakini cha ajabu baadaye waligeuza wakaenda upande wa pili. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ooh.

**MHE. JOCOB D. SHIBILITI:** Sasa huku yule Mkandarasi anataka ang'oe nguzo zake kwa kuvuruga mazao ya wananchi kwa mara nyingine ya pili na wao wanasema kwamba hilo haliwezekani. Kwa hiyo, kuna dalili ya mapambano hapa. Namwomba kabisa Mheshimiwa Waziri atimize ahadi yake kwa maana ya kwamba wananchi hao wapate umeme. Nguzo zipo, nyaya zipo, vifaa vyote vipo, wekeni mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru ndugu yetu Idrisa Rashid ambaye amekuwa Mkurugenzi wetu Mkuu kwenye suala hili, hatumfundishi kazi lakini kwa sababu yeye ni mahiri, kesi ndogo ndogo kama hizi yeye ndio ataanzia kuzimalizia kuagiza ili suala hili liishe, wananchi wapate neema yao. Ni tatizo kubwa kweli. *Transformer* iko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaeleze haya kwa sababu hali ni mbaya kweli. Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani analifahamu hili. Barua ya wale jamaa anayo, kwa hiyo, hilo napenda lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahamia Kisesa, Mwanza kuelekea Sumve. Naipongeza sana Serikali, imejitahidi wananchi wa Sumve hasa kwenye hospitali yetu ya Sumve tayari umeme unawaka pale. Lakini huo umeme umetoka pale Kisesa ukaja Bujingwa ukaenda Kanyelele, Koromije, Bogomba na baadaye mpaka Sumve. Mheshimiwa George Lubeleje, kwa sababu yeye alikuwa ni mtumishi wetu upande wa afya anapafahamu vizuri pale. Pale Koromije kuna sekondari na sasa hivi kuna kituo cha afya, acha wewe Lubeleje wakati unafanya kazi kulikuwa na zahanati sasa hivi ni kituo cha afya. Sasa kwa nini wasipate umeme katika eneo hilo. Kanyerere pale kuna sekondari ambayo tayari ipo, kwa nini wasipate umeme pale? Naiomba sana Serikali ione umuhimu wa kuwapa umeme kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Mabuki wapo wachimbaji wa almasi. Kuna mzee wetu mmoja mstaafu Mzee Rwakatare alikuwa Katibu Mkuu naye anapembuapembua pale. Nimemfikia pale Dar es Salaam na kumweleza kwamba tuna tatizo la kununua eneo kwa ajili ya kupanua shule ya Mabuki. Kwa heshima yule mzee hakuwa na matatizo, akasema nilikuwa mgonjwa lakini Mheshimiwa Shibiliti huwezi kukosa chochote, akanipa shilingi 100,000 nitaifikisha. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mzee Rwakatare kwa kujali kuchangia shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kulikuwa na upozaji wa ule umeme wa Gridi ya Taifa pale Mabuki. Mheshimiwa William Ngeleja umetaja hapa wakati ukijibu swali sikumbuki ni la nani. Ulipoitaja tu Mabuki ukawa umenigusa, utueleze, utakapopoza pale umeme ina maana kwamba Nh'ungumalwa itapata umeme na *ginnery* zote za ukanda huo. Sasa ni lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwe mstaarabu kwamba nisipigiwe kengele ya pili niunge mkono kwa asilimia mia moja na ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja hii jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, basi na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Marehemu Amina Chifupa, ambaye alitutoka tukiwa hapa Bungeni. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kwa kumpongeza mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Ameiwasilisha vizuri ilikuwa ni fupi na ni hotuba ambayo imeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu chake hiki ambacho ametupatia siku hii ya leo ukurasa wa 17, mojawapo ya taarifa aliyotupatia ni kwamba katika hatua za kutaka kuboresha sera na sheria ya madini, pamoja na mafaniko mengi yaliyopatikana lakini mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa umeendelea kuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato la Taifa linatakiwa lichangiwe ni pamoja na maliasili zetu za Taifa. Madini ni moja ya eneo ambalo kwa kweli lina sababu ya kuchangia kwa ukubwa sana. Kwa sasa hivi tunayo madini ya kutosha na madini Tanzania yanaendelea kupatikana maeneo mbalimbali na Mkoa wa Kagera umetajwa na hata mimi katika Jimbo langu wapo pia wajasiriamali wameshaona maeneo yenye madini na wenzangu wengine wamesema hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kushauri ni kuomba kwamba kama pale ukurasa wa 18 mtoa hoja ameeleza kwamba mchakato wa kudurusu Sheria ya Madini ya mwaka 1998 uendelee. Nashauri uendelee kwa bidii ili uweze kuendana na mabadiliko yanayotokea na mambo ya msingi ya kuzingatia kwa mujibu wa mtoa hoja, ni mfumo mzima wa utoaji wa leseni za madini na usimamizi wa leseni zenyewe. Haya yakizingatiwa katika hiyo sheria ambayo itakuwa imeshakamilika, naamini kwamba mchango wa madini katika Pato la Taifa unaweza kuwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo napenda nilizungumze na pia naishukuru Serikali, liko pale ukurasa wa 29. Katika ukurasa wa 29 kipengele cha 64, kuna umeme wa nguvu ya maji ambao unatafutwa. Umeme huu umekwishaonekana katika maeneo mbalimbali lakini kwa mujibu wa kipengele hiki ni pamoja na Mto Rusumo. Mto Rusumo ni mto uliopo katika Mkoa wa Kagera. Una maji mengi ya kutosha mimi, sijawahi kuona umekauka na maji yake yanakwenda kwa kasi sana. Kwa hali hiyo nimeipongeza Serikali kwa ubunifu huu ambapo imetajwa mito mingi ambayo itakwenda kupunguza mapungufu ya kuhitaji pengine umeme wa ziada au umeme wa kukodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyovyote vile umeme tunaoupata nje ya umeme wetu wa maji, kwa kweli ni umeme unaoliingizia Taifa letu hasara. Naendelea kuishauri Serikali kwamba niliposoma kipengele hiki kinachofuata kinasema muda halisi wa utekelezaji wa miradi inayoainishwa hapo juu utabainishwa kwenye mpango kamambe wa umeme wa miaka 25. Miaka 25 inaonekana kama mingi kwa sababu kwa hali

tuliyonayo mimi nadhani Tanzania ni nchi ambayo ina maporomoko mengi yanayoweza kutumika kwa njia mbalimbali na tukaweza kupata umeme. Lakini tuna mvua nyingi ambapo zikitumiwa vizuri tunaweza kupata umeme wa nguvu ya maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maporomoko ambayo tuseme wataalamu au wajasiriamali ambao Watanzania wamefanya ambayo nimeyashuhudia mimi mwenyewe ni pamoja na Mto Ndolage, unaitwa Mto Bugonzi katika Wilaya ya Muleba. Wafanyakazi pale Ndolage wakati huo alikuwepo mzungu anaitwa Penning House, alitengeneza maporomoko ambayo mpaka sasa kwa sehemu kubwa ndiyo yanaendesha hospitali ya Ndolage. Sasa kama yale maporomoko yangeendelezwa, siku moja niliwahi kusikia swali likijibiwa hapa kwamba ni pamoja na vyanzo vidogo vilivyopo katika Wilaya ya Muleba.

Nashauri kwamba maporomoko haya yangeendelezwa hakika yangesaidia na yangepunguza mahitaji mengi katika baadhi ya vijiji ambavyo viko karibu na eneo la Mto Bugonzi na tukaweza kupata umeme katika vyanzo vyetu sisi wenyewe. Naishauri Serikali hilo jambo iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo kuna vijiji vingi tu ambavyo vimezunguka shule, maeneo ambayo yanapitiwa na Gridi ya Taifa ambapo vijiji hivi vingeweza na vyenyewe kupatiwa umeme. Katika Wilaya ya Muleba na katika Jimbo langu la Muleba Kaskazini ni miongoni mwa Wilaya ambazo zinapitiwa na umeme wa gridi unaotoka Uganda, *of course* unaingia katika Gridi ya Taifa, lakini umeme huo umeruka vijiji vingi. Katika tathmini ya matumizi ya umeme Kitaifa Mkoa wa Kagera ni mmojawapo ambao unatumia umeme kidogo sana asilimia mbili tu za umeme wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha kwamba Mkoa wa Kagera tulipopata umeme wa Uganda pengine tuliridhika, lakini kama ungekuwa unafuatilia madai yetu mengi ambayo tumekuwa tunayafikisha kwako katika meza yako Tukufu na katika kiti hicho ulichokalia, tumekuwa tukiomba kuweza kupatiwa umeme katika vijiji mbalimbali na katika shule mbalimbali katika maeneo yetu ambayo bado hatujatekelezewa. Kwa kuangalia haraka haraka bila mahesabu mimi nilikuwa nadhani sisi tuna hali nzuri pengine maeneo mengi yamekwishapata umeme, lakini kitakwimu unaona kabisa kwamba Mkoa wetu wa Kagera kwa kweli bado tuko chini kabisa katika matumizi mazuri ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe katika maeneo ambayo nimewahi kuwasilisha na ambayo bado nazidi kuyaombea umeme yanakopitiwa na nyaya za umeme, ninaposema hivyo, wananchi wa Muleba wanafahamu, wataalamu wao siwezi kurudia wanaelewa vizuri ninachozungumza, ni pamoja na eneo la Ruhanga, Bushagara, Kafyunzo, Bushumba na Izigo Sekondari ambayo iko karibu sana na tulikwishaomba na hata tukaahidiwa kwamba ingeweza kutekelezwa lakini bado mpaka sasa haijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nishukuru kwa huu mradi unaokuja huu wa umeme wa vijijini na mfuko wa umeme wa vijijini pamoja na kwamba ni kweli umetengewa pesa kidogo, shilingi 10,000,000,000 si pesa nyingi, lakini mimi naishauri

Serikali kwamba kwa sababu imelitamka, inalifahamu, imeliona kwamba huu ni mwanzo na mimi nasema hongera kwa sababu pasipokuwa na mwanzo huwezi kusema utakuwa na nyongeza. Naishauri Serikali ijitahidi sana kutafuta watu watakaotusaidia. Wapenzi wetu wanaotuunga mkono katika masuala ya maendeleo, naomba watusaidie kuinua mfuko wa umeme vijijini kusudi umeme uweze kufika katika maeneo mbalimbali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita niliwahi kumsumbua sana aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini na maswali yangu mengi yalikuwa yanajibiwa na aliyekuwa Naibu Waziri wakati huo Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha aliniahidi kwamba umeme wa Kagoma ulikuwa unashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano ilikwisha, tumeanza miaka mitano mingine. Ninachopenda kuiomba Wizara inayohusika na Serikali kwa ujumla ni kuangalia hayo ambayo yalikuwa maombi ya siku nyingi yaangaliwe sasa ili tuweze kupata umeme wa Kagoma. Kwa sababu wananchi pale wamekwisha kujiandaa, kuna wananchi sasa hivi zaidi ya 60 na pale kuna shule ya sekondari ambayo sasa hivi iko mpaka kidato cha nne, tunahitaji umeme katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naishauri Serikali iangalie kupeleka umeme katika maeneo ya taasisi kwa sababu sasa hivi ushindani wetu upo katika elimu na katika huduma za afya unaendelea kuwa ni wa kitaalamu zaidi kwa kushindana na Mataifa mengine. Ni vizuri elimu yetu katika shule zetu za sekondari zote ikawa ni ile ambayo inalenga watoto waweze kupata mafunzo si pekee tu katika maabara, lakini sasa pia waweze kupata mafunzo ya kompyuta wakiwa bado wapo shuleni. Hatuwezi kupata mafunzo ya kompyuta kama hatuna umeme shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile hatuwezi kutoa huduma nzuri katika zahanati tunazotaka kujenga kila kijiji na vituo vya afya kwenye Kata bila kuwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nilikuwa naiomba Serikali iliangalie sana. Shule zangu zote zilizopo katika Jimbo la Muleba Kaskazini ambazo sasa hivi zinafikia takriban 11, nilikuwa naziomba ziweze kupata umeme na vituo vyetu vya afya pamoja na zahanati ziweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachokishauri sana ni kuona hii habari ya matumizi ya umeme wa *solar*. Hiyo gharama iangaliwe, Serikali iangalie inasaidia wapi ikiwa ni pamoja na umeme wa vijijini, Serikali itafute mahali pa kusaidia ili gharama hizi mwananchi wa kawaida aweze kuzimudu na aweze kufaidika na umeme huo tunaokusudia kuwa nao kwa lengo la kusaidia umeme kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda nilizungumzie nimeguswa sana na kufurahi pale kwenye ukurasa wa 25 ambapo panazungumzia habari ya *TPDC* kwamba sasa itaanza tena kujiingiza katika biashara ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mafuta katika Mkoa wa Kagera inatisha. Hivi tunavyozungumza kama Dodoma mafuta yamefika shilingi 1,600, sijui tarehe ya

leo, Kagera mafuta yatakuwa yamefikia shilingi ngapi. Kwa sababu nilipoondoka huko juzi siku ya Jumatatu, lita moja ilikuwa shilingi 1,700 Bukoba Mjini. Sasa unapoendelea kutoka Bukoba Mjini maana yake bei inapanda zaidi. Hii imetuathiri sana.

Sasa hivi nauli ya mwananchi anayetoka Bukoba Mjini kuelekea Kamachumu ambapo ni kama kilomita 41 tayari imeishafikia shilingi 2,500 hadi shilingi 3,000 hii ni nauli kubwa sana. Lakini kila mahali ambapo kulikuwa na nauli kati ya shilingi 500 imepanda kati ya shilingi 500 na shilingi 1,000. Hiyo ndiyo hali halisi katika Mkoa wa Kagera. Lakini ukiuliza chanzo wanakwambia chanzo kikubwa ni mafuta yamepanda bei. Sasa pamoja na ongezeko kubwa hilo la hao wafanyabiashara wa huduma ya usafiri, lakini unaona ukweli kwamba Mkoa Kagera bei ya mafuta inakuwa ni kubwa sana ikilinganishwa na Mikoa mengine. Watafute uwezekano wa bei ya mafuta kuwa isipishane sana katika Tanzania nzima kusudi waweze kutoa huduma inayolingana kwa masuala ya usafiri na kwa masuala ya huduma zingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kusema kwamba mabadiliko ya Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* ni tumaini kwa Watanzania. Naomba atumie sifa hizo tunazompa, matumaini yetu atujengee kwa kuturejeshea huduma nzuri kwa Watanzania hasa zinazohusu matumizi ya umeme kwa Watanzania na kufikishia umeme katika maeneo mbalimbali kwa gharama nafuu ambayo Watanzania wanaweza wakaimudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi narudia kukushukuru na hata bila ya kufanya *summary,* yale ambayo nimeyazungumza ninaamini kabisa kwamba wame-*take note,* mchango wa sekta ya madini, umeme unatokana na nguvu ya maji uende katika huduma za jamii na vile vile turudishe tumaini kwa kuona kwamba tunapata huduma nzuri za umeme kwa Watanzania wote kwa sababu sasa hivi tunaye Mkurungenzi mzalendo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kuchangia katika hoja hii muhimu. Ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote katika Wizara hii na taasisi zote kwa hotuba nzuri sana na kazi ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nishati na Madini inaweza kuchukuliwa kama vile tunasema Hazina ni moyo katika mwili wa binadamu, nishati na madini inaweza kuchukuliwa kama mapafu katika mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati na madini ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba huduma nyingine za nchi pamoja na shughuli zingine za maendeleo zinapata maendeleo yanayostahili kutokana na mambo hayo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuchukua fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa jitihada kubwa iliyofanya kwa ujasiri mkubwa sana. Tulikuwa na matatizo sana katika sekta ya nishati kama tunavyojua, lakini jitihada zimefanywa za mpango wa muda mfupi na mpango wa muda mrefu zimesaidia sana

kuleta matumaini makubwa sana kwamba hali hii itazidi kuwa nzuri. Tunashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi maalumu kwa jinsi ambavyo Serikali imechukua hatua thabiti kukosoa makosa yaliyopo kuondoa wenzetu wale wa Afrika ya Kusini ambao walikuwa wanaliongoza Shirika hilo na kuweka uongozi wa kizalendo ambapo tayari tumeishaona kwamba imeweka misingi imara ya maendeleo. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali na kumpongeza Dr. Rashid, kwa shughuli zake ambazo zinaelekea mwelekeo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali imechukua hatua thabiti za kuimarisha na kuijenga upya Shirika la Mafuta Tanzania. Hatua ambazo zimechukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa zinatoa matumaini makubwa ya kuweza kupata maendeleo katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Shirika letu la *STAMICO* lilikuwa kama limekufa, Serikali imeanza kuchukua jitihada ya kuliendeleza na ni muhimu jitihada ziendelezwe. Nasema hayo ambayo yamefanyika na hayo ambayo yameelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri yakiendelea kufanyika yataendelea kuleta matumaini na maendeleo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TANESCO* tunashukuru kwamba jitihada zimefanywa za kutoa mipango mizuri na zimeombwa fedha nyingi kwa Serikali ili liweze kuisaidiwa kwenda kuendeleza shughuli zake za kujikwamua na kuendelea kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati yetu tuliliona hilo na tumelieleza na tumeishauri Serikali kama Serikali yenyewe haitakuwa na uwezo wa kuisaidia *TANESCO* basi angalau Serikali itoe idhini au dhamana waweze kupata fedha za kufanya shughuli hizo muhimu ili kwamba hayo mengine yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Shirika la Mafuta tunashukuru kwamba jitihada nyingi sana zimefanywa kuhusu utafiti wa mafuta na gesi na ni jitihada nyingi zimefanywa na Mikataba mingi imeshawekwa saini na maendeleo mazuri yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kabisa katika haya ni kwamba gesi asilia ambayo imepatikana siyo tu imeanza kutumika vizuri katika viwanda na katika shughuli nyingine za uzalishaji bali sasa hivi jitihada zinafanywa vile vile na kama Waheshimiwa Wabunge wengine walivyoona kwenye maonyesho hapo nje kwamba matumizi hayo yaende mpaka majumbani na matumizi yake yaende mpaka katika magari. Sasa huu ni ugunduzi mzuri sana bila shaka utatusaidia kupunguza gharama kubwa ambazo sasa hivi tunapata. Kama ambavyo Serikali imeeleza na kama ambavyo pia Gavana alisisitiza jana katika maelezo yake kwamba mfumuko wa bei ambao unatupata katika nchi hii kwa sehemu kubwa sana unatokana na kupanda kwa gharama ya mafuta. Sasa jitihada hizi za kupata gesi yetu na kuitumia bila shaka itatusaidia kwanza kupunguza gharama

zetu za uagizaji mafuta kutoka nje. Halafu pili, itatuwezesha sisi kutumia gharama ndogo zaidi za uzalishaji na kupunguza mfumuko wa bei katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili ningependa kutahadharisha kwamba wakati tulipokuwa tunatembea katika machimbo mbalimbali tulipata kuuliza kwa nini gesi hiyo ambayo inatoka hapa inakuwa na bei kubwa namna hiyo ukiangalia kwa hali halisi ilivyo. Jibu tulilolipata ni kwamba gesi hii ya kwetu asilia wanaiweka katika bei za Kimataifa. Bei ya Kimataifa zilivyo na wao wanaiweka kwenye hilo na kwamba suala hilo limependekezwa Serikalini kupitia *EWURA* na *EWURA* inakubali bei hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kushauri kwamba *EWURA* iwe macho sana katika masuala haya ili kwamba faida ambayo inaweza kupatikana kutokana na kuonekana kwa gesi hiyo na matumizi ya gesi hiyo isije ikatuondolea ile faida ambayo tunaitazamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba Shirika la Mafuta linafanya jitihada kubwa kusambaza utaratibu huu katika sehemu mbalimbali za nchi kuanzia Dar es Salaam. Michoro ya awali na mipango ya awali imeshatengenezwa, gharama zake ni kubwa sana. Kamati yetu imesisitiza na mimi ninaongeza kusisitiza kwamba huu ni mradi mzuri sana na mwema sana, tunaiomba Serikali ifikirie kulisaidia Shirika la Mafuta ili liweze kutengeneza mradi huo kwa haraka iwezekanavyo ili Dar es Salaam na kwingineko nchini waweze kufaidika kadri vile ambavyo wamepanga. Sasa hilo ni jambo zuri naomba tuendelee nalo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *STAMICO*. *STAMICO* ni tegemeo kubwa sana la wananchi wetu. Wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa na migogoro mikubwa na wachimbaji wakubwa, lakini kuna haja kubwa sana ya kuwasaidia wachimbaji wetu wa dhahabu na *STAMICO* ndiyo tegemeo la wachimbaji dhahabu wadogo wadogo kuweza kupata mafunzo, maelekezo na kuweza kupata utaalamu na kupata mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelitambua hilo imeanza kufanya hivyo, lakini bado inaonekana kasi ya kuimarisha *STAMICO* haijawa katika ngazi ile inayotakiwa. Kwa hiyo, naomba suala hilo Serikali ilitilie mkazo na *STAMICO* wapewe uwezo zaidi ili kuweza kutekeleza kazi zake hizo kwa faida kubwa ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la madini kwa jumla, tunashukuru kwamba Serikali imo katika harakati ya kupitia sheria na kufanya mabadiliko na kwa kuzingatia kwamba sheria ya ardhi imetoa thamani kwa ardhi. Tunapendekeza na ni vizuri kusisitiza kwamba pengine ni vizuri wananchi badala ya kuondolewa pale walipokuwa kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walivyosema hapa kwamba wananchi hao mara nyingi ndiyo wamekuwa wafumbuzi wa madini hayo katika sehemu mbalimbali, lakini hatimaye huondolewa hao wananchi bila kulipwa fidia yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunataka ile ardhi pale walipo wananchi iwe inachukuliwa na thamani ile iongezwe katika hisa wanakuwa wao ni washiriki kwa hao. Hilo linaweza kufanyika moja kwa moja ama na wananchi wenyewe katika jamii yao waliopo ama kwa kupitia *STAMICO* kama muongozaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limetambua na wananchi wametambua kwamba pamoja na jitihada za ubinafsishaji na nia ya kuendeleza sera hiyo, lakini tumeona kwamba pale panapoingia mkono wa umma mara nyingi panakuwa na uchungu na mara nyingi ulinzi wa masuala hayo unakuwa ni mzuri. Sasa kwa *STAMICO* na kwa *Petroleum Development Corporation* ni vizuri kuhakikisha kwamba hizo hisa katika madini na katika uchimbaji wa mafuta, katika uchimbaji wa gesi wanapewa zile hisa toka mwanzo ili hatimaye tusije tukakosa hayo mambo. Tumejifunza kutoka *ATC,* tumejifunza kutoka sehemu mbalimbali, kwa hiyo, naomba hayo mambo kwa upande huo tuendelee kwa mwelekeo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo ya jumla, ningependa kuzungumza kidogo yale ambayo nimetumwa na wananchi wangu wa Wilaya ya Mkinga. Wilaya ya Mkinga ni Wilaya mpya na baadhi yetu wengi hatuifahamu, lakini ni Wilaya ambayo kimaendeleo kidogo iko nyuma, lakini ina nafasi nzuri sana ya maendeleo. Wilaya hii ni Wilaya ambayo inaanzia katika bahari ya Hindi ina mwambao wa karibu kilomita 60 kutoka bahari ya Hindi na inaendelea katika Milima ya Usambara inapakana na Lushoto, Korogwe, Muheza na Tanga kwa Kusini na Pemba huko Baharini. Wilaya hii ina rasilimali nyingi sana, rasilimali za bahari, rasilimali za ardhi, ina ardhi nzuri yenye rutuba nyingi na safi sana. Ina mabonde mengi, milima mingi na vitu vingi sana ambavyo ni vizuri sana kwa maendeleo ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wilaya ya Mkinga ina nafasi hiyo nzuri ya kuendelea, lakini moja ya miundombinu muhimu ya maendeleo ukiacha ya barabara na nini, ukosefu wa umeme. Ukosefu wa umeme unakwamisha uwekezaji, unakwamisha na utalii. Nafasi nzuri ya Wilaya ya Mkinga imeongezwa zaidi kwa hivi karibuni ambapo Serikali imeamua kupandisha daraja Pori la Umba kuwa Hifadhi ya Taifa ya Umba na kwa hiyo, kuongeza nafasi ya utalii pale, ukiongeza na utalii wa Pwani watu wanatoka Mombasa, Zanzibar, Pemba na kuja mpaka kwetu kule. Sasa hiyo imeongeza tena mahitaji ya umeme kuwa makubwa zaidi. Ukiacha hivyo, taasisi, shule, zahanati, kutokana na jitihada kubwa zilizofanywa na wananchi kwa kushirikiana na Serikali chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne wamejenga shule nyingi sana na wamejenga zahanati nyingi sana na tutaendelea kufanya hivyo na kujenga vituo vya afya na vyote hivyo vinahitaji umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya maombi yetu ya muda mrefu ya umeme hayajapata mafanikio bado. Maombi hayo yameanza siku nyingi sana. Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, alipokuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati ule na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Tanga alikuja akatoa ahadi kwa wananchi kwamba jitihada hizo zingefanywa. Bahati mbaya hilo halikuweza kufanyika. Katika Awamu iliyofuata nilipata fursa ya kwenda na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini katika vijiji kadhaa kule na ahadi zilitolewa kwamba

kijiji cha Daruni, kijiji cha Gombero, kijiji cha Kwale, kijiji cha Mkinga, kijiji cha Manza, vingepata umeme. Lakini bahati mbaya hilo halijaweza kutekelezeka, limetekelezeka kwa kiasi fulani kidogo, lakini bado halijafanyika kwa kiasi kile ambacho kilitarajiwa. Kijiji cha Manza kwa bahati mzuri walikuwa na umeme karibu ukaunganishwa kwenye *transformer* pale wakawa wamepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Mkinga zililetwa nguzo na nyaya zaidi ya miaka miwili sasa zimekaa, lakini bahati mbaya umeme haujateremshwa kuingia majumbani mwa watu; na tunaambiwa sijui kuna matatizo ya *transformer* na nini na hivi, na hivi tumepata ahadi hiyo mwaka wa tatu sasa, ninaamini kwamba mwaka huu katika utaratibu huu wa *Rural Electrification* hilo litafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi hayo yameongezeka vile vile kwamba hapo Kasera ambapo kuna Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga, nyumba za Serikali za Makao Makuu ya Wilaya zimejengwa tayari, nyumba ya *DC,* Boma na nyumba za watumishi wengine zipo, *wiring* imeshafanyika, lakini umeme haujaweza kuteremshwa kwa sababu hiyo. Naamini pale ilipozungumzwa kwamba Makao Makuu yote ya Wilaya yatapata umeme, chini yake nazidi kusisitiza kwamba tafadhali msitucheleweshe, tungeomba hili lifanyike haraka iwezekanavyo kwa sababu nyumba zile zipo tayari kwa kufunguliwa sasa na ni vizuri zikapata umeme ili ufunguzi rasmi wa nyumba hizo uweze kufanyika haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hivyo, ningependa kueleza kwamba Wilaya ya Mkinga bahati mzuri ina maeneo mengi ambayo yana umeme kutokana na mashamba ya Mkonge, mashamba ya Kakao na mashamba mengine ambayo yalikuwepo hapo zamani. Kwa hiyo, uunganishaji umeme kutoka kwenye mashamba hayo na vijiji mbalimbali si kazi kubwa sana. Ninaamini ndugu yangu Dr. Idrisa Rashid na wenzake wamelisikia hilo na Wizara itatoa msimamo unaostahili ili liweze kufanyika hilo. Naamini hilo litaweza kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi siku ya leo ili niweze kuchangia hoja hii. Pia napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa kuandaa hotuba hii nzuri, ndogo fupi ambayo ni rahisi kuisoma toka mwanzo hadi mwisho pasipo kusimama wala kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitoe pole kwa wale wote waliopatwa na misiba, naamini Mungu atawaponya majeraha mahali walipoumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa wananchi wa Wilaya ya Bukombe kwa kuendelea kuniamini na wana CCM kwa kunipa ushirikiano mkubwa hasa katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee suala la nishati na madini hasa katika upande wa nishati ndipo nitakakoanzia. Najua Waheshimiwa Wabunge wengi waliosimama wameongelea tatizo la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nimejaribu kukiangalia na kuona ni wengi tunapoongelea tatizo la umeme, wengi wanaomba umeme vijijini. Wilaya ya Bukombe haina kabisa umeme Makao Makuu ya Wilaya. Nikawa ninaangalia lakini pia kabla ya kuingia sana kwenye tatizo hilo la umeme Bukombe ambalo wananchi wa Bukombe wamenituma labda niipongeze Serikali kwa kukabiliana na tatizo zito la ukame lililotokea mwaka jana na hatimaye nchi yetu ikaweza kupita katika hali ya uvumilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bukombe tuna tatizo la umeme, ninaamini Serikali inafahamu, Mheshimiwa Waziri anafahamu, kwa sababu hata katika Bajeti ya mwaka jana tulipitisha hapa wakasema kwamba watapeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ikiwemo Bukombe Makao Makuu yake Ushirombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati napitia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, leo ukurasa wa 26 naomba ninukuu amesema kwamba: "Upelekaji wa umeme Makao Makuu ya Wilaya…," zimetajwa Wilaya pale na Wilaya ya Bukombe sikuiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba cha Bajeti cha mwaka 2006/2007 ukurasa wa 13, nitaomba ninukuu kidogo kinasema: "Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika Miji Mikuu ya Mbinga na mingine," Ushirombo ambapo ndipo Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata shida sana nilipoona katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri cha safari hii Bukombe siioni. Sasa napenda labda Serikali iweze kunisaidia. Kwa sababu wengine wanalilia umeme kwenda vijijini, Bukombe tunalilia umeme kwenda Makao Makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Bukombe tuna shida kweli na mpaka ninaendelea kujiuliza pengine labda Serikali inafikiria nini kwa sababu hata katika michango yangu yote ninaposimama sijawahi kuongelea na kusema ahadi za Mheshimiwa Rais. Lakini Mheshimiwa Rais tarehe 8 Oktoba, 2005 alipofika Bukombe alisema maneno yafuatayo:- "Nichagueni mimi, mchagueni Luhahula umeme mtapata." Baada ya kuchaguliwa Bajeti ya mwaka 2006/2007 zikatengwa fedha kwa ajili ya kupeleka umeme Bukombe, lakini leo katika Bajeti hii silioni hilo.

Mheshimwia Mwenyekiti, Waswahili husema siri ya mtungi aijuae kata, niulizeni mimi matatizo ya Bukombe kuhusu umeme. Ninapoongelea tatizo la umeme Bukombe naongea nyuma yangu wapo wananchi laki tano na kitu wanasubiri umeme huo. Halafu kizuri ninaamini Mheshimiwa Waziri ni jirani yangu ili aweze kufika Jimboni kwake

kama ameondoka kwa gari ni lazima apite Bukombe. Kwa hiyo, mimi ninaamini kwa hali hiyo watanikumbuka kupeleka umeme. Kwa sababu mwaka jana niliweza kuandika barua ya kuulizia baada ya kuona umefika mwezi Oktoba, 2006 sioni dalili yoyote.

Nikaiandikia Serikali, nikawaambia nimechoka kujibu maswali ya wananchi Bukombe, hebu ninaomba mnipe majibu. Kwa barua yao ya Kumb. Na.CBD248/324/02 ya tarehe 28 Desemba, 2006 nanukuu kipengele kidogo walisema kama ifuatavyo:- "Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya mradi huo ni shilingi milioni 100 fedha za hapa ndani na shilingi bilioni 2.8 fedha za nje." Ikasema; "Hivyo basi, mradi wa Bukombe/Kagera umepata kiasi chote cha fedha za hapa zilizotengwa kwa utekelezaji wa mradi huo." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Serikali Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake awajibu wananchi wa Bukombe kwa sababu gani hawajaonekana katika kitabu cha hotuba yake, wananchi wa Bukombe wamesahauliwa au wataupata lini umeme huo? Kwa sababu najua umeme huo kama utapatikana kama tulivyoahidiwa kutoka katika kituo cha Irongi utanufaisha kijiji cha Segese, Lunguya, Kanengele, Masumbwe ambapo ni *centre* kubwa sana, Ushirombo Makao Makuu ya Wilaya, Uyovu ukiwa unaelekea kwenye Mgodi wa Tulawaka. Lakini unaweza ukaelekea kwenye vijiji vya Kagera. *(Makofi)*

Naomba hilo sana Serikali itusaidie kwa sababu sasa hivi tunasaidiwa na wafanyabiashara binafsi ambapo *bulb* moja kwa mwezi si chini ya shilingi 8,500/= ni kazi kweli. Lakini uendeshaji wa Halmashauri unaweza ukawa ni mgumu. Naomba kusaidiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee suala la madini, nampongeza Rais wa nchi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati analihutubia Bunge alisema mambo mengi sana kuhusiana na madini. Lakini naipongeza Wizara kwa kazi na jitihada kubwa wanazozifanya kwa sababu katika mambo yaliyosemwa ya kupitia Mikataba upya nimeona katika ripoti ya Kamati ndogo ya Dr. Jonas Kipokolo. Kwa kweli Serikali inafanya kazi na katika mafanikio yaliyotokea ni pamoja na kutoa fedha zinazotolewa kwenye Halmashauri zetu kama ilivyoelezwa, ongezeko la Pato la Taifa, lakini pia mambo ambayo Serikali na wenye Makampuni kama *Barrick* na *Resolute* wamekubaliana. Kwa kweli ni mafanikio makubwa ambayo hayahitaji kubezwa katika Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ni mafanikio ambayo tuna kila sababu ya kuipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika habari ya madini tatizo langu lipo kwa watafiti wa madini. Mwaka jana niliuliza swali hapa Bungeni wapo watafiti katika kijiji cha Nyakafuru maeneo ya Masumbwe inaitwa *Resolute* hao watafiti wapo pale zaidi ya miaka 10. Serikali mwaka jana wakati nauliza swali walisema kwamba leseni yao itaisha mwezi Julai, 2007, lakini watafiti hao ukiongea nao wanasema hawana mashapo ya kutosha ya kuwekeza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na ujenzi wa sekondari katika Kata moja ya Bukandwe, sekondari ile tumeijenga tumemaliza boma, wale watafiti wakaja wakasema hapa ni sehemu yao, wakalipa gharama zote wakasema nendeni mkajenga sehemu nyingine. Sasa hao watafiti najiuliza wamekosa dhahabu au bado wapo na kwa nini Serikali isifikie hatua hao watafiti wapangiwe muda. Kwa sababu sasa wananchi wa maeneo yale hawafaidiki, wananchi wa Nyakafuru kabla ya kuwepo watafiti hao walikuwa wanachimba dhahabu, walikuwa wanapata dhahabu kidogo kidogo, sasa hivi wananchi wa pale wamekaa. Kila ninapokuwepo ofisini unakutana na maandamano ya wananchi kutoka pale wanakuja kwangu kunieleza jinsi wanavyopata shida. Naomba Serikali itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wachimbaji wadogo wadogo. Tunaiomba Serikali iwasaidie na nilikuwa naomba sana nililiongea hata mwaka jana wapo wachimbaji maeneo ya Matabe ipo Kagera, Biharamulo, lakini wananchi wanaochimba pale wengi wanatoka Bukombe na wakati wa kampeni kabla hawajahamia Kagera nilienda kufanya kampeni pale. Tunaiomba Serikali ikiwezekana eneo lile litengwe liwe eneo la wachimbaji wadogo wadogo wa Kanda ile watafaidika sana pale, kwa sababu kama ni msitu mbona mgodi wa Tulawaka upo ndani ya hifadhi. Lakini wapo watafiti wengine kwenye pori la Kigosi/Mnyowosi wanatafiti. Naomba sana hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee mgodi wa Tulawaka. Mgodi wa Tulawaka upo kilomita chini ya 10 kuingia katika Wilaya ya Bukombe. Wafanyakazi wa Tulawaka wanaishi katika kijiji cha Uyovu ambacho kiko Jimboni kwangu ndiyo *centre* yao. Wanapata huduma za matibabu katika Kituo cha Afya cha Uyovu. *(Makofi)*

Naomba Serikali inisaidie, wamechangia kiasi gani katika eneo lile. Kwa sababu wanaishi pale hawana *contribution* zozote pale, kwa hiyo, naomba Serikali itusaidie sana ili tuone na hii ndiyo kudumisha mahusiano na jamii na vile vile hata katika sekta za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nirekebishe kwenye kitabu Taarifa za Takwimu ukurasa wa 49 pawepo na marekebisho. Mwaka jana nilisema lakini bado pia kuna makosa. Kuna vijiji ambavyo...

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ungetusaidia labda ni kitabu gani kwa sababu tunatumia vitabu vingi, ili kuweka rekodi sawa sawa ni muhimu ukatuambia kitabu gani unachokitumia cha kufanya marekebisho.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Taarifa za takwimu muhimu kuhusu sekta za nishati na madini kilichotolewa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 49 kuna vijiji ambavyo vinatamkwa ni vijiji vya Wilaya ya Kahama panapopatikana madini. Vijiji hivyo ni Nungwiza lakini hivyo vijiji viko Bukombe. Kijiji cha Ushirombo ni Bukombe tena ni Makao Makuu ya

Wilaya. Kijiji cha Kanegele. Kwa hiyo, nilikuwa naomba wataalamu wasahihishe ili taarifa zingine zisomeke kwamba ni Bukombe na sio Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sana Serikali itusaidie kabisa, itufafanulie wananchi wa Bukombe awajibu kwamba umeme wao wataupata lini na ile ahadi ya Rais iliyosemwa iweze kuaminika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nakushuru sana Mheshimiwa Luhahula na hasa kwa kutunza muda vizuri. Kwa hiyo, tunaweza kupata nafasi Mheshimiwa Ernest Mabina naye akatoa mchango wake. Mheshimiwa Mabina tafadhali unisamehe kwa kukushtua lakini muda upo na unaweza ukachangia mada hii. Karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ingawa nilikuwa sina taarifa kama ningeweza kuchangia kama ilivyo ada, nafikiri Mheshimiwa Mbunge inabidi ajitayarishe kwa kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa rambirambi zangu kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wameshapoteza maisha yao humu Bungeni, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kuchelewa ningependa tu niipongeze hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Ni hotuba nzuri ambayo kila Mbunge amejaribu kuisifia hapa. Lakini tukiangalia katika maeneo mbalimbali kila Mheshimiwa Mbunge anachangia kutokana na tatizo kubwa la umeme hapa nchini. Sisi wananchi wa Geita tuna tatizo la umeme. Umeme tulioupata ni mdogo sana. Unafika katika majumba mengine unawaka kama kibatari kiasi ambacho hata kuweza kuonana unaweza ukashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba umeme katika Wilaya ya Geita ni muhimu sana. Kwanza kabisa pale kuna mgodi mkubwa wa *Geita Gold Mine* ambao unahitaji kupata umeme mwingi ambao unaweza ukaendesha mashine zilizoko pale. Tatizo hili limetokana na kutokuthamini uzalishaji ambao unatokea pale. Sasa unajikuta kwamba Mgodi wa Geita uendeshaji wake unakuwa ni mkubwa sana ukilinganisha na mafuta yanayotumika pale. Kama wangekuwa wanatumia umeme gharama yake ingekuwa ni ndogo sana. Naiomba Serikali ilete umeme wa gridi katika Mji wa Geita na ningeshukuru sana kama Waziri angeweza akatamka katika majumuisho yake kwamba lini umeme utaingia katika Wilaya ya Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri ajaribu kufikiria hata miji midogo kama Kasamwa. Kasamwa waliteremsha umeme wakaweka *transformer* lakini walipewa wananchi 12 tu, maombi yaliyoko pale ni zaidi ya mia moja. Sasa hao wananchi mnategemea watafanya nini? Kila ninapowaambia wanasema hali ya fedha sio nzuri itakuwa nzuri lini? Lakini ukiangalia

utakuta kwamba kuna sehemu ambazo umeme unapelekwa. Naomba Kasamwa tupewe umeme wa uhakika, kwa sababu kuna taasisi nyingi, kuna kituo cha afya pale, kuna shule ya sekondari, kuna Makanisa makubwa pale sasa tukipata umeme nina uhakika kabisa kwamba Kasamwa wanaweza wakaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ninakumbushia tu kwamba Waziri alipokuja Geita alizungumza na wananchi wa Katoma, walikuwa wanamdai fidia. Fidia hii sielewi watalipwa lini? Kuna wananchi 553 ambao tayari wameshatathminiwa lakini kuna wananchi watatu tu ambao wamepeleka kesi Mahakamani. Sasa hebu Serikali iangalie iweke uwiano kipi ni kizuri kwa sababu hawa wananchi wa Geita wa sehemu ya Katoma utakuta kwamba wamekaa hawana uzalishaji wa aina yoyote. Hawana tegemeo lingine zaidi ya kutegemea fidia. Hebu jifikirie na wewe kwamba kwa mfano mwezi huu wa Julai, mtu hapa hajapata mshahara wake anategemea kwamba ataupata baada ya wiki moja, hapati, baada ya wiki moja inapokwisha unakuja mwezi hapati, utajisikiaje hata wewe ukiwa hapa Mbunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi wa Katoma wamekaa pale hawana fedha, hawajui watalipwa lini, lakini Serikali imekaa kimya. Kwa nini msifanye juhudi za ziada wakalipwa wale wananchi 553 basi hawa watatu waliopeleka kesi zao Mahakamani wakafikiriwa baadaye? Lakini tukiwaadhibu hawa wananchi 553 nafikiri mtaangalia kabisa kwamba wakati tulipokuwa tunawasiliana na Waziri kwenye vipindi vya televisheni wanatoa wale wananchi wana hali mbaya, hawalimi, hawana tegemeo lolote hawajui watakwenda wapi. Lakini kibaya zaidi utakuta kwamba hao wananchi wa sehemu za Katoma na sehemu zingine ambazo zinahitajika fidia unakuta kwamba hawana ule upeo waelekee wapi. Nazungumza haya kutokana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakati mgodi wa Geita unakuja pale waliwaahidi wananchi kwamba ndio mmepata neema na wakawa na matumaini kwamba watafaidika na mgodi. Baada ya kuja mgodi wananchi wa Geita hawajafaidika lolote, kila siku ni mateso kupata fidia mpaka Mbunge ahangaike alie. Mwaka 2002 mpaka tulilia ndio watu wakapata fidia yao. Sasa vilio hivi vitaisha lini? Naomba Serikali iwafikirie wananchi wa Geita maeneo ya Katoma na maeneo mengine kama Nyamatakata kulikuwa na wananchi 111 ambao walikuwa wamefidiwa wakalipwa wananchi 40 tu. Wananchi 71 wakabaki bila ya malipo mpaka leo hii. Serikali ipo, haiwajali wananchi ambao ndio Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba wananchi hawa wa Katoma na sehemu za Nyamatakata walipwe. Bila kulipwa hatutaelewana na wana Geita kwa sababu ni fidia ya muda mrefu, zile fomu zimeshajazwa ziko pale zinasubiri malipo, sasa haya malipo kwa nini hawalipwi? Ni kitu cha kusitikitisha kwa kweli. Mtu hata ambaye hajui kuzungumza anaweza akazungumza ukajisikia kwamba huyu amechanganyikiwa au vipi lakini anazungumza kwa uchungu akiona kwamba kuna watu ambao wanamtegemea hawajatendewa haki yao. Naomba Serikali ilifikirie hili walipwe wananchi wa Katoma. Wako wananchi 553 wamekubali na wanasema kwamba sisi watulipe hizi fedha basi. Kama waliobaki hawa watu watatu ambao wamepeleka kesi yao Mahakamani basi wajuane na Serikali. Sasa kwa nini hawa wananchi kilio cha wengi ni kilio cha Mwenyezi Mungu. Tuwasaidie hawa wananchi bila ya kuwasaidia na huwa tunasema

migogoro haianzi kwa kitu kikubwa inaanza kwa kitu kidogo hatutaki kufika katika migogoro. Naomba sana kwa Serikali hii iweze kunifikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka kuzungumzia adha inayowapata wananchi wa Geita. Tarehe 28 Novemba, 2006 bila kutegemea ilikuwa saa 10.00 jioni wananchi wa Geita walipata mshtuko mmoja mkubwa sana, watu wa Mgodi wa Geita walikuja wakalipua maeneo ya Katoma. Wananchi wale wengine walikuwa wazee walizimia wakalazwa hospitali, kuna nyumba zilipasuka Mheshimiwa Waziri tulikwenda naye akaona maeneo yale na tulifanyia kikao kule kule katika maeneo ambayo yameathirika lakini utakuta kwamba katika hali isiyoweza kujulikana au kueleweka wananchi wale wameachwa hivi hivi wala hakuna mtu ambaye anaweza akasema kwamba watapata nini kutokana na mshtuko ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba yafuatayo, kwa sababu Mji wa Geita uko katika eneo la machimbo, nilikuwa naomba wananchi wote ambao wamezunguka pale wafidiwe, waondoke maeneo ya Mgodi ili kupisha ule Mgodi. Wasipofanya hivyo utakuta kwamba kero kila siku zitakuwepo. Naomba wananchi wa sehemu ya Katoma yenyewe wahamishwe, sehemu za Katani, Magema na Nyakabale wahamishwe, lakini bila hivyo utakuta kwamba migogoro haitaisha Geita la sivyo utakuta kwamba hata mtu mwingine atakwenda kuchukuwa umaarufu wake maeneo yale kule na msishangae utakuta mtu anazungumzia suala la Geita wakati sio Mbunge wa kule, je, utajiuliza hilo ni nini? Watu wanatafuta umaarufu kama ule lakini *solution* kubwa ni kuwahamisha wananchi ili kuweza kuleta usalama katika mji wetu wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo lilikuwa ni wazo langu lakini ndio ufumbuzi wa kuweza kuwasaidia wananchi wa Geita. Bila hivyo utakuta kwamba ndio tulipata taarifa kwamba kuna ng'ombe sijui wangapi wamekufa na nini na nini, lakini wale ng'ombe hawakuwa wananchi waliokufa hivi juzi. Wale ng'ombe baada ya sakata la kule Uganda kuhamisha ng'ombe na nini wale ng'ombe walitembea kwa mguu mpaka wakaja katika pori la Geita wakaja wakaishia kwenye mgodi pale. Sasa ndio wanazagaa zagaa maeneo ya pale sio wa wananchi. Nilikuwa naomba kwa hali hiyo Serikali iweze ikafikiria hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka kuzungumzia wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa ni watu wa kuhangaishwa. Wakiona sehemu ambapo kuna dhahabu kwa sababu ndio wavumbuzi wa dhahabu hakuna anayevumbua dhahabu zaidi ya hao wachimbaji wadogo wadogo. Wakishavumbua unakuta kwamba wawekezaji ndio wanakuja. Wakishakuja pale hawa wanafukuzwa wanakosa sehemu ya kukaa. Mheshimiwa Luhahula amezungumza hapa kwamba kuna wananchi ambao wamehamishwa Matabe sasa hivi wako Geita sehemu ambayo nimeizungumza ya Nyamatakata. Wamejaa sehemu ile wanahitaji hifadhi ya Serikali. Nilikuwa naomba tu wameshaleta maombi yao hawa wachimbaji wadogo wadogo angalau waruhusiwe kuchimba katika leseni kubwa ya *GGM.* Sasa kama hiyo itatoka nitashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona shughuli ambazo tulikuwa nazo katika jioni ya leo zote zimekamilika kwa maana

ya muda. Tutaendelea na mjadala huu Jumatatu na kadri ya utaratibu nafikiri niwataje angalau wasemaji wawili wa mwanzo ili tuone ratiba itakavyopangwa Jumatatu tutafanya nini.

Tumeishia leo na Mheshimwa Ernest Mabina, siku ya Jumatatu kama tutaendelea na shughuli hii ya kuchangia mada ambayo imewekwa mbele yetu tutaanza na Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa atakuwa ni msemaji wetu wa pili, lakini ninaomba tusubiri utaratibu wa *Order Paper* ya Jumatatu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo mengine mawili, matatu hapa kabla sijaahirisha shughuli zetu. La kwanza ni taarifa ya mchezo wa mpira kati ya timu ya Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa dini. Nimeombwa na Mheshimiwa Joel Bendera, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kesho tarehe 14 Julai, 2007 kutakuwa na mchezo wa mpira wa miguu kati ya timu ya Waheshimiwa Wabunge na timu ya viongozi wa dini hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mchezo huo utafanyika katika Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 9.00 mchana. Waheshimiwa Wabunge tunaombwa wote tuhudhurie kuishangalia timu yetu na kwa taarifa nilizonazo hapa mezani kwamba Kamati ya ufundi na ushindi itaongozwa na Mheshimiwa Manju Msambya na chini ya uongozi wa Mheshimiwa Msambya basi tunaamini kabisa ushindi wa timu yetu ni mkubwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tangazo la pili, ni kwamba kesho tutakuwa na semina ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na itaanza saa 3.00 asubuhi. Kwa hiyo, tunaombwa tuhudhurie na nafikiri tunafahamu wote tunaangalia ni namna gani Serikali imejipanga katika azma ya kuongeza ajira kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuhudhurie semina hiyo ili tuweze kushirikiana na Serikali kuona nini kinatakiwa kufanyika. *(Makofi)*

Lakini Waheshimiwa Wabunge, nimekuwa hapa nikipata pia maoni mbalimbali kuhusiana na siku ya kesho tarehe 14 Julai, 2007 tunafahamu kwamba Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete atazindua rasmi Kampeni ya Kitaifa ya Upimaji wa UKIMWI kwa hiari katika nchi yetu.

Kwa hiyo, nimekuwa nikipokea maoni mbalimbali ya namna moja ama nyingine kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na hivyo nilimwomba Mheshimiwa Naibu Spika anisaidie kupata mwongozo kutoka kwa Spika ili niwape taarifa rasmi Waheshimiwa Wabunge.

Naomba niwape sasa taarifa rasmi, Mheshimiwa Spika, amemwagiza Mheshimiwa Naibu Spika aniagize Mwenyekiti wa Bunge nitangaze kuwa shughuli za kupima afya zetu hazitafanyika siku ya kesho zikiendana sambamba na uzinduzi wa Kampeni hiyo utakaofanywa na Mheshimiwa Rais, lakini kabla ya kumaliza Mkutano huu wa Bunge, Bunge litaandaa utaratibu rasmi wa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais

katika Kampeni hii ya Kitaifa ya Upimaji. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nafikiri siku hiyo itakapofika wote tutashiriki kwa kikamilifu kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, labda tu nitoe tangazo lingine kwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Jumapili saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 122 kutakuwa na Kikao cha Kamati kwa ajili ya kujadili masuala ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, naomba wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, siku ya Jumapili wasikose kuhudhuria katika kikao hicho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa matangazo hayo sasa kama niliyosema shughuli zetu zimefikia mwisho na naomba niahirishe shughuli za leo na tukutane tena siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi katika ukumbi huu. Ahsanteni sana.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 16 Julai, 2007 saa tatu asubuhi)*